

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Arobaini – Tarehe 30 Mei, 2018**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae, Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MADINI (MHE. DOTO M. BITEKO):**

Randama ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Madini kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN- KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Maswali Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu swali la Mheshimiwa Katherine Nyakao Ruge, litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Khadija.

Na. 331

### **Tatizo la Ajira kwa Vijana**

**MHE. KHADIJA N. ALI (K.n.y. MHE. CATHERINE N. RUGE)**  
aliuliza:-

Pamekuwa na wimbi kubwa la ukosefu wa ajira kwa sasa huenda kuliko wakati mwingine wowote tangu nchi yetu ipate uhuru, wahitimu wa tangu mwaka 2015 hawajaajiriwa na Serikali mpaka sasa, sekta binafsi nazo kila kukicha zinapunguza wafanyakazi na kutoajiri wapya:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuhakikisha ajira zinapatikana kwa vijana hawa ambao hawajapatiwa elimu ya kutosha ya kujajiri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha tunakabiliana na changamoto za ukosefu wa ajira nchini Tanzania Serikali ina mikakati ifuatayo:-

(i) Kuongeza fursa za wigo mpana wa nafasi za ajira kupita sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo uwekezaji katika uchumi wa viwanda na utekelezaji wa miradi mikubwa kama ilivyoainishwa katika Mpango wa Pili wa Maendeleo nchini;

(ii) Kutekeleza Programu ya Taifa ya kukuza ujuzi inayowezesha Nguvu Kazi ya Taifa kuwa na ujuzi stahiki na kutoa fursa kwa vijana kuwa na sifa ya kuajirika na kujajiri;

(iii) Kuendelea kusimamia vijana kujunga katika makampuni, ushirika na vikundi vyatuzishaji mali ili

kupatiwa fursa ya mikopo yenyewe masharti nafuu kupitia Mifuko ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kwa lengo la kuwaongeza mitaji ya kufanya shughuli za kiuchumi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija.

**MHE. KHADIJA N. ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, hotuba ya Wizara ya Viwanda na Biashara ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2018/2019 ilieleza kwamba tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani imeshajenga viwanda 3,036. Je, ni vijana wangapi wameweza kuajiriwa katika viwanda hivyo mpaka sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili, pamoja na juhudhi nyingi ambazo Serikali inazifanya katika kuhakikisha vijana wanapata ajira na nyezo za kujiajiri. Ripoti ya *UN Tanzania* ya 2018 inaonesha kwamba kati ya vijana 87 ni vijana wanne tu ambao wanaweza kujikimu kiuchumi, hili suala linazidi kuwa baya au linazidi kuwa gumu siku hadi siku. Je, Serikali sasa ina mpango gani wa dharura kuweza kuwanusuru vijana katika udumavu huu wa kiuchumi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema tu kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Khadija kwa kazi kubwa anayoifanya kuwasimamia vijana wa nchi hii na amekuwa mtetezi wa kweli wa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza, ametaka kujua idadi ya vijana walioajiriwa katika viwanda. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sababu idadi hii ya walioajiriwa kwenye viwanda siwezi kuipata hapa ndani Bungeni hivi sasa, lakini nitakachokifanya nitahakikisha kwamba tunafanya *coordination* na wenzetu kuweza kujua

katika viwanda hivyo ambavyo vimeanza kutoa ajira kwa vijana ni asilimia ngapi ya vijana ambao wameshapata ajira mpaka hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mchango mkubwa wa sekta ya viwanda, tunaamini kabisa kundi kubwa la vijana ndiyo hasa waliopata nafasi ya kuajiriwa kwa sababu katika nguvu kazi yetu ya nchi Tanzania tuliyonayo asilimia zaidi ya 65 ni vijana, kwa hiyo automatically hapa kundi kubwa ambalo watakuwa wamepata ajira ni vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni namna gani Serikali tunakuja na mpango wa kukwamua vijana kutokana na udumavu wa kipato...

**MWENYEKITI:** Kwa kifupi Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango tuliyonayo mikubwa kabisa ni kuhakikisha kwamba tunawashirikisha vijana katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Lengo letu ni kuwapatia fedha za Mifuko ya Uwezeshaji ili wafanye shughuli za kiuchumi za kuweza kujisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huo ndiyo mkakati mkubwa wa Serikali kwa sasa. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima Bulembo, jiandae Mheshimiwa Amina Mollel.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 iliahidi kujenga *VETA* katika kila Wilaya. Je, ni lini sasa Serikali itaanisha mkakati wa kujenga *VETA* katika kila Wilaya ili kuwasaidia vijana kupata ujuzi wa kuweza kujiajiri? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kama alivyosema kwamba llani ya Chama cha Mapinduzi imeainisha kwamba Serikali itajenga VETA katika kila Wilaya. Serikali imeanza ujenzi wa VETA katika baadhi ya Wilaya na mpango upo wa kujenga VETA katika kila Wilaya na kila Mkoa, lakini tunajenga kadri fedha zinavyopatikana. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba mpango upo pale pale. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Amina Mollel, jiandae Mheshimiwa Emmanuel.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Miongoni mwa vijana wapo pia vijana wenye ulemavu na tunaposema kwamba tatizo la ajira kwa vijana, basi vijana wenye ulemavu ndiyo waathirika namba moja. Nataka kufahamu katika mkakati huu wa sasa kwamba Tanzania ya viwanda. Je, ni mikakati gani ya haraka Serikali inaandaa katika kuhakikisha kwamba vijana wenye ulemavu nao wanakuwa ni sehemu ya ajira na hawaachwi nyuma katika kuendeleza gurudumu la maendeleo hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (*Makof!*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mipango yote ya Serikali hasa ya ukuzaji ujuzi, yenye lengo la kumfanya kijana wa Kitanzania aweze kusimama kiuchumi na aweze kuwa na sifa za kujajiri na kuajiri vijana wengine. Mkakati wetu ni kuhakikisha kwamba katika kila mpango kundi la watu wenye ulemavu wanajumuishwa ili na wao pia wapate fursa ya kupata ujuzi stahiki ambao watautumia katika uchumi huu wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba katika progamu iliyoko chini

ya Ofisi ya Waziri Mkuu ya ukuzaji ujuzi kwa vijana ambao lengo lake ni kuwafanya vijana hao kuwa na sifa za kwenda kufanya katika viwanda, kundi la watu wenyewe ulemavu wanajumuishwa na tumetenga asilimia kadhaa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba kila programu imguse na mtu mwenye ulemavu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emmanuel.

**MHE. ADAMSON E. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Katika hii Mifuko ambayo wanakopeshwa vijana, kumekuwa na tatizo kubwa la wale wanaokopeshwa kurudisha mikopo hiyo ili na wengine waweze kukopa. Je, Serikali ina mpango gani mahsusini kuhakisha wale wanaokopeshwa wanarudisha ile mikopo ili na wengine waweze kukopeshwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA)** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunao Mfuko wa Maendeleo ya Vijana ambao umekuwa ukitoa fedha za mikopo kwa makundi mengi ya vijana na kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge wapo baadhi ya vijana kupitia makundi hayo wameshindwa kurejesha fedha hizi kwa wakati. Tunachokifanya ni kuwasiliana na Halmashauri husika ambao tunafanya kazi kwa pamoja kuhakikisha kwamba wanaendelea kutoa elimu kwa makundi haya ya vijana kwa sababu fedha ile si fedha ambayo inatakiwa tu watu wapewe na ibaki hivyo hivyo, ni pesa ambayo ni *revolving*. Kwa hiyo, tunaendelea kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumekuwa tukifanya kaguzi za mara kwa mara kuwahimiza vijana hawa kuendelea kurejesha fedha, mpaka ninavyozungumza hivi sasa makundi makubwa ya vijana wameelewa na wameanza kurudisha fedha hii kwa ajili ya kuwafanya vijana wengine waweze kukopeshwa pia.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Michael Mkundi kwa niaba, Mheshimiwa Mabula, mwenyewe alitoa maagizo swali lake aulize Mheshimiwa Mabula.

Na. 332

### **Ujenzi wa Kituo cha Afya Nakutunguru**

**MHE. STANSLAUS S. MABULA (K.n.y. JOSEPH M. MKUNDI)** aliuliza:-

Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe (Nansio) inakabiliwa na msongamano wa Wagonjwa; Mwaka 2002 Halmashauri ya Wilaya ilitumia zaidi ya shilingi milioni 200 kuanza ujenzi wa Kituo cha Afya Nakutunguru kama njia ya kupunguza msongamano huo. Hata hivyo, ujenzi huu haujakamilika kutokana na ukosefu wa fedha:-

Je, Serikali ipo tayari kuondoa upungufu uliopo ili Kituo hicho kianze kutoa huduma?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Serikali ilitoa fedha kiasi cha shilingi milioni 200 kupitia fedha za Ruzuku ya Maendeleo kwa Serikali za Mitaa yaani (*Local Government Development Grant*) mwaka 2012 kwa ajili ya kuanza kwa awamu wa kituo cha Afya Nakutunguru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo hilo *OPD* ulikamilika mwezi Aprili, 2015 na lilizinduliwa rasmi tarehe 18 Februari, 2018 na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. Mpaka sasa

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

kituo hiki kinafanya kazi kwa kutoa huduma kwa wagonjwa wa nje (*OPD*) na huduma za Mama, Baba na Mtoto (*Reproduction and Child Health (RCH)*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa Fedha 2018/2019, Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe imeidhinishiwa jumla ya shilingi milioni 45 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya watumishi wa Kituo hiki. Kwa sasa Serikali ipo katika awamu ya nne ya utekelezaji wa mpango wa ukarabati wa Vituo vya Afya nchini, hivyo tutakiingiza Kituo cha Afya Nakutunguru katika awamu zijazo ili kuhahakisha kinakamilika na kutoa huduma zote ikiwemo huduma za upasuaji kwa akinamama wajawazito.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada kubwa za Serikali kuititia Wizara yake ya TAMISEMI kuhakikisha inaboresha vituo vingi vya afya kikiwemo na Kituo cha Afya hiki cha Ukerewe, kama Mheshimiwa Waziri anavyofahamu kwamba kumekuwa na changamoto kubwa ya watumishi, vifaa tiba ambavyo kwa kweli vingesaidia zaidi ufanisi na ubora wa utumishi kwenye hospitali hii. Je, ni lini hasa Serikali itahakikisha suala hili linafanyiwa kazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali dogo la pili, kwa sababu matatizo ya Ukerewe kwa namna fulani yanafafana sana matatizo yaliyoko kwenye hospitali ya Wilaya ya Nyamagana. Ni nini sasa mpango wa Serikali kwa sababu mara kadhaa hospitali ya Wilaya ya Nyamagana imeshaomba kupatiwa vifaa kama *ultra sound* na ni lini sasa Serikali inaweza kuhakikisha hospitali ya Nyamagana inapata *ultra sound* pamoja na *X-Ray machine*?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi, anataka kuua ni lini tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, anauliza kuhusiana na Kituo cha Afya Nakutunguru kukamilika na hasa kuwepo na vifaa vya kutolea huduma, pamoja na suala zima la watumishi. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba vituo vya afya vyote vinavyokamilika ni pamoja na kuwa na vifaa vya kufanya kazi ikiwepo *X-Ray, ultra sound* hayo yote ni muhimu ili kituo cha afya kiweze kukamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalii lake la pili anaulizia hospitali yake ya Wilaya. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mabula amekuwa akipigania hospitali hii kwa muda mrefu kuhakikisha kwamba inatoa huduma kwa kadri inavyokusudiwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba hospitali zote za Wilaya zinakuwa na vifaa vya kutosha ili viweze kutoa huduma inayotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni azma yetu kuhakikisha kwamba hospitali ya Nyamagana ni mionganini mwa hospitali za Wilaya ambazo zitakua kwa viwango vinavyotakiwa ikiwa ni pamoja na kuwa vifaa vyote vinavyotosheleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Kwanza, naishukuru sana Serikali kwa kuweza kunipatia fedha za Kituo cha Afya cha Mwese na Kituo cha Afya cha Mishamo. Tatizo ambalo lipo kwenye eneo la Wilaya ya Tanganyika vituo vya afya havina Wahudumu na Madaktari kwa ujumla. Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari ili waweze kufanya kazi iliyokusudiwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kakoso anafahamu kabisa kwamba sasa hivi Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeshatangaza nafasi kwa

ajili ya watu wa afya wakiwepo Madaktari, Wahudumu, Manesi. Naomba nimhakikishie katika hawa ambao watakuwa wameajiriwa na naamini kwamba na wengi watakuwa wameomba wakiwa wanatokea maeneo huko ili pale wanapopewa nafasi ya kwenda kufanya kazi wasije wakasema mazingira yale kwao ni mageni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namhakikisha Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni wajibu wa Serikali kuhakikisha Watumishi tunawasambaza ili wakatoe huduma kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi, ajiandae Mheshimiwa Catherine.

**MHE. RASHID A SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Halmashauri ya Lushoto na hospitali ya Wilaya ya Lushoto inahudumia Majimbo matatu na Halmashauri mbili kwa maana ya Lushoto na Bumbuli na inakabiliwa na msongamo mkubwa sana wa wagonjwa. Je ni lini sasa Serikali itaipa fedha ili kupanua huduma hizi za afya katika Wilaya ya Lushoto?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, naomba majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba Wilaya ambayo Mheshimiwa Mbunge anaitaja ina *population* kubwa. Pia ni ukweli usiopinga kwamba Halmashauri wanajua uhitaji, naomba kwa kushirikiana na Halmashauri na hasa Mheshimiwa Mbunge akiwa wa kwanza kuelekeza namna ilio bora ya kuhanikiisha maeneo mengi vituo vya afya vinajengwa hasa kwa kushirikisha wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni vizuri kama ni suala la ujenzi wa vituo vingine ili kuweza kutoa nafasi kwa hospitali ya Wilaya, wazo hilo jema ni vizuri likaanza kwao na sisi Serikali tutaunga mkono jitihada za wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza Swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Ngorongoro Mkao wa Arusha hususani Loliondo wamekuwa wakitegemea hospitali ya Waso kwenye matibabu na hali hii inapelekea msongamano mkubwa katika hospitali ya Waso. Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kujenga hospitali ya Wilaya ya Ngorongoro?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ni lini, bajeti mshapata unamwambia tu mchakato unaendelea. (*Kicheko*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Magige ni shuhuda kwamba tumeweza kujenga hospitali ya Wilaya Arusha pale na Vituo vya Afya vingi ikiwepo na Murieti na yeze ni mionganoni mwa watu ambao wamekuwa wakipigania suala zima la afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimhakikishie tumeanza na hospitali 67, tukishamaliza hizo 67 tutaenda maeneo yale ambayo hakuna hospitali za Wilaya ili kupunguza mlundikano kwa wananchi kupata huduma.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara hiyo Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene.

Na. 333

### **Kugawanya Kijiji cha Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza:-

Kata ya Bukene Wilayani Nzega inaundwa kwa Kijiji kimoja tu chenye wakazi zaidi ya 7,600 jambo ambalo linakwamisha uharakishaji wa huduma za maendeleo kwa

***NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)***

wananchi. Tulishafuata taratibu zote za kuomba Kijiji cha Bukene kigawanywe ili kupata Kijiji kingine kipywa:-

Je, Serikali haioni kuwa siyo sahihi kuwa na Kata inayoundwa na Kijiji kimoja?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Selemani Jumanne Zedi, Mbunge wa Bukene, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu za kuzingatiwa wakati wa kuanzisha au kupandishwa hadhi maeneo ya utawala zimeelezwu katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) Sura ya 287 na (Mamlaka za Miji) Sura 288, Toleo la 2002. Sambamba na taratibu hizo upo mwongozo uliofanyiwa marekebisho mwaka 2014 unaofafanua vigezo vya kuzingatiwa katika kuanzisha maeneo hayo ili kuepusha uanzishwaji holela wa maeneo ya utawala yasiyokuwa na sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipo vigezo vinavyopaswa kuzingatiwa katika kuanzisha vijiji. Mapendekezo ya kugawanywa kwa Kijiji cha Bukene kilichopo katika Kata ya Bukene, Halmashauri ya Wilaya ya Nzega hayajawasilishwa rasmi kwa kuzingatia taratibu zilizopo kisheria ikiwa ni pamoja na kujadiliwa na kuitishwa katika vikao vyote vya kisheria ambavyo ni Serikali ya Kijiji, Mkutano Mkuu wa Kijiji, Kamati ya Maendeleo ya Kata, Baraza la Madiwani, Kamati ya Ushauri ya Wilaya na Kamati ya Ushauri ya Mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kipaumbele cha Serikali kwa sasa siyo kuanzisha maeneo mapya ya kiutawala bali kuimarisha maeneo ya kiutawala yaliyopo ili yaweze kutoa huduma stahiki kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana taarifa kwamba mchakato huu wa kuomba Mji wa Bukene upandishwe hadhi ulianza siku nyingi na mpaka Wizara ikatoa *GN* Namba 176 ya mwaka 1996 ambayo mpaka sasa haijafanyiwa mchakato wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kwenye swali langu la msingi niliuliza, je, muundo wa kuwa na Kata moja inayoundwa na Kijiji kimoja tu ni sahihi? Kwa sabbau muundo huu unapelekea Mtendaji wa Kijiji kutokuwa na tofauti yoyote na Mtendaji wa Kata na Serikali ya Kijiji haina tofauti yoyote na *WDC* na ni sawa sawa na kuwa na Mkoa mmoja unaoundwa na Wilaya moja tu ambayo kutakuwa hakuna tofauti yoyote ya Mkuu wa Wilaya na Mkuu wa Mkoa, kwa sababu mkoa ni mmoja na Wilaya ni mmoja. Je, muundo huu ni sahihi kuwa na Kata moja ambayo inaundwa na Kijiji kimoja tu? (*Makof!*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza ananiuliza kama najua kwamba kuna *GN* ambayo ilikuwa imetolewa na kwamba mpaka sasa hivi *GN*hiyo haijafanyiwa marekebisho yoyote, taarifa hiyo ninayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, anauliza uwezekano wa Kijiji hicho kimoja kikawa Kata, naomba nitoe ufanuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Zedi anajua kwamba ilikuwa mchakato wa kupandisha Kijiji cha Bukene kuwa Halmashauri ya Mji Mdogo na Bukene kama ilivyo ina vitongoji vyake 11 na lengo lilikuwa hivyo Vitongoji vije vibadilike kuwa Mitaa ambayo ingeweza kutosha katika kubadilisha sasa kuwa na Mamlaka ya Mji Mdogo wa Bukene. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Selemani Zedi, taratibu hizo zingine ziendelee ili ukifika wakati ambapo Serikali

itakuwa tayari kuongeza maeneo ya kiutawala na Bukene iwe na sifa ya kuweza kuongezeka.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Monko, jiandae Mheshimiwa Massala.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kijiji cha Ndwamughanga kilichopo katika Jimbo la Singida Kaskazini kina vitongoji ambavyo viro Mukulu ambavyo viko kilomita 23 kutoka Makao Makuu ya Kijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukiomba Vitongoji hivi visajiliwe kama Kijiji kwa muda mrefu. Je, ni lini Vijiji hivi vyta Mukulu vinaweza kupata usajili wa kuwa kijiji kinachojitegemea ukizingatia umbali ili wananchi waweze kupata huduma za Kiserikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anasema kuna Kitongoji ambacho kipo kilomita 20 kutoka katika Kijiji ambacho ndiyo kimezaa hicho Kitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sifa za Kitongoji kutoka katika Kitongoji kuwa Kijiji sasa sina uhakika na sifa ya hicho Kitongoji ambacho kinalazimika kufuata huduma ya kilomita 20. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwa kuzingatia vigezo na sifa za kitongoji kubadilika kuwa kijiji pindi zitakapokuwa zimekamilishwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI haitasita kuhakikisha kwamba Kitongoji hicho kinakuwa Kijiji kama sifa stahiki zinakidhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Masala.

**MHE. HASSAN E. MASALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Wilaya ya Nachingwea ina jumla ya Kata 36 na

tayari inakidhi vigezo nya kupata Majimbo mawili ya uchaguzi na taratibu zote tumeshazifluta. Ni lini Wizara ya TAMISEMI itakwenda kuligawanya Jimbo la Nachingwea ili liwe na Majimbo mawili ya uchaguzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri mwaka 2020 inaingia hiyo. Kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kwenda Wilaya ya Nachingwea na Jimbo la Nachingwea, kwa hiyo najua ambacho Mheshimiwa Mbunge anaongelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo taratibu ambazo zinatakiwa zifuatwe ili Jimbo ligawanywe na hii huwa inapelekwa kwenye Tume ya Uchaguzi ndio wenyewe mamlaka ya kugawanya Majimbo na siyo Ofisi ya Rais, TAMISEMI.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, Wizara hiyo hiyo Mheshimiwa Edwin Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini.

Na. 334

### **Hitaji la Gari la Wagonjwa Hospitali ya Mji-Kondoa**

**MHE. EDWIN M. SANNDA** aliuliza:-

Pamoja na kuhudumia wagonjwa wengi wakiwemo watokao Wilaya ya Kondoa, Chemba, Kiteto, Babati na wakati mwingine hata Hanang', lakini Hospitali ya Mji wa Kondoa haina gari la wagonjwa (*Ambulance*) na uhitaji wa huduma za dharura na rufaa umeongezeka sana baada ya kukamilika kwa barabara kuu itokayo Dodoma – Babati:-

Je, ni lini Serikali itaipatia gari la wagonjwa hospitali hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE) alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Mgante Sannda, Mbunge wa Kondoa Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa kwa muda mrefu hospitali ya Mji wa Kondoa imekuwa na ukosefu wa gari la wagonjwa hali ambayo imechangiwa na uchakavu wa gari liliolokuwepo. Hata hiyo, Halmashauri ya Mji wa Kondoa imepata gari la wagonjwa (*Ambulance*) iliyotolewa tarehe 16 Machi, 2018 katika mgao wa magari yaliyotolewa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na pia nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Labda niseme tu kweli tunaishukuru Serikali kupata, nitumie lugha ya haka kagari, tumepata gari aina ya Suzuki Maruti ndogo sana ambayo kwa mazingira ya Jimbo la Kondoa lina uwezo wa kufanya *shunting* katika kata tatu za mjini tu, huku pembezoni litakuwa haliwezi kwenda kabisa kwa sababu njia haziruhusu. Je, ule umuhimu wa uhitaji wa huduma hii, Serikali haioni?.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; barabara kubwa imekamilika ya kutoka Dodoma kwenda Babati. Ongezeko la uhitaji wa huduma za dharura umekuwa mkubwa kweli, ajali ni nydingi kila uchao tunapata taarifa hizi, gari hili haliwezi kumudu. Je, ni lini sasa Serikali itatuletea gari la wagonjwa lenye kukidhi mahitaji ya hospitali ya Mji Kondoa? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, kwanza naomba nimtoe wasiwasi Mheshimiwa Sannda anaita 'kagari' lakini gari zile zimetengenezwa kwa ajili ya mazingira ya Kiafrika na ukitazama jiografia ya Kondoa ukilinganisha na maeneo mengine ambayo gari zile zimepelekwa, nimtoe wasiwasi, wanasema 'ukubwa wa pua siyo wingi wa makamasi'. Ile gari itamudu kufanya kazi iliyokusudiwa na katika maeneo ambayo gari kama zile zimepelekwa hatujapata malalamiko yoyote. Ni vizuri, wanasema 'asiyeshukuru kwa kidogo hata ukimpa kikubwa hawezi kushukuru'. Ni jitihada za Mheshimiwa Rais na tuna kila sababu ya kuziunga mkono. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swalı lake la pili, anauliza ni lini sasa itapatikana gari nyingine. Naomba nimhakikishie kwamba ni azma ya Serikali kuhakikisha kwamba inapunguza adha ya usafiri hasa kwa wagonjwa wetu, pale ambapo uwezo utaruhusu zikapatikana gari zingine tutaanza kuzipeleka maeneo ambayo hawakupata magari kabisa. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lubeleje, jiandae Mama yetu Salma Kikwete.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swalı moja la nyongeza. Kwa kuwa, Kituo cha Afya cha Mbori kinachojengwa kinakaribia kukamilika pamoja na kwamba hakijapata milioni 500, lakini kwa kuwa kituo hiki kitahudumia Kata ya Lupeta, Kimagai, Godegode, Mlembule na Matomondo. Je, Mheshimiwa Waziri uko tayari kuwapeleka gari la wagonjwa kwa sababu litahudumia watu zaidi ya laki moja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Lubeleje jinsi ambavyo amekuwa akiwapigania wananchi wake na hasa kuhusiana na suala zima la afya.

Baada ya kupongeza ni vizuri Mheshimiwa Lubeleje kwa kushirikiana na wananchi na Halmashauri yake wakahakikisha hicho kituo cha afya ambacho anakisema hakijamalizika jitihada ziongezwe ili kiweze kukamilika kwa wakati. Pia nimhakikishie kwamba ni azma ya Serikali pale ambapo uwezo unaruhusu kupeleka gari za *ambulance* maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mama Salma, jiandae Mheshimiwa Bobali.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, naomba nimuulize Mheshimiwa Naibu Waziri. Hospitali yetu ya Mkoa wa Lindi ya Sokoine haina gari la Mganga Mkuu wa Mkoa na hii hupelekea Mganga Mkuu wa Mkoa kutumia gari yake ya binafsi (*private car*). Je, ni lini hospitali yetu ya Lindi ya Mkoa itapelekewa gari kwa ajili ya Mganga Mkuu? (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Mheshimiwa Salma Kikwete kwa jinsi ambavyo amekuwa akilifuatilia jambo hili. Mimi binafsi ameshanifuata na suala hili nikalichukua na kulipeleka Ofisi ya Rais, TAMISEMI na tulikuwa tunafanya *logistics* juu ya tatizo hili na ukubwa wake. Naomba nimhakikishie, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imelipokea kwa sababu siyo hali ya kawaida kwa Mganga Mkuu wa Mkoa kutumia gari yake binafsi katika kufanya shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba atupe muda kwa kadri tutakavyoweza tukipata nafasi ya kwanza kabisa suala hili tatalitatu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bobali, wajiandae Mheshimiwa Aisharose na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, magari ambayo ameyazungumzia Mheshimiwa Sannda kwetu Mchinga tunayahitaji sana. Kituo cha Afya Kitomanga kinahitaji gari la wagonjwa lakini hakuna, nataka kujua tu, ni sifa gani ambazo haya magari yanapatikana ili tufuate hizo *procedure* kwa sababu taarifa tulizonazo humu ndani kuna Wabunge wamepewa mpaka magari mawili, wengine matatu, wakati wengine hatuna hata moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni hilo kwamba tutumie vigezo gani tupate haya magari?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwamba kuna sifa *specific* ambayo inabidi itumike ili kupata gari, hilo sina. Kinachozingatiwa ni uhitaji mkubwa wa maeneo ambayo yanahitaji magari na kwa uwiano kwamba zimepatikana gari ngapi ndipo zinagawiwa. Kwa hiyo, hakuna *specific procedure* kwamba sasa Mheshimiwa Bobali sasa hiyo sifa uwe nayo ili uweze kupata gari hiyo. Pale ambapo kuna uhitaji mkubwa na kwa kuzingatia jiografia ya maeneo husika na umbali wa wananchi kuweza kwenda kupata huduma hizo ndiyo sifa ambazo zinatakiwa.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri, amekuelewa vizuri. Mheshimiwa Mtuka, Mheshimiwa Aisharose.

**MHE. AISHAROSE N. MATEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Tatizo lilitopo Kondoa Mjini halina tofauti na tatizo lilitopo Jimbo la Singida Mjini. Kwa kuwa, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida ndiyo kimbilio la wananchi wengi katika kupata huduma za afya, lakini hospitali hiyo haina kabisa gari la kubebbea wagonjwa. Je, ni lini sasa Serikali itapeleka gari la kubebbea wagonjwa ili kuokoa vifo vya akinamama na watoto?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu, anauliza ni lini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyezekiti, jiografia na maeneo yanatofautiana. Kama hitaji kubwa kwa hospitali ya mkoa ni gari la wagonjwa na kwa sasa halipo, naomba nimtake Mkurugenzi wa Halmashauri ya Singida ahakikishe mionganoni mwa gari zilizopo anateua gari moja itumike kwa ajili ya kuhudumia wagonjwa wakati Serikali ikijipanga kuja kupeleka gari la wagonjwa. (Makof)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtuka.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyezekiti, nakushukuru, nami niulize swalii moja dogo la nyongeza. Hospitali ya Wilaya ya Manyoni pamoja na kuhudumia Wilaya ya Manyoni lakini inahudumia Wilaya ya Ikungi, Sikonge, Wilaya ya Bahi, Wilaya ya Chemba imezidiwa sana na haina kabisa gari la wagonjwa. Je, ni lini sasa Serikali itaipatia hospitali hii ya Wilaya gari la wagonjwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, wote ni lini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE):** Mheshimiwa Mwenyezekiti, tutakubaliana Wabunge wote kwamba, nia ya Serikali na jinsi ambavyo inatenda katika kupunguza adha ya wagonjwa kwa maana ya uwepo wa magari sote ni mashuhuda tumeliona. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pale ambapo nafasi ya kifedha itaruhusu tuna kila sababu ya kuhakikisha kwamba maeneo yale yote ambayo yanahitaji kupelekewa gari za wagonjwa tunapeleka na kwa kufuata vigezo kama ambavyo niliviotangulia kujibu katika swalii langu la msingi.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri. Tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Saada Salum Mkuya, Mbunge wa Welezo.

### **Ajira Katika Taasisi za Muungano**

**MHE. SAADA MKUYA SALUM** aliuliza:-

Kati ya mambo yaliyokubalika katika mkakati wa kutatua changamoto za Muungano ni pamoja na kugawana ajira zilizopo katika Taasisi za Muungano kwa asilimia 21 (Zanzibar) na asilimia 79 (Tanzania Bara):-

Je, ni kwa kiasi gani mkakati huo umetekelozwa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS,  
MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Saada Mkuya Salum, Mbunge wa Welezo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo wa ajira katika Taasisi za Muungano wa asilimia 21 kwa Zanzibar na asilimia 79 kwa Tanzania Bara unatekelezwa kwa mujibu wa waraka wa Serikali Kumb.Na.CDA279/350/01/D/95 wa tarehe 10 Mei, 2013. Tangu kutolewa kwa mwongozo huo, umetekelozwa kwa asilimia 82.7 kwa Tanzania Bara na asilimia 18 Tanzania Zanzibar.

Changamoto iliyopo katika kupata taarifa sahihi za Wazanzibari wanaopata ajira katika Taasisi za Muungano ni kutokana na anuani zao za Zanzibar badala ya wengi wanaotumia anuani za Mikoa ya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi zote za Muungano zina mwongozo wa utekelezaji wa makubaliano hayo na zinaendelea kuzingatia utaratibu huo pindi wanapopata fursa ya kuajiri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu. Kabla sijaauliza maswali yangu mawili ya nyongeza, nilikuwa nimepata *confusion* kwa sababu Mheshimiwa Waziri anasema kwamba, mwongozo umetekelizwa kwa asilimia 82.7 kwa 18 ambayo inawezekana ikawa ni jambo nzuri sana. Vile vile anasema kuna changamoto, kwa hivyo hizi *statement* zenyewe zina-*contradict*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, huu mchanganuo wa asilimia 82.7 kwa Tanzania Bara na asilimia 18.3 umetumia vigezo gani? Maana yake huu mchanganuo yaani *success*, hii *rate* umetumia vigezo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, *as far as I understand* kwamba, ni karibuni tu hivi kumetolewa kumbushio kutoka Wizara inashughulika na Utumishi wa Umma kwamba baadhi ya Taasisi hazitekelezi agizo hilo. Kutokana na miongozo hii kutolewa bila kuwa na utaratibu wa kisheria, je, ni lini Serikali itakuwa inaandaa miongozo hii ikiambatana na utaratibu wa kisheria ili tuone kwamba hizi taasisi pamoja na mambo mengine zinatekeleza hii miongozo kwa mujibu wa sheria?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, NA MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Saada Mkuya Salum ambaye amekuwa akifuatilia sana masuala ya Muungano na hasa changamoto za Muungano. Ni Mheshimiwa Mbunge ambaye kwa akinamama tunasema ni mama wa nguvu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, majibu tuliyyoyatoa hayana *confusion*, ni majibu ambayo yamenyooka kwa sababu mwongozo ule unazungumzia asilimia 21 Zanzibar na asilimia 79 Tanzania Bara. Sasa kilichokuja kutekelezwa ambapo kwa

Zanzibar ni asilimia 18.3 halafu Bara ni asilimia 82.7 ambapo pengine yeye anadhani ule ndio mkanganyiko, tumetoa sababu Mheshimiwa Saada Mkuya, kwamba tumepata ugumu sana wa kujua Wazanzibar ambao wanaajiriwa kwenye Taasisi za Muungano kwa sababu wengi wanatumia anuani za Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, miaka miwili tulikuwa na zoezi la kuhakiki watumishi hewa na vyeti hewa. Kwa hiyo, Serikali haikuweza kuajiri, ndiyo maana hizi asilimia hazikwenda juu sana. Hata hivyo, nimpe mfano mmoja; Wizara ya Mambo ya Nje, katika ajira za mwaka wa fedha 2014/2015, walajiri watumishi 28, lakini kati ya 28 watumishi saba (7) wote ni Wazanzibar na ukipiga asilimia ni asilimia 25 ambayo iko juu zaidi asilimia 21 kwenye mwongozo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la pili anasema baadhi ya Taasisi hazizingatii, hazitekelezi mwongozo huo na kwamba na ili utekelezaji uwe na nguvu kwa nini kusiwe na sheria. Wazo lake ni nzuri kwamba, pengine mwongozo unaweza usitekelezeke, lije suala la sheria. Nimhakikishie kama ziko taarifa ambazo Mheshimiwa Mbunge anaweza akatuletea ofisini kwamba Taasisi zifuatazo hazitekelezi bado Serikali tuna uwezo wa kuzitaka zitekeleze hata kama Sheria haijatungwa. Kwa hiyo mawazo yake ni mazuri. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante umemjibu vizuri na yeye ameitikia kwa hiyo atakufuata baadaye. Mheshimiwa Fakharia.

**MHE. FAKHARIA SHOMAR KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona, nina swal moja dogo tu la nyongeza. Je, ni lini Zanzibar kutakuwa na Ofisi au Kurugenzi inayoajiri kwa shughuli za Muungano badala ya kuzifuatilia Bara?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Fakharia alikuwa Kamishna mwenzangu kwenye Tume ya Utumishi wa Bunge, najua kabisa uwezo wake wa kuwakilisha Wazanzibari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli hoja aliyoitoa ya kuwa na Kurugenzi kule Zanzibar siyo jambo baya, lakini nimhakikishie kwamba mpaka sasa tunavyokwenda na ndio maana tukaja na utaratibu wa huu mwongozo amba tuliamini kama Serikali kwamba tunaweza tukatatua changamoto. Kikubwa ni kile ambacho Mheshimiwa Saada amesema kuzibana taasisi zinazohusika zihakikishe kwamba wanazingatia ule mwongozo katika kuajiri. Hata hivyo, wazo lake pia siyo baya.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu sahihi. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda, Mheshimiwa Rukia Ahmed Kassim.

Na. 336

### **Mpango wa Kuwavutia Wawekezaji wa Viwanda Nchini**

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM** aliuliza:-

Lengo la Serikali ya Awamu ya Tano ni kujenga Uchumi wa Viwanda ifikapo 2025:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwavutia Wawekezaji wa Viwanda nchini?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rukia Kassim Ahmed, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo la kufikia uchumi wa kati unaoongozwa na viwanda ifikapo 2025 limetafsiriwa vema katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2015/2016 - 2020/2021, wenye dhima ya kujenga uchumi wa viwanda ili kuchochea mageuzi ya kiuchumi na maendeleo ya watu. Utekelezaji wa mpango huu unaenda sambamba na utekelezaji wa Mkakati Uunganishi wa Maendeleo ya Viwanda (*Intergratged Industrial Development Strategy*) wa mwaka 2011 mpaka mwaka 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango na mikakati hiyo inalenga katika kuhakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji nchini ikiwa ni pamoja na kuhakikisha kunakuwa na amani na usalama wa nchi, kuondoa vikwazo kupitia sera na sheria wezeshi, uwepo wa miundombinu wezeshi na saidizi na upatikanaji wa taarifa muhimu kuhusu fursa za uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza mipango na mikakati niliyoirejea hapo juu, Serikali inahamasisha wawekezaji wa ndani na nje kujenga viwanda vidogo, vya kati na vikubwa kupitia *TIC*, *EPZA*, Balozi zetu nje ya nchi pamoja na Serikali ngazi za Wilaya na Mkoa. Uhamasishaji huo unaenda sambamba na kutoa vivutio vya kodi na visivyo vya kikodi kupitia sheria za uwekezaji pamoja na zile za uendelezaji maeneo maalum ya uwekezaji (*EPZna SEZ*). Aidha, Serikali kupitia Taasisi za *SIDO*, *NDC* na *EPZA* inatoa ushauri wa namna ya kuanzisha viwanda vidogo sana, viwanda vya kati na kuvilea ili vikue na kuwa vikubwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Rukia.

**MHE. RUKIA KASSIM AHMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini bado nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa viwanda vingi vimeshindwa kuijendesha kutohana na gharama za uendeshaji kuwa kubwa, kama vile kodi kuwa nyingi pamoja na bei ya umeme kuwa ghali hata ukilinganisha na nchi jirani zetu hapa Afrika ya Mashariki. Je, Serikali iko tayari kupunguza hizi kodi pamoja na gharama

za umeme ili iwe kivutio kwa wawekezaji wengine kuweza kuja kuwekeza na hivi tulivyonyavo vijiendeshe kwa faida ili vijana wetu waweze kupata ajira?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali pili, kwa kuwa viwanda vingi ambavyo Serikali ina lengo la kuvifufua miundombinu yake ni ya kizamani. Je, Serikali ina mpango gani wa kuvifufua viwanda hivi ili viende na hali tuliyonayo na vijiendeshe kwa faida na vijana wetu waweze kupata ajira.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la kwanza la kuhusu gharama za uendeshaji na mazingira wezeshi ya kufanya biashara nchini, nimwondoe tu hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba hata wakati wa usomaji wa bajeti wa Wizara, Mheshimiwa Waziri alieleza mipango na mikakati ya Kiserikali ya kuhakikisha tunaweka mazingira wezeshi ya kuweza kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje kufanya biashara nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kati ya jambo kubwa ambalo linaendelea hivi sasa ni matayarisho ya mpango ambao unaitwa *Blue Print to Emprove Business Environment in Tanzania* ambao lengo lake kubwa ni kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi ya kuwafanya Wawekezaji wote wavutike na kuja kuweka katika nchi yetu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika swali lake la pili alitaka kufahamu kuhusu ufufuaji wa viwanda kutokana na miundombinu chakavu. Wizara inaendelea na mchakato huo na kama ambavyo imekuwa ikitolewa taarifa mara kwa mara, tumepitia katika maeneo mengi ya viwanda ambavyo vilishabinafsishwa na maelekezo yalitoka ili vifufuliwe, viweze kuajiri vijana wengi zaidi, kwa sababu lengo hapa kubwa ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2025 kundi kubwa zaidi ya asilimia 40 lipate ajira kupitia viwanda.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kwa ajili ya muda, Mheshimiwa Dkt. Kafumu.

**MHE. DKT. DALALY P. KAFUMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kumuuliza swali moja Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa, moja ya mbini za kuhamasisha wawekezaji ni kushauriana nao na hasa sekta binafsi; na kwa kuwa nafahamu Serikali ilianza mashauriano ya kila mwezi na wawekezaji, naomba kufahamu kitu gani hasa kimejadiliwa na mwelekeo wa Serikali ni nini kwenye jambo hilo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi. Huyu ni Waziri wa Kazi lakini anacheza viwanja vyote. (*Makofî*)

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y. WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Serikali sasa imekuja na mpango wa kuhakikisha kwamba tunakaa na sekta binafsi kujadiliana changamoto zilizopo, mpaka sasa tunavyozungumza vimeshafanyika vikao vitatu ambapo viwili vilifanyika Dar es Salaam na kimoja Dodoma. Kikao hicho sasa ndiyo kimetengeza hasa hii *Blue Print* kutokana na changamoto ambazo walizisema sekta binafsi ambazo zinawakwaza kwenye ufanyakaji wa biashara, Serikali ikaichukua na ndiyo maana tumetengeneza hiyo *document* kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira wezeshi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama Serikali tunafahamu kwamba ni muhimu sana kuitunza na kuilea sekta binafsi kwa ajili ya ustawi wa Taifa letu.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anna Kilango, halafu tunaendelea.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba kuuliza swali dogo la nyongeza; je,

Serikali ina mpango gani wa kuwavutia zaidi wawekezaji ambao wakija watawekeza kwenye viwanda vyatia kuongeza thamani mazao yetu kuliko viwanda vingine vyovoyote. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Same kuna tangawizi kibao, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (K.n.y WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimpongeze kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatetea wananchi wake hasa kwenye suala la viwanda ambalo linahusisha masuala la vitunguu na tangawizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili niseme kwa ufupi ya kwamba, kama Serikali tumeona ni vema kuendelea kutumia Balozi zetu, vilevile tumeona ni vema kufanya makongamano mbalimbali ili kuwavutia wawekezaji wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ninavyozungumza mwaka jana Desemba, tulifanya mazungumzo na kongamano kubwa na Wafanyabishara kutoka China. Mwezi Desemba pia tulifanya kongamano kubwa na wafanyabiashara kutoka Jordani, tarehe 18 mwezi wa Nne tulifanya Kongamano kubwa sana na wawekezaji kutoka Ufaransa kwa lengo hilo hilo. Vile vile tarehe 23 - 24 Aprili tulikutana na watu kutoka Israel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu kuwavutia wawekezaji wengi zaidi na kuwaomba kuja kuwekeza hasa katika maeneo haya ya kuongeza thamani. Nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hiyo Serikali inaendelea kuifanya. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, aulize swali lake.

Na. 337

## **Ujenzi wa Barabara ya TAMCO – Mapinga**

**MHE. SILVESTRY F. KOKA** aliuliza:-

Barabara ya *TAMCO* – Mapinga kupitia Kata ya Pangani ilichukuliwa na *TANROADS* takribani miaka nane (8) iliyopita:-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya kujenga barabara hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Silvestry Francis Koka, Mbunge wa Kibaha Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wakala wa Barabara (*TANROADS*) imekamilisha maandalizi ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya *TAMCO* – Mapinga yenye urefu wa kilometra 23 kwa kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, pamoja na uthamini wa mali ambao ulikamilika Februari, 2014. Baada ya usanifu wa kina kukamilika, Serikali imeanza kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 kilomita moja ilijengwa kwa kiwango cha lami na katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali imetenga kiasi cha shillingi bilioni 4.234 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa barabara hii kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali kupitia *TANROADS* imekamilisha taratibu za ununuzi wa kumpata Mkandarasi na inaendelea na maandalizi ya kusaini mkataba.

Vilevile katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi biliioni 1.5 zimetengwa kwa ajili ya kuendelea na mradi huu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Koka.

**MHE. SILVESTRY F. KOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nichukue fursa hii kuipongeza Serikali yetu chini ya Mheshimiwa Dkt John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ya ujenzi wa barabara inayofanya. Pamoja na pongozi hizo nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa kero kubwa kwa wananchi wetu ni fidia. Barabara hii ya kilomita 23 ina jumla ya fidia ya bilioni 8.9; je, kwa nini Serikali sasa isilipe wananchi hawa fidia wakaweza kufanya shughuli zao za kiuchumi na ikaendelea na ujenzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kuna barabara ya Kwa Mathias mpaka Msangani ambako ndiyo Makao Makuu ya Jeshi la Wananchi la Ardhini (*Land Force*). Barabara hii ina ahadi ya lami muda mrefu. Je, Serikali imefikia wapi kukamilisha au kujenga lami hii katika barabara hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu, Waheshimiwa muda wetu wa maswali mwisho saa nne, bado tuna maswali nane.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua umuhimu wa kulipa hizi fidia kwa wananchi. Nimpongeze tu Mheshimiwa Mbunge kwa sababu mara nyingi nimemsikia hapa ndani ya Bunge na hata tukizungumza kule nje amezungumza juu ya fidia hii ya wananchi wa maeneo haya. Kwa hiyo, nimhakikishie tu kwamba suala hili linaendelea kushughulikiwa na kwa mujibu wa taratibu na sheria wananchi watalipwa mapema sana fidia yao hii ambayo Mheshimiwa Mbunge anaitaja. Kwa hiyo, nimwondoe hofu pamoja na wananchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swalii lake la pili, kuhusu barabara ya Kwa Mathias – Msangani ni ahadi ya Serikali. Katika mwaka huu wa fedha 2018/2019, Mheshimiwa Mbunge anatambua tumetenga fedha kwa ajili ya kuendelea kuboresha barabara hii ili hatimaye iweze kutengenezwa katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwatoe hofu wananchi wote wa maeneo ya Kwa Mathias na maeneo ya Msangani na maeneo yote ya Kibaha kwa ujumla tu kwamba, Serikali imeitazama barabara hii na kuangalia umuhimu wa maeneo yenye we tutaendelea kuiboresha ili barabara hii iweze kuitika vizuri zaidi na kutoa huduma kwa vikosi vyetu ya Jeshi vlivyopo katika maeneo haya.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dkt. Ishengoma. Waheshimiwa tunaomba radhi muda wetu umekwenda sana.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niweze kuuliza swalii dogo. Barabara ya Msangani –Kwa Mathias ni sawasawa na barabara ya Ifakara – Mlimba kwa umuhimu wake kwa uzalishaji wa mpunga. Je, ni lini barabara hii ya Ifakara – Mlimba itajengwa kwa kiwango cha lami?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Serikali inatambua umuhimu wa kuboresha maeneo haya, kwa sababu maeneo haya ambayo Mheshimiwa Mbunge anayazungumza ni korido ambalo lina uzalishaji mkubwa wa mazao ya mahindi na mazao ya mpunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kuanzia Kidatu sasa ujenzi wa kilomita 66 unaendelea kwenda Ifakara na ili

tuweze kuwa na muunganiko mzuri, hii barabara ya kutoka Ifakara kwenda Mlimba na kutoka Mlimba kwenda Madeke itaenda kuungana na wenzetu kule upande wa Njombe. Barabara hii tayari iko kwenye utaratibu, mchakato wa kuitengeneza barabara hii na kuiboresha kwa kiwango cha lami unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huduma zitakuwa nzuri pia kwa wananchi ambao wako maeneo haya ya Mlimba tutaweza kuwaunganisha na wenzao wa upande wa Malinyi, kwa maana tutakuwa na kivuko ambacho tutakiweka ili kuboresha huduma ya mawasiliano ya huko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ahsante. Tunaendelea na Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Mheshimiwa Abdul- Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini.

Na. 338

**Mgogoro wa Ardhi kati ya Jeshi na Wananchi wa  
Kauzeni na Luhongo**

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD** aliuliza:-

Kuna mgogoro wa ardhi kati ya Jeshi la Wananchi kwenye mipaka katika Kata ya Kauzeni na Luhongo ambapo wananchi wanashindwa kufanya shughuli zao za maendeleo hasa kilimo, Jeshi linaweka mipaka na kuingiza ndani ya mashamba ya wananchi wakati miaka yote maeneo hayo yalikuwa nje ya mipaka ya Jeshi:-

(a) Je, ni lini Serikali itawarudishia wananchi maeneo yao ya kilimo?

(b) Je, kwa nini Serikali isichukue hatua kwa kuruhusu wananchi wamiliki maeneo hayo ambayo ni ya asili na Jeshi limewakuta wananchi katika eneo hilo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abdul-Aziz Mohamed Abood, Mbunge wa Morogoro Mjini, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufumbuzi wa mgogoro wa mipaka ulishafanyika kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. Hivyo, kimsingi Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania halina mgogoro na wananchi kwenye mipaka ya Kata za Kauzeni na Luhongo hasa baada ya upimaji mpya wa mwaka 2002 ambapo uliacha nje maeneo ya vijiji. Manung'uniko yaliyopo yanatokana na uamuzi wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kusitisha utaratibu wa kuwaruhusu kwa muda baadhi ya wananchi kulima mashamba ndani ya mipaka yake kwa sababu za kiulinzi na kiusalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yanayomilikiwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania yapo kwa ajili ya ulinzi wa nchi na sehemu hizo zipo kimkakati kwa ajili ya usalama wa nchi. Serikali imetumia rasilimali nydingi za wananchi wa Tanzania kujenga miundombinu iliyopo kwenye eneo hilo. Hivyo, haitokuwa vema kwa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania kuondoka katika maeneo yaliyochaguliwa kistratejia kwa ajili ya ulinzi. Ni vema wananchi waelimishwe juu ya jambo hili na nimwombe Mheshimiwa Mbunge ashirikiane na wadau mbalimbali katika Halmashauri ya Mkoa kutoa elimu kwa wananchi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Abood.

**MHE. ABDUL-AZIZ M. ABOOD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swalii la kwanza, kwa kuwa, wananchi wa Kauzeni na Luhongo walihamia pale mwaka 1969 wakati wa Vijiiji vya Ujamaa na wakapewa maeneo ambayo yalipimwa mwaka 1970 ikawekwa mipaka kati ya shirika na wananchi;

je, kwa nini Serikali isitumie mipaka hiyo ya mwaka 1970 ili wananchi wakapata haki yao na mashamba yao yakawa katika eneo lao?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, si swali lakini ningewomba Mheshimiwa Waziri angekuja katika maeneo haya akaangalia yeye mwenyewe na kuweza kukutana na wananchi akapata ukweli ulivyo katika meneo haya. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba upimaji wa awali umefanyika mwaka 1970 na baada ya pale kutokana na migogoro hii ya kuingiliana kati ya maeneo ya Jeshi na Wananchi, mwaka 2002 ulifanyika upimaji mpya ambao ulikuwa na lengo la kuondoa wananchi waliokuwa ndani ya mipaka ya Jeshi kwa hivyo wakaachwa nje, sasa inaonekana baada ya pale mgogoro umeendelea. Nataka nimkubalie na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba niko tayari kwenda katika eneo hilo pamoja na wataalam wangu ili tukazungumze na wananchi na kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee tu kusema kwa ufupi kwamba, matatizo ya mipaka kati ya maeneo ya Jeshi na wananchi yako sehemu nyingi sana. Naomba niwaarifu tu Waheshimiwa Wabunge kwamba nimetengeneza utaratibu maalum wa kupita katika maeneo hayo ili mimi na wataalam wangu tutuhititishe mipaka hiyo na kuhakikisha kwamba tunaondoa hii mogogoro ambayo imeendelea kwa siku nyingi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu hapa kwamba kuna mgogoro ambao nimeupata kutoka kwa Mheshimiwa Mwakyembe kwenye Kata za Bondeni, Ipiyana na Kajunjumele katika Wilaya ya Kyela, nimhakikishie pia kwamba katika utaratibu nitakaopanga wa kuzunguka katika maeneo haya nitafika na pale nizungumze na

wananchi ili hatimaye tuondoe matatizo yanayowakabili wananchi katika maeneo hayo. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa wote ambao mna matatizo haya ombeni kibali cha Spika yatakuja kwenye Kamati ya Ulinzi na tutayazungumza kwa faragha. Tunaendelea na Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani kwa niaba yake Mheshimiwa Machano, Wizara hiyo hiyo.

Na. 339

**Kambi za Jeshi za Ubago na Dunga Kuvamia  
Maeneo ya Wananchi**

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID (K.n.y. MHE. SALUM MWINYI REHANI)** aliuliza:-

Kambi za Jeshi za Ubago na Dunga zinawanyanyasa wananchi wa Shehia ya Kidimi kwa kuwataka waondoke katika maeneo hayo ambayo ni ya iliyokuwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Ushirika kwa zaidi ya miaka 40 wameanza kupima na kuweka bikoni:-

Je, Serikali inatoa tamko gani juu ya hali hiyo na hatma ya wananchi wanaoishi kwenye maeneo hayo?

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Salum Mwinyi Rehani, Mbunge wa Uzini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya Ubago na Dunga yalipimwa mwaka 1985, kwa unyeti wake Uongozi wa Mkoa na Wilaya husika zilishirikishwa. Aidha, taratibu zote za utwaaji ardhi kwa matumizi ya umma zilitumika na kuruhusu maeneo haya kupimwa yaani Ubago na Dunga. Maeneo yote mawili tayari yamejengwa miundombinu ya Kijeshi ambayo siyo rafiki kwa matumizi mengine ya kiraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria ya Ardhi Na. 12 ya mwaka 1992 ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ilipoanza kutumika, ramani za upimaji wote uliofanyika kabla ya 1992 zilitakiwa kupitiwa upya. Hivyo, ramani za upimaji wa maeneo ya Ubago na Dunga zilikwama kupata Hatimiliki kutokana na sheria hiyo. Hali hii ilitoa mwanya kwa wananchi kuingilia sehemu ya maeneo ya Kambi kwa shughuli za kiraia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 19 Mei, 2018 kulifanyika kikao na ukaguzi wa pamoja kati ya Wizara yangu na Waheshimiwa Mawaziri wa SMZ pamoja na Mkurugenzi wa Mipango Miji na Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani wa Zanzibar kwa lengo la kupata ufumbuzi wa kudumu wa wananchi walioko katika maeneo haya. Ukweli ni kwamba eneo hili linatumwiwa na JWTZ kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, timu ya watalaam kutoka Idara ya Ardhi ya SMZ ikishirikiana na Uongozi wa Mkoa na Wilaya husika wanaendelea na zoezi la kufanya tathmini ya uvamizi wa maeneo haya ili hatimaye kusaidia kufikia uamuza kuhusu hatma ya wananchi ndani ya maeneo haya nyeti ya JWTZ.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Machano.

**MHE. MACHANO OTHMAN SAID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri majibu yake mazuri na ya ukweli, pamoja na majibu hayo naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, katika bajeti ya mwaka jana Mheshimiwa Waziri aliahidi kulimaliza tatizo la Kambi ya Kisakasaka ambayo iko katika Wilaya ya Magharibi B. Je, ni hatua gani zimefikiwa hadi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Kambi ya Mtoni ambayo iko katika Wilaya ya Magharibi A ni ya muda mrefu na watu waliikuta kambi kabla ya kuhamia wao na kuna viashiria vya kuvamiwa na wananchi; Je, Mheshimiwa Waziri anatuambia nini kuhusu suala hili na kama kuna upimaji au

tayari imeshapimwa kambi ile ya Mtoni ili kuepuka uvamizi wa wananchi katika eneo lile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo la Kisakasaka ambalo tuliahidi kwamba tutamaliza tukiweza kupata bajeti, nieleze tu kwamba mpaka sasa fedha za ulipaji wa fidia na upimaji bado hazijapatikana, ni mategemeo yetu kwamba tunaweza tukapata kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha ili tuweze kulimaliza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kambi ya Mtoni ni dhahiri kwamba kambi karibu zote zimepimwa lakini kuna kuhuisha mipaka, kwa hivyo tutakachofanya kama nillivyoeleza awali ni kwamba tunatengeneza utaratibu maalum sasa wa kuititia maeneo yote ili tuweze kuhakikisha kwamba mipaka yetu inahuishwa na kuwataka wananchi wale ambaeo hawana stahili, basi waweze kutoka katika maeneo hayo, lakini wale ambaeo wataonekana na stahili aidha turekebishe mipaka au wapatiwe fidia zao ili tuondokane na migogoro ambayo imeonekana kwamba haiishi kati ya Wananchi na Wanajeshi. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maji, Umwagiliaji. Swalii la na Mheshimiwa Mulugo.

Na. 340

**Mipango ya Serikali Kuhusu Ziwa Rukwa**

**MHE. PHILIP A. MULUGO** aliuliza:-

(a) Je, ni nini mpango wa Serikali kuhusu Ziwa Rukwa hasa kwa kuzingatia kudumaa na kukosekana zao la samaki katika Ziwa hilo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuliendeleza bonde la Ziwa Rukwa hasa katika kilimo cha umwagiliaji?

## **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-**

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Philipo Augustino Mulugo, Mbunge wa Songwe, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuwa shughuli za uvuvi katika Ziwa Rukwa hudumaa na kukosekana kwa zao la samaki. Hali hii ilikuwa ikitababishwa na changamoto mbalimbali kubwa ikiwa ni uvuvi haramu ambapo wavuvi hutumia dhana haramu za uvuvi ambazo ni makokoro na nyavu zisozoruhusiwa kuvua. Pia uchafuzi wa mazingira unaotokana na kuongezeka kwa shughuli za binadamu kama vile uchimbaji wa madini na shughuli za kilimo karibu na Ziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Halmashauri zinazozunguka Bonde la Ziwa Rukwa imeweka utaratibu unaozingatia sheria ambapo shughuli za uvuvi kwa baadhi ya maeneo hufungwa ili kuwapa nafasi samaki kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Bonde la Ziwa Rukwa linafaa kwa shughuli za kilimo cha umwagiliaji kutokana na kuwa na mito mingi yenye kutiririsha maji mwaka mzima na maeneo yanayofaa kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uwepo wa fursa hizo katika bonde hilo Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kuboresha kilimo cha umwagiliaji kupitia Skimu za Ifumbo, Mshewe na Utengule, Bara, Ipunga, Iyura na Mbolumlowo, Naming'ongo, Sakalilo na Ng'ongo, Kilida, Mwamkulu, Kakese, Uruila na Usense.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kuboresha skimu zote za umwagiliaji zilizopo kwenye Bonde la Ziwa Rukwa na hivi sasa Serikali imeliweka Bonde la Ziwa Rukwa kwenye mpango ulioboreshwaa na kuendeleza kilimo cha umwagiliaji Kitaifa.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Philip Mulugo, swali la nyongeza.

**MHE. PHILIP A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kwa kupata muda wa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Ziwa Rukwa kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri huwa linafungwa kila wakati lakini pale Serikali inaporuhusu kufunguliwa bado samaki wale ni wadogo na wamedumaa kabisa na utafiti unafanya lakini haufanywi ule utafiti wa wa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni zaidi ya miaka 20 sasa toka mwaka 1978 toka Serikali imepandikiza samaki Ziwa Rukwa. Nataka Mheshimiwa Waziri anijibu ni lini Serikali itafanya uthabiti wa kina kabisa wa uhakiki wa kuja kufanya utafiti katika Ziwa Rukwa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika skimu za umwagliaji nimeona hapa ameorodhesha maeneo ya Rukwa kule Sumbawanga, Mbozi pamoja na kule Mombia lakini mimi nimeuliza Bonde la Songwe maana yake ni Jimboni Songwe, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa Nanjembo ambao tayari usanifu ulishafanyika kwa ajili ya umwagiliaji, watupe fedha tuweze kufanya miradi ya umwagiliaji? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Waziri wa Uvuvi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, Mwalimu Mulugo na nashukuru pia kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge anataka kujua ni lini tutafanya utafiti wa kina, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika bajeti yetu ya mwaka huu, taasisi yetu ya utafiti ya *TAFIRI* tumeitengea pesa na tayari tumeshailekeza kwamba katika moja ya kazi muhimu za kufanya ni kwenda

kuangalia hatma ya Ziwa Rukwa na samaki wa Ziwa Rukwa ili waweze kuwanufaisha Watanzania wa kule Songwe. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Shekilindi, jiandae Malocha jiandae Dkt. Kikwembe.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona ili niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa, Wilaya ya Lushoto ina milima inayotiririsha maji hasa kipindi cha mvua. Je, Serikali haioni sasa ipo haja ya kujenga mabwawa hasa katika maeneo ya Kwekanga, Mbwei, Kwai, Makanya, Bweloi, pamoja na Bonde la Ubiri kwa ajili ya wakulima wa Wilaya ya Lushoto kulima kilimo cha umwagiliaji? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mbunge Shekilindi kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini nikubaliane na yeye ipo haja ya Serikali kuwekeza katika kilimo cha umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha tunafikia azma ya viwanda lazima tuwekeze katika kilimo cha umwagiliaji. Wizara yetu Mheshimiwa Waziri ameona haja sasa ya kupitia mpango kabambe wa mwaka 2002 wa Tume ya Umwagiliaji katika kuhakikisha tunauboresha umwagiliaji ili uweze kuwa na tija na manufaa kwa nchi yetu. Nimhakikishie katika uboreshaji huo watu wa Lushoto hatutawaacha katika kuhakikisha wanawakeza katika kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Malocha, ajiandae Dkt. Kikwembe.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa umaarufu huo wa mabonde katika Ziwa Rukwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ilishaomba

miradi ya umwagiliaji yapata sasa miaka mitano hajapata fedha ambayo ni Maleza, Ilemba, Msiya, Uzia, Kwilo na Milepa. Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili miradi hiyo iweze kujengwa kwa manufaa ya wananchi? (*Makofii*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana. Kikubwa ni wahakikishie Waheshimiwa Wabunge sisi kama Wizara ya Maji kama nilivyoeleza tunaendelea kutokana na changamoto zilizopo katika kilimo cha umwagiliaji ama uwekezaji wa umwagiliaji, tunazo skimu nyingi lakini hazijakamilika, Waziri wangu akaona haja sasa ya kupitia mpango huu kabambe ili tuwe na skimu chache ambazo zitakuwa na tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge baada ya mapitio haya katika maeneo ambayo ameyaelekeza tutawekeza fedha katika maeneo yake ili wananchi wanaweza kulima kilimo cha umwagiliaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Pudenciana Kikwembe.

**MHE. DKT. PUDENCIANA W. KIKWEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kunipatia nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Katika majibu yake ya msingi Mheshimiwa Waziri ametamka mradi ambao uko katika Bonde la Ziwa Rukwa lakini uko katika Jimbo langu mradi wa umwagiliaji wa Kirida ambao nilikwishaleta maombi pamoja na mradi wa Mwamapuli. Je, Serikali inakuja na kauli gani sasa kuhusiana na hii miradi ambayo tayari tulikwishawekeza pesa isipokuwa iliharibika kwa ajili ya mvua ili iweze kuendelezwa na kuleta tija kwa wananchi ambao tayari miundombinu ipo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Serikali ama kauli ya Serikali ni kuhakikisha miradi ya maji ambayo hajakamilika

ni kuikamilisha na ile ambayo inahitaji ukarabati tufanyie ukarabati katika kuhakikisha inaleta tija katika uzalishaji. (*Makof*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha sasa ni kipindi cha wageni.

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wa 40 wa Mheshimiwa Angeline Mabula Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ambao ni Viongozi wa Chama cha Mapinduzi na Jumuiya ya vijana CCM (UVCCM) kutoka Wilaya ya Ilemela Mkoani Mwanza, wakiongozwa na Katibu wa CCM Wilaya ya Ilemela ndugu Maulid Acheni. Karibuni. (*Makof*)

Pia kuna mgeni wa Mheshimiwa Ikupa Alex, Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Watu Wenye Ulemavu ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha St. Francis Kilichopo Mkoani Mwanza wakiongozwa na Ndugu Festo Ngadaya, karibuni. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, pia kuna wageni wanne wa Mheshimiwa Hassan Masala ambao ni Waheshimiwa Madiwani na ndugu zake kutoka Mkoani Lindi wakiongozwa na Mheshimiwa Rabia Penengu Diwani Kata ya Mchonda, karibuni. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, vile vile tunao Wageni 45 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao ni wanafunzi wa Madrasat Ashrafiya kutoka Chang'ombe Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Madrasat Ustaadh Hamis Itara. Karibuni Madrasat simameni hampo? (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni 40 wa Mheshimiwa Rose Kamili Sukum ambao ni vijana 30 na Viongozi Waandamizi 10 kutoka Shirika la *Compassion International* liliopo Hanang' Mkoani Manyara, karibuni Dodoma. (*Makof*)

Wageni watano wa Mheshimiwa Bupe Mwakang'ata ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mkoani Rukwa, karibuni. (*Makof*)

Tunao wageni 80 wa Mheshimiwa Bonnah Kaluwa ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari ya TUSIIME iliyopo Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Walimu wao, karibuni hongereni sana baada ya hapo mwambieni Mbunge awapeni chai, inapatikana saa nne na nusu pale, watu 80 siyo mchezo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, wapo wageni waliotembela Bunge kwa ajili ya mafunzo wanafunzi 63 wa Chuo cha Biblia cha Tanzania *Assemblies of God* kutoka Jijini Dodoma, karibuni Dodoma. (*Makof*)

Pia kuna wanafunzi 80 na Walimu 10 kutoka Shule ya Msingi Makole Jijini Dodoma. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Waziri wa Madini Mheshimiwa Angellah J. Kairuki anaomba kuwaalika Waheshimiwa Wabunge wote pamoja na Watumishi wa Bunge kutembelea viwanja vya Bunge ili kupata nafasi ya kuona na kujifunza kuititia maonesho ya sekta ya madini yatakayohusisha kazi za Wizara ya Madini, wachimbaji wa madini, wachenjuaji wa madini, wakataji wa madini, masonara na wauzaji wa madini.

Waheshimiwa Wabunge, kwa kuwa, maonesho hayo ni ya aina yake, wote mnakaribishwa na ni muhimu kutembelea ili kuweza kujifunza vizuri kuhusu madini. (*Makof*)

Mheshimiwa Shally Joseph Raymond Mwenyekiti wa Jumuiya Mtakatifu Thomas Moore Bungeni, anawatangazia kwamba leo Jumatano tarehe 30 kutakuwa na Ibada ya Misa kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha Bunge saa saba mchana katika Ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Waheshimiwa Wabunge wote mnakaribishwa kushiriki Ibada hiyo ya Misa.

Waheshimiwa Wabunge, kutohana na changamoto ambazo tunazo leo hakuna Mwongozo. Tunaendelea Katibu.

**NDG. ATHUMAN HUSSEIN - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa  
Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Ardhi,  
Nyumba na Maendeleo ya Makazi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na michango yetu, tutaanza na Mheshimiwa Hamidu Bobali, ajiandae Zuberi Kuchauka.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwanza niendelee kumwombea Mbunge Mwenzangu Ndugu yangu Mheshimiwa Kasuku Samsoni Bilago safari yake anayokwenda Mwenyezi Mungu ampooke na amuweke mahali pema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisikilize. Mwaka jana nilimpongeza humu ndani ya Bunge kwa kazi aliyoifanya pale Mchinga ya kuamua kumnyang'anya yule mtu ambaye alituibia ardhi yetu zaidi ya hektaa 4,000 na kuzirudisha Serikalini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nataka nimwambie kwamba lile jambo kuna Watendaji wa Serikali waliopo ndani ya Mkoa wetu wa Lindi halikuwafurahisha. Huwezi kuamini kwamba mwaka jana mwezi Machi, Mheshimiwa Rais alifika Mchinga akaoneshwa vile Vituo vya Afya viwili ambavyo alijenga yule jamaa pale Mchinga na Ruvu, akatoa agizo kwamba ndani ya mwezi mmoja viwe vimefunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka nimwambie Mheshimiwa Waziri mpaka sasa hivi tumepata mfadhili amekubali atatuletea vifaa tiba vyote. Hivi sasa nihavyosema viko baharini vinaleea vitafika mwezi wa Tisa, lakini lile eneo tumezuiwa tusilitumie, tumezuiwa zile Zahanati tusizitumie, tumezuiwa kila kitu pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna vitu vinaletwa na mfadhili lakini Serikali ya Mkoa na Serikali ya Wilaya tena iliagizwa na Mheshimiwa Rais kwamba walishughulikie jambo lile ili tupate funguo, mpaka sasa hivi yule jamaa funguo amezi-*withhold*, hataki kuzitoa, Mkoa ule una Mkuu wa Mkoa, una Mkuu wa Wilaya na una watendaji wote wa Serikali lakini wanashindwa namna ya kufungua zile Zahanati

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri nataka nimwambie jambo lile halikuwafurahisha. Tulikwenda kwenye kikao cha RCC, Kiongozi ninayemheshimu sana wa mkoa anasema kwamba kuna utaratibu ambao haukuuatwa vizuri, kwa hiyo jamaa amegoma kutoa funguo. Yeye kama Mkuu wa Mkoa, kama kiongozi wa mkoa anachukua hatua gani kulazimisha ama kuhakikisha kwamba zile funguo tunazipata na yule jamaa lile eno letu anatuachia. Maana inakuwa ni kana kwamba lile eneo bado analo yeye. Kama tunashindwa kuvitumia vitu ambavyo yeye alivijenga na tukamnyang'anya, sasa inaonekana kwamba sisi wenyewe kwenye Mkoa ndio tuna matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, kama alitoa amri ambayo haikuwa na *document*, hakufanya *documentation*, naomba aiandikie Serikali ya Mkoa yale maagizo yake, kwa sababu inaonekana kwamba wao wanaona *just business as usual*. Sasa namwomba sana Mheshimiwa Waziri alichukulie jambo hilo kwa umuhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu tatizo la mipaka kati ya vijihi, kati ya halmashauri na halmashauri, kati ya kata na kata. Mheshimiwa Waziri huwezi kuamini

kwamba Wilaya ya Lindi ambayo mimi ndiko ninakotokea; sisi tuna migogoro mizito kwanza ndani ya Wilaya kati ya Halmashauri ya Manispaa ya Lindi na Manispaa ya Lindi *DC*. Pia tuna mgogoro wa kati ya Lindi *DC* na Wilaya ya Ruangwa. Sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili la migogoro ya mipaka walichukue, walifanyie kazi, waje mpime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza mimi Ruangwa ilikuwa sehemu ya Wilaya ya Lindi, wao wametoka mbavuni kwetu wakachukua eneo lao wakaondoka. Sasa leo na wao wanakuja wanasogea wanachukua baadhi ya maeneo yetu tena ya Lindi *DC* wanasema ya kwao. Kuna mgogoro mzito, hata pale ambapo mimi napasema kila siku kuna mjesi alichukuliwa leo watu wa Ruangwa wamesogea kabisa na tusipokuwa makini mwakani tutakuja kuambiwa yule mjesi amechukuliwa Ruangwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana hii migogoro aje atutatulie, aje aseme kwamba mpaka wa Wilaya umepita humu na *GN* inasoma hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro ya kwenye kata huko, hiyo ndiyo mingi, lakini kwanza angalau tuanze na hii ya Wilaya. Huwezi kuamini kwamba watu wa Manispaa maeneo ambayo tuliyowapa juzi tu ili wakidhi vigezo kuwa Manispaa leo wanakwenda wanatunyang'anya. Wao wameanzisha mkakati wao wa kuhakikisha watu wanalima korosho wanauzu maeneo yao, wanawapa wenye fedha walime mashamba makubwa ya mikorosho. Sasa wamegawa maeneo yamekwisha wanakuja kuchukua na maeneo yetu ya Lindi Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri atume watu wake, waje Lindi, waje watutatulie migogoro iliyopo kati ya Lindi Manispaa, Lindi *DC*, na watu wa Wilaya ya Ruangwa kwa sehemu ndogo. Naamini hata huu mgogoro wa Ruangwa hata Waziri Mkuu siju kama anaufahamu labda kwa sababu yupo bize na mambo mengine ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aje atatulie hili, kwa sababu tatizo la migogoro ya ardhi Lindi sasa hivi, viongozi tunaowaamini kwamba wanaweza kuwa ma-referee wao ndio *part and parcel* ya hii migogoro; kwa sababu nao wamejichukilia hayo maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hao watu wa Manispaa watu ambao wamegawa maeneo, hao ambao tunawategemea kwamba wangesimama katikati ndio waliochukua hayo maeneo. Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri hili ni tatizo. Sasa ukienda ukawaambia hili eneo la Lindi *DC* na hili la Manispaa hawakuelewi kwa sababu wao ni wanufaika wa hayo mambo. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aliangalie kwa umakini sana suala la migogoro ya ardhi kwa sababu linaleta shida.

Mheshimiwa Mweyekiti, jambo la tatu, ni suala la upatikanaji wa hati ya umiliki wa ardhi. Jana nilimsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Waziri, akasema kwamba wameongeza upatikanaji wa hati ndani ya miezi sita, sjui miezi mingapi, lakini mchakato huu bado ni mkubwa sana, bado mchakato ni mrefu. Mimi naishi Dar es Salaam, tupo pale kwenye mtaa wetu kule Chamazi, tumefanya *application* tangu mwaka jana mpaka leo hatujapata hati, tunahangaika na suala la hati na tuko watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Waziri akija akisema kwamba tumeongeza na mimi naamini si suala la kwangu; na nilimwona wakati anazunguka Mikoa ya Kanda ya Ziwa, aliona namna ya watu wanavyomjalia, alikuwa anafanya kazi mpaka saa sita usiku, ni ushahidi kwamba kuna tatizo kubwa kwenye mfumo wa Wizara yake, kuna tatizo kubwa kwa walio chini ya Wizara yake, kwamba wao ndio wanategemewa waipunguze hii migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ukiona kwamba Mheshimiwa Waziri anakwenda anapokelewa na zaidi ya watu 1000 au 2000 *which means* walio chini yake hawawajibiki vizuri. Kwa hiyo hili liwe changamoto kwa Mheshimiwa Waziri, lisiwe suala la Kanda ya Ziwa na maeneo

mengine tuu, hata akija Lindi na Mtwara tatizo litakuwa ni hilo hilo, kwamba kunakuwa na ucheleweshaji mkubwa, mtu anaomba hati, basi namna ya kuja kuipata zaidi ya miaka miwili au miaka mitatu hili nalo ni tatizo sana. Kwa hiyo namwomba Mheshimiwa Waziri suala la upatikanaji wa hati za ardhi liwe ni suala ambalo ni haki ya Mtanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ziko hati zinaitwa Hati za Kimila. Sisi Halmashauri yetu ya Wilaya ya Lindi, kwa kutumia MKURABITA na sisi wenyewe tumeomba baadhi ya maeneo tupatiwe Hati za Kimila. Hata hivyo, hapa tunapomweleza Mheshimiwa Waziri hakuna hata kijiji kimoja ambacho kimeanza kutoa Hati za Kimila.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mahitaji makubwa sana kwa Mkoa wa Lindi na Mtwara sasa hivi ardhi ikawa inamillikishwa na kwa sababu mbilli; kwanza kwa *potentiality* ya maeneo yale, kugundulika kwa gesi kumeongeza au kume-*attract* watu wengi kuja kumiliki ardhi kule. Sasa hawa watu leo wasipokuwa na Hati zao, ni rahisi kuja kunyang'anywa, ni rahisi kuja kurubuniwa na watu wenye vijisenti wakachukua maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi mkubwa, katika eneo ambalo linakwenda kujengwa mradi wa LNG, pale Likong'o mpaka ukija pale Geza eneo ambalo lipo kwenye jimbo langu; maeneo yale tayari wale watu wamiliki wa asili wote walishaondolewa. Wale wamiliki wa asili wameondolewa na waliopo sasa hivi ukienda ukiangalia majina yao hakuna hata mtu mmoja ambaye ni mwenyeji wa Mchinga, hakuna mtu ambaye ni mwenyeji wa maeneo yale. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri suala la upatikanaji wa Hati za Kimila kwa Lindi na Mtwara liwe *priority* kwa sababu ya *potentiality*ya maeneo yale. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kuchauka dakika tano, Mheshimiwa Maftah dakika tano na Mheshimiwa Mbaruku dakika tano.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii ya Ardhi na nichukue fursa kumwomba Mwenyezi Mungu amweke Mbunge mwenzetu ambaye ameitwa mbele ya haki, mahali pema peponi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shida yangu kubwa ni upande huu huu wa migogoro ya ardhi. Pamoja na kwamba Liwale ardhi tunayo kubwa sana, lakini kutokana na uroho wa baadhi ya taasisi wameamua kutuingiza kwenye migogoro mikubwa sana. Sisi Liwale tuna mgogoro mkubwa sana na Selous. Nilikwenda ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, majibu aliyonipa aliniambia kwamba mgogoro huu upo ndani ya Mkoa au Kamishna wa Ardhi, atakaposhindwa ndio atampelekea. Naomba nimwambie kwamba hawezikushindwa akamletea, akimletea maana yake ni kwamba ameshindwa kazi na akishindwa kazi maana yake hataki ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kinakachofanyika pale, ule mgogoro kwa sasa una miaka zaidi ya kumi, haujatatuliwa, sisi na Selous tunagombana. Mpaka sasa hivi watu wanenye wamepoteza maisha, kwenye mgogoro ule kati ya Kijiji cha Kikuyungu pamoja na Selous.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, vile vile tuna mgogoro wa ardhi sisi pamoja na Wilaya ya Kilwa, sehemu ya Nanjilinji. Huu mgogoro nao ni wa muda mrefu sana na mgogoro huu ndio ulionipeleka mimi kwa Mheshimiwa Waziri na akanipa hayo majibu kwamba Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa akishindwa ataniandikia. Mkuu wa Mkoa hawezikushindwa akamwandikia, akishindwa maana yake ameshindwa kazi, lakini bado watu wanaendelea kuteseka. Naomba Mheshimiwa Waziri achukue *initiative* kwenda kutatua huu mgogoro kati yetu pamoja na Kilwa, pamoja na huu mgogoro wa Selous. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba niongelee huyu Kamishna wa Ardhi wa Kanda ya Mtwara. Mimi kwa kweli kwenye Halmashauri yangu ya Wilaya ya Liwale, migogoro

hii kama kweli huyu Kamishna wa Ardhi wa Kanda ya Mtwara, angekuwa anafanya kazi kwa weledi hii migogoro mingine isingekuwepo. Sio hivyo tu, vile vile hata upatikanaji wa hati pale Mtwara; sisi kwanza tuko mbali sana; kutoka Liwale mpaka Mtwara ni umbali mrefu sana, lakini hata ule ushirikiane wake nao ni mgumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano hawa vijana wa Selous Kijiji cha Kikulyungu, walikuja mpaka hapa Bungeni tukawapeleka mpaka kwa Mheshimiwa Waziri na akaturudisha kwa Kamishna. Kamishna mpaka leo anawazungusha hakuna chochote kinachoendelea na wala hawajui waelekee wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huyo Kamishna wa Ardhi wa Mtwara aliokasimiwa madaraka mimi naona kwamba ye ye badala ya kutatua migogoro analimbikiza migogoro, pengine ni kwa sababu ya kuogopa ajira yake, kwamba akionekana ameshindwa basi ataonekana hajafanya kazi vizuri. Kwa hiyo namwomba kabisa Mheshimiwa Waziri kwa nia njema aje Liwale atutatulie hii migogoro ya ardhi kati ya sisi pamoja na Kilwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile kwa upande wa watumishi katika Halmashauri yetu. Halmashauri ya Wilaya ya Liwale kuna mtumishi mmoja tu wa ardhi mwenye sifa, waliobaki wengine si watumishi wenye sifa. Matokeo yake sasa kuna tatizo kubwa sana, unapoingia mahali ambako sasa tunataka tupime ardhi kwa matumizi bora ya ardhi tatizo hilo linakuwa kubwa sana kwa sababu uhaba mkubwa sana wa watumishi wa ardhi katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, si watumishi peke yake na vifaa vile vile. Mara nydingi tunatumia vifaa kutoka Halmashauri ya Nachingwea, kwa maana ya kwamba hatuwezi kufanya kazi pale mpaka tutafute wataalam na vifaa kutoka Nachingwea, ndipo tuweze kufanya kazi pale kwenye Halmashauri yetu ya Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili limesababisha viwanja Wilaya ya Liwale viuzwe ghali sana kwa sababu mara nyingi tunatumia wataalam kutoka nje; badala ya sisi wenyewe kupewa vifaa vya upimaji tukaenda kupima ardhi ili watu wapate viwanja kwa bei nzuri. Kuna tatizo kubwa sana la vifaa vya upimaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ajaribu kuiangalia Halmashauri ya Wilaya ya Liwale hasa kwa upande wa watumishi wa ardhi pamoja na vifaa ili nasi tuweze kufanya matumizi bora ya ardhi. Kwa sababu sasa hivi tunashindwa kupata wawekezaji; mwaka jana tulipata mwekezaji lakini kijiji ambacho ilikuwa aende kikakutwa bado hakijafanyiwa matumizi bora ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jambo hili sehemu nyingi tunakosa wawekezaji kwa sababu vijiji vyetu vingi havijaingia kwenye matumizi bora ya Ardhi. Hakuna mtu ama Kamishna ambaye anaweza akatoa hati kwa mwekezaji kwenye kijiji ambacho hakijapata matumizi bora ya Ardhi. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri aliangalie...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Maftah, ajiandae Mheshimiwa Anna Kilango.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanah wataala*, naomba nichangie kwa dakika hizi tano kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni suala la fidia ya ardhi. Ndani ya Bunge hili hii ni mara yangu ya nne nasimama nikiwa nazungumza suala zima la eneo la Mjmwema pale Mtware Mjini. Eneo ambalo lilichukuliwa na Serikali, Serikali iliyopita na Serikali hii ya Awamu ya Tano wakaahidi kulipa fidia, kuwalipa wananchi wa Mjmwema.

Tangu mwaka 2013 walipochukuliwa yale maeneo yao wale wananchi wamekatazwa kulima maeneo yale wala kuendeleza maeneo yale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaleta swali mara mbili ndani ya Bunge hili na Serikali ikaahidi kwamba itaenda kulipa mwaka jana baada ya bajeti tu. Hata hivyo jambo la kusikitisha sana, baada ya kumalizika kwa bajeti naambiya Serikali haiwezi kulipa. Sasa nashangaa sana, yaani Serikali hii inachukua maeneo ya wananchi zaidi ya miaka mitano sasa tangia mwaka 2013, halafu inaahidi kulipa na hatimaye inakuja inawaacha njiani, inasema haiwezi kulipa fidia Halmashauri wenyewe ndio waende wakalipe fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo sana, wananchi wa Mjmwema, Mtwara Mikindani wanasiitika sana kwa sababu wamekosa kuendeleza yale maeneo kwa ahadi kwamba Serikali itawapa fidia, lakini mpaka leo Serikali inasema haiwezi kufidia wakati ilishaahidi hapa. Mimi nina *Hansard* mbili; ndani ya Bunge hili Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi ikisema inaenda kulipa fidia watu wa Mjmwema. Naomba safari hii Mheshimiwa Waziri atupe majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana nilimpongeza sana hapa Mheshimiwa Waziri kwa mpango kabambe wa Mtwara, lakini katika hili Mheshimiwa Waziri Lukuvi ametuangusha wananchi wa Jimbo la Mtwara Mjini. Naomba hizo pesa kama ni Waziri wa Fedha ampatie hizo pesa ili aweze kuwalipa wale wananchi. Wananchi wanalia sana, wananchi wa Mjmwema, Mtwara Mjini hawawezi kuchukuliwa kwa siku zote hayo maeneo yao halafu Serikali inawaacha njiani kwamba haiwezi kulipa, haiwezekani. Serikali hii haisemi uongo na hili ni Bunge, *Hansard* mbili zimezungumza hapa kwamba tunawalipa lakini wanasema hawawezi kulipa ni jambo la ajabu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, naomba kuzungumzia suala la urasimishaji, tunashukuru kweli mpango huu wa urasimishaji Mtwara ni Mji wa pili na urasimishaji

unaendelea pale Mtwara. Hata hivyo, niseme Mheshimiwa Waziri kwamba vifaa hajatusaidia, kwamba wale wanaopima hawana vifaa nya kutosha, kwa hiyo kasi imekuwa ndogo sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya mwaka hivi sasa na maeneo waliyopima ni machache mno pale Mtwara mjini. Kwa hiyo nimwombe Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Lukuvi kwa sababu ni msikivu sana tunamwaminia, naomba atupe vifaa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ili urasimishaji uende kwa kasi katika maeneo ya Chipuputa, maeneo ya Kiholo, maeneo ya Komoro, maeneo ya Magomeni, Kata ya Ufukoni; tunataka urasimishaji kwa sababu wale wananchi walijenga kiholela holela. Kwa hiyo tunaomba vifaa ili kazi iweze kuendana na maagizo yake ambayo ameyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo llingine ambalo naomba kuzungumza ni suala la migogoro ya ardhi. Ni kweli kwamba hata pale kwetu Mtwara bado lipo na mwaka jana Mheshimiwa Waziri nilimweleza suala la yule jamaa tapeli, anaitwa siju Azimio, sijui nani sijui, maeneo mengi amefuta hati zake, lakini Mtwara mjini eneo la Libya mpaka leo wale wananchi walinyang'anywa na bado Mheshimiwa Waziri Lukuvi pamoja na usikivu wake Mtwara Mjini amekaa kimya juu ya mgogoro huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule tapeli naona kaenda mahakamani sasa hivi kwa sababu yale maeneo alichukua kinyume na taratibu. Yaani watu wamelala, wanaamka asubuhi wanakuta *beacons* zimebekwa pale; mwaka jana nilizungumza hapa. Kwa hiyo hili suala halihitaji mahakama, linahitaji yeye kama Waziri kwa mamlaka yake aliyopewa aende akachukue yale maeneo awarudishie wananchi wa Libya Mtwara Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wananchi wanalia sana na yule ni tapeli na Mheshimiwa Waziri tumeshamsikia anazungumza katika maeneo mengi kwamba huyu tapeli lazima maeneo aliyochukua yarudishwe kwa wananchi. Kwa

hiyo, hili suala la mgogoro wa Libya Mtwara Mjini Mheshimiwa Waziri mwaka huu aende akatusaidie wananchi wale wapate lile eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna mgogoro ambao nao nilizungumza mwaka jana, naomba utusaidie Mtwara Mjini juu ya suala hili ili wananchi wapate haki zao, kwa sababu Serikali zilizopita huko nyuma zilikuwa ni Serikali za kudhulumu wananchi, ilikuwa ni udhulumati, wananchi wananyang'anywa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nilikuwa nataka kuzungumza ni suala hili la mashamba ya walowezi. Tanzania hii kuna maeneo mengi ambayo yalikuwa ni mashamba ya walowezi. Hata pale Lindi ukija *Kikwetu Estate* pale lile shamba ni kubwa sana. Wananchi wanahitaji maeneo waweze kujenga nyumba, wanahitaji kuendeleza pale Kikwetu pale Lindi, lakini wanasesma lile ilikuwa ni shamba la mlowezi mmoja kamuuzia Mohammed enterprises.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa haliendelezwi na Mheshimiwa Waziri ameshatamka kwamba kisheria kama mtu hajaendeleza kwa muda fulani basi yale maeneo yanarudishwa kwa wananchi. *Kikwetu Estate* wananchi wanahitaji kujenga pale, wanahitaji kulima pale. Niombe sana kwa sababu yalikuwa ni mashamba ya walowezi huko nyuma tunaomba yarudishwe kwa wananchi ili waweze kuyaendeleza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa mama Anna subiri dakika kidogo tu, Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hii kupata nafasi ya kuchangia katika Wizara hii. Niseme tuu kwamba *this is a noble chance for me* kwa

sababu nimeomba Wizara karibu tano, lakini hii ni Wizara yangu ya mwisho ambayo niliomba na ndio mwanzo kupata leo. Nashukuru sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Waziri pamoja na Naibu wake pamoja na watendaji wote wa Wizara, kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. Niseme tu kwamba Wizara hii ina changamoto nyngi sana na ni Wizara ambayo ni ngumu sana kwa sababu ardhi ni rasilimali ya Watanzania wote na kila mtu anategemea ardhi kufanya shughuli zake. Sasa kama hatukupata watu, watendaji kama Waziri na Naibu waliopo hivi sasa, basi kwa kweli hayo malengo ambayo tunategemea kuyafikia tunaweza tusiyafikie kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka makubwa sana, kwamba ule uchumi amba malengo ya Serikali ya awamu hii tumekusudia kufikia, uchumi wa kati na uchumi wa viwanda, huenda hatutoufikia kutokana na matatizo ya ardhi. Matatizo ya ardhi bado ni makubwa mno na Serikali inashindwa kwa kweli Serikali inashindwa kutatua migogoro mingi ya ardhi ambayo ipo. Ukilingenisha labda Mheshimiwa Waziri atatuambia; hii migogoro kwa sisi watu wa nje tunavyoona ni kwamba badala ya kupungua, inazidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna migogoro mingi kati ya wakulima na wafugaji; kuna migogoro mingi kati ya wafugaji na watu wa hifadhi; kuna migogoro mingi hata katika taasisi za Serikali. Sasa, sitegemei au hatutegemei kwamba huko ambako tumelenga kufikia tunaweza tukafikia. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wasiwasi wangu ni kitu kimoja, kwamba kama ardhi ni tegemeo la watu wote nina wasiwasi kwamba kunakosekana *coordination, coordination* ya Taasisi za Serikali hakuna, kwamba kila taasisi inawania kipande hicho hicho cha ardhi lakini hakuna mtu ambaye ana-*coordinate* matumizi hayo ya ardhi. Sasa hili ni tatizo na inawezekana hili ndilo jambo ambalo linatusababishia migogoro mingi katika matumizi yetu ya ardhi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingekuwa tunafuata utaratibu mzuri wa matumizi ya ardhi, kuna mbinu nyingi nyuma ambazo zimeweza kutumika/kuanzishwa ambazo zingeweza kutusaidia katika utatuzi wa migogoro ya ardhi. Kwa mfano, kuna mambo ya mbinu hizi za *agro-forestry* ambazo ni matumizi bora ya ardhi, tuliianzisha lakini utekelezaji wake unaonekana kama ni wa kusuasua. Pia kuna *conservation agriculture* ambacho ni kilimo kinachotumia ardhi vizuri, kinaonekana kwamba kimeanzishwa lakini uendelezaji wake ni wa kusuasua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mambo kama haya ambayo labda tungewaweka watumiaji wa ardhi kwenye eneo dogo tu wakaweza kutumia kwa pamoja, tukapunguza migogoro; sasa tunaanzisha halafu tunaacha. Tafiti zinaonesha kwamba haya mambo tukiyatumia vizuri kwa kweli tunaweza tukaenda vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa niligusie ni kuhusu bajeti. Bajeti ya Wizara hii inaonekana kwamba kila mwaka inashuka. Sasa bajeti inashuka; pamoja na kwamba bajeti ni ndogo lakini kile kima ambacho kinakisiwa pia hakitoki kikawaida. Kwa kweli ni jambo ambalo tunaifanya Wizara hii ishindwe kutekeleza kazi zake kama ambavyo imepanga kufanya. Napata mashaka makubwa kwamba utendaji wa Wizara hii unaweza ukawa mbovu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie ni kuhusu *Programu ya Land Tenure Support*, ambayo ni nzuri na imeonekana kwamba inafanya vizuri. Hata hivyo, kwa sababu ya mfumo tu wa Serikali inaonekana kwamba hatuiendelesi. Ingawa Waziri ameigusia gusia katika kitabu chake lakini kuna *technology* inaitwa *MAST...*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

**MHE. MBAROUK SALIM ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna wageni 45 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ambao hawakuwepo Bungeni ambao ni wanafunzi wa madrasa ya Shafia kutoka Chang'ombe Jijini Dodoma wakiongozwa na Mkuu wa Madrasa Ustadh Hamis Itara. Karibuni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Anne Kilango na Mheshimiwa Daniel Mtuka ajiandae.

**MHE ANNE K. MALECELÀ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi kuchangia Wizara hili muhimu, Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme ukweli, nimekuwa hapa Bungeni tangu mwaka 2000. Tumekuwa tuna migogoro mingi sana ya ardhi kuanzia mwaka 2000 mpaka sasa hivi ni mwaka 2018. Nimpongeze Mheshimiwa Waziri Lukuvi, amepunguza migogoro ya ardhi kwa kiwango kikubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme ukweli Mheshimiwa Waziri William Lukuvi, anachapa kazi sana. Anafanya kazi kubwa sana, lakini sio kwamba achukue sifa zote peke yake, ana mke wake ambaye anamwangalia vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi natoka Mkoa wa Kilimanjaro. Mkoa wa Kilimanjaro una wilaya saba. Ndani ya wilaya saba, Wilaya ya Same iko hapo ambayo katika ardhi inachukua takriban asilimia 40 ya ardhi ya Mkoa wa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wilaya ya Same asilimia 68 iko milimani, asilimia 32 iko tambarare. Tuna matatizo

makubwa mawili ambayo ndiyo yamenifanya nisimame hapa, Nianze kwa kusema kwa Mheshimiwa Waziri; Same tunamwita aje aone matatizo yetu. Haya matatizo ni matatizo yako sehemu kubwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kata mbili, Kata ya Makanya ambayo iko Same Magharibi, kata hii tangu mwaka moja elfu mia tisa, kwanza *population* ya Kata ya Makanya ni takriban wananchi 15,000 kwa sensa ya mwaka 2012. Kwa hiyo, ni Kata yenye watu wengi sana. Kuna tatizo kubwa sana la ardhi pale kwenye Kata ya Makanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna haya mashamba ya mikonge ambayo watu wengi tunayalalamikia kwamba yame-end up kutokuwa na tija kwa wananchi kwenye kata zetu. Kata ya Makanya ni kata yenye matatizo ya mafuriko ya mara kwa mara. Lile eneo zuri kwenye Kata hii ya Makanya ndilo eneo ambalo lina mkonge, la mwekezaji ambaye simjui ni nani lakini ni mwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu mwaka 1994, wakati huo Waziri wa Ardhi akiwa ni Mheshimiwa Edward Lowassa, kama sikosei, wananchi wa Kata ya Makanya, Kijiji cha Makanya walileta maombi kwamba wapatiwe ardhi takriban hekta 30, kwa sababu ile ardhi wanayoishi wao ndiyo ardhi ambayo ina mafuriko mara kwa mara. Kwa hiyo, hili tatizo ni kubwa sana kwa Kata ya Makanya. Mheshimiwa Waziri, namnyenyeka, aje aione kata ile, aone wananchi wanavyoteseka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, hawana eneo la makazi, pili, ukiangalia kama unatokea Hedaru kwenda Same ardhi kbwa ya Makanya huku kando ya barabara ni kilimo cha mkonge. Vijana wa Kata ya Makanya nao wangependa kufanya biashara kandokando ya barabara ya lami, lakini kandokando ya ile barabara ya lami kuanzia Makanya mpaka Same ni mashamba ya mkonge ambayo nina uhakika hayana tija kwa wananchi wa Kata ya Makanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimetumwa na wananchi wa Same nimwite Mheshimiwa Waziri aje Same na mimi nitakuwepo Same. Tuzunguke Kata ya Makanya aone ni kiasi gani wananchi wa Kata ya Makanya, Same ya Magharibi wanapata adha kwa ajili ya yale mashamba ya mkonge. Mheshimiwa Waziri nafikiri *messageameipata* vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Makanya ni kata ambayo mara kwa mara Watanzania mnasikia mafuriko, ni kwa sababu ardhi ile ambayo ni nzuri ndiyo yenye mkonge na ardhi ambayo ina mafuriko ndiko wanakoishi wananchi. Mheshimiwa Waziri nimalizie hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi Kata ya Ndungu. Tangu Bunge zima la Kumi nimekuwa nalalamikia Kata ya Ndungu. Kata ya Ndungu asilimia kubwa ni mashamba ya mkonge pia; vijana wa Kata ya Ndungu hawana sehemu ya makazi, hawana sehemu ya biashara, ni mashamba ya mkonge. Mheshimiwa Waziri, nimemwona anazunguka Tanzania, anafanya mikutano mpaka saa sita usiku; namsihi aje kwetu Same, tunamsubiri, tunamsubiri atapata zawadi ya mpunga, atapata tangawizi, aje aone matatizo ya ardhi, mashamba ya mkonge yametuzidi, lakini hayana tija kwa Kata ya Makanya na Kata ya Ndungu. Karibu Same tunakusubiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtuka, wajjandae Mheshimiwa Mwakasaka na Mheshimiwa Stanslaus Mabula.

**MHE. DANIEL E. MTUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu katika bajeti hii ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Niwapongeze sana Waheshimiwa Mawaziri hawa wawili, Waziri Lukuvi na Naibu wake, dada yangu Mabula, anafanya kazi kubwa sana kwa sisi wataalam kwa kweli wanatufurahisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shukrani hizo, nina maombi mawili/matatu. Ombi la kwanza nianze na Wilaya yangu ya Manyoni. Nimejaribu kupekua kitabu hiki cha bajeti cha Mheshimiwa Waziri, nimefurahishwa sana na mipango hii kabambe ya uendelezaji wa miji na naziona juhudi katika wilaya nyingine. Hata hivyo, mara nyingine nimekuwa nikiimba sana na kuomba na kulia kwamba hebu itazameni na Manyoni katika mipango hii kabambe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalia kwa sababu Manyoni naitazama iko karibu na Dodoma, Manyoni pale ni kama *hub* ya mkakati wa maendeleo. Dodoma itakapojaa, mahali pazuri pa kupumulia ni pale Manyoni na si mahali pengine; kwa nini wanakuwa wanairukaruka? Nimechambua sana na naona Manyoni iko *sidelined*. Naomba sana wajaribu ku-concentrate Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Manyoni pale tukiweka mipango kabambe tuna nafasi za viwanda, nimehangai ka katika juhudi zangu binafsi, nimewasiliana na Walimu wa Morogoro, tumepatiwa wanafunzi pale, tunahangaika sana kuwalisha, kuwatunza kidogo angalau kwa bei nafuu, lakini bado tunazidiwa na juzi walikuwepo pale wameondoka jana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba mkono wa Serikali basi, hebu tuipange Manyoni, kwani kuna shida gani Manyoni? Naona wanaruka tu, wakienda wanapita Manyoni kama vile hawaioni, wakati ile ni *hub* nzuri kwa maendeleo wapange ule mji, utatusaidia sana utasaidia maendeleo ya Dodoma hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naliongea kwa uchungu kwa sababu nimekuwa nikifuatilia kwa muda mrefu na mimi ni mtaalam; sasa ninapoona maeneo mengine yanapewa huduma lakini Manyoni inarukwa na iko karibu na ni *strategic position* Manyoni pale, inaniumiza na inawaumiza watu wa Manyoni. Mheshimiwa Lukuvi, naomba hebu aikumbuke Manyoni, *please*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nalo niseme, nimeona katika ukurasa wa 45 Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, tumeona *TANAPA* walivyojitoa sasa kusaidia vijiji. Nikiona namba ya vijiji vile 392, sijajua, hakuna mchanganuo, sijui kama Manyoni pia ipo kwa sababu *TANAPA* inasaidia hivi vijiji ambavyo vimepakana na hifadhi za misitu, wanyama. Manyoni inavyo vijiji 12, sasa sijui kama Manyoni na vijiji ndani ya Manyoni ni mionganini mwa hivi vijiji 392.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana, tafadhali, kama havipo hebu wavitezame waviweke, wasiipitepite Manyoni hivi hivi, Manyoni ni Mji mzuri mmo, tunauita Ghana ndogo ile. Manyoni kwa wanahistoria ndiyo wilaya ya kwanza kuwa na Mkuu wa Wilaya Mwafrika, tuikumbuke Manyoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia katika Mpango huo huo ukurasa wa 45, hawa wenzetu wa misitu, pia nao wanasaidia katika upangaji wa matumizi bora ya ardhi. Naomba pia katika vijiji 50, sijajua kama Manyoni pia ipo, watusaidie kuipanga Manyoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho niombe tu kwa ujumla kama ambavyo katika hotuba zote za bajeti za mwaka jana, mwaka juzi, mwaka huu, wanazungumza maneno mazuri sana, kwamba kupangwe matumizi bora ya ardhi katika nchi hii ili kupunguza migogoro; hebu wapunguze maneno sasa twende kwenye vitendo. Mimi napenda sana vitendo kuliko maneno, ndiyo maana huwa siongei sana, napenda sana kutenda, wakatende.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hayo ndiyo mafupi ambayo nilikuwa nataka kuchangia. Nashukuru sana kwa nafasi hii. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, wajiandae Mheshimiwa Mabula na Mheshimiwa Shekilindi.

**MHE. EMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye hii Wizara muhimu na nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabla ya mchango wangu nianze kuipongeza hii Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Wizara ya Ardhi kwa kweli kuna changamoto nyingi, lakini Mheshimiwa Lukvi na Mheshimiwa Mabula wanafanya kazi nzuri, nawapongeza sana. Hamuiangushi Serikali ya Awamu ya Tano. Pamoja na pongezi hizo, naomba niende kwenye changamoto moja kwa moja ambazo zimekuwa zikiakili Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro ya ardhi kwakweli imekuwa ni mingi. Pamoja na kwamba mingine inapungua lakini mingine imekuwa ni ya kawaida. Kwa mfano, tunapoongelea suala la watu kupewa ardhi, watu wawili au watatu au wateja wawili au watatu yaani (*double allocation*) hili jambo ni la muda mrefu, lakini wanaosababisha hivyo ni hao hao watendaji wetu wa ardhi ambao wameaminiwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi wasiwasi au mashaka yangu ni zile hatua wanazochukuliwa hawa watendaji ambao wamekuwa wakisababisha hii Wizara kupata matatizo mengi sana hasa haya ya *double allocation*. Sioni kama ni sahihi kumuhamisha mtu baada ya kufanya matatizo sehemu fulani anapelekwa kwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona wangechukuliwa hatua ambazo zitawafanya hata wengine wasiwe na ile kwamba atafanya makosa kama hayo ya (*double allocation*) halafu anajua kabisa kwamba mimi hapa watakachofanya kama sio kuniteremsha cheo, watanihamishia sehemu nydingine. Hawa wachukuliwe hatua kali kwa maeneo waliyopo ili kuwapunguzia wananchi matatizo haya yanayojitokeza mara kwa mara. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala hili la wenye uwezo. Wamekuwepo watu mbalimbali ambao wanavamia

maeneo ya watu ambao hawana uwezo. Mtu anakwenda, anajenga eneo la mtu ambaye anajua hana uwezo kwa kutegemea kwamba; anasema huyu ataenda Mahakamani na akienda Mahakamani anajua yeye kwamba kwa uwezo wake aidha anaweza kukawiza kesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu kuna mahali inafika mtu anamdhulumu mzee ardhi halafu anaanza kumhesabia miaka. Mathalani, mtu ana miaka kama 60, mtu anasema muache tu aende Mahakamani, akienda Mahakamani huyu hata kabla kesi haijkwisha huyu atakuwa ameondoka. Sasa vitu vya namna hii vinafanyika, naomba Wizara waweze kuviangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nije kwenye wangu wa Tabora na hasa Tabora Manispaa. Katika eneo hili, Mheshimiwa Lukuvi na Mheshimiwa MAbula, wamekuja Tabora mara nyingi, nawapongeza kwa hilo. Migogoro mingi ya ardhi iliyopo Tabora wanaifahamu, lakini ile migogoro mingi pia imesababishwa na watendaji wa ardhi pale Tabora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba lifanyiwe uchunguzi, waporaji wengine wa ardhi ni miongoni mwetu, kwamba ni viongozi tena wengine ni viongozi wa chama ambao nadhani Mheshimiwa Lukuvi anakumbuka alipokuja Tabora hata Mheshimiwa Mabula walikumbana na kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini basi isifike mahali Serikali ikaanza kufanya uhakiki kama kunavyofanyika uhakiki mwingine. Uhakiki wa wamiliki halali wa viwanja vile. Inawezekana na sioni ugumu kwa sababu kuwatambua watu ambao wamefoji viwanja vile ni kufanya uhakiki. Ningependekeza hicho kwamba ufanyike uhakiki wa maeneo yenye migogoro ili ionekane ni nani hasa wamiliki wa vile viwanja kwa sababu hili tatizo lipo nchi nzima. katika maeneo mbalimbali viongozi wanajitwalia ardhi kwa kutumia vyeo vyao lakini wanaandika majina tofauti tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati viwanja kwa mfano vinagaiwa tuseme kwenye halmashauri au manispaa viongozi wanajitwalia viwanja vingi tu. Mtu mmoja anaweza akachukua viwanja hata 30 kwa majina tofauti halafu baadaye anaanza kuvuza kidogo kidogo kwa bei kubwa ya kuwaumiza wananchi. Sasa kwa nini lisifanyike zoezi la uhakiki kuwabaini hawa ili vile viwanja vingine wanapobainika pamoja na hatua za kisheria kuchukuliwa kwa wao kufoji majina mbalimbali lakini pia kuwapa wale ambaao hawana uwezo wa kumiliki hivyo viwanja?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kwa pale sisi Tabora Manispaa tuna bahati mbaya, kwa upande mwingine bahati nzuri kwamba tunazungukwa na majeshi lakini pia tunazungukwa na hifadhi. Kumekuwa na migogoro ya muda mrefu ya ardhi kati ya wananchi pamoja na wanajeshi, kwa maana ya mipaka ile ambayo kwa muda mrefu hajaoanishwa sawasawa, ni nani hasa ambaye anastahili kuwa na eneo lile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wananchi wamekuwa wakilima muda mrefu, wale ambaao wanapakana na maeneo ya majeshi, lakini hivi karibuni imetokea suala la jeshi kudai kwamba yale maeneo ni yao, ambayo wananchi wamekuwa wakilima zaidi ya miaka 40 pale. Sasa naiomba Wizara ya Ardhi kwa kushirikiana na Wizara ya Ulinzi, waweze kufanya haraka zoezi la kupata ramani zile ili kujuu ni nani hasa ni mmiliki wa maeneo gani na kwa mipaka gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba hilli suala la hifadhi, hifadhi wote tunazihitahiji, wote tunahitaji utalii, tunahitaji kutunza misitu, lakini kuna sehemu kubwa ambayo wananchi wanafanyiwa uonevu. Wako wananchi miaka na miaka kabla hata ya hayo maeneo ya hifadhi hayajatamkwa bayana. Leo hii wanaondolewa maeneo ambayo hawajua sasa watakwenda wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba pia Wizara hii kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii waweze

kuona ni wapi wananchi wale sasa haki yao ipo. Nadhani baada ya haya machache ambayo yanajitokeza kwenye suala hili, kama yakifanyiwa kazi nadhani tutaweza kuwa tume-solve hili suala...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya machache, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mabula, wajiandae Mheshimiwa Shekilindi na Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana nami kupata nafasi angalau ya kuchangia mchana huu maneno machache juu ya Wizara hii muhimu kabisa katika maisha ya Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini niwapongeze sana na nianze na pongezi kwenye Wizara hii. Nimshukuru na nimpongeze sana Waziri wa Ardhi pamoja na Naibu wake, pamoja na Watendaji wao wote kwa namna ya kipekee wanavyofanya kazi lakini kwa ubunifu wa hali ya juu ambao wamekuwa wakiunesha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wenzangu watakubaliana na mimi, kwa mara ya kwanza safari hii tumeona maonyesho makubwa hapa ndani ya Bunge yanayoendana sambamba na taasisi mbalimbali za kifedha ambapo kwa maana ndogo kabisa sisi Wabunge tumepata fursa za kujua vitu ambavyo pengine ingetuchukua zaidi ya siku nyingi kupata fursa ya kwenda kwenye benki, taasisi hizi za *National Housing*, sijui *Watumishi Housing* na nyingine nyingi kujadili na namna ya kuona namna ya upatikanaji wa mikopo ya ujenzi wa nyumba zenyenye gharama nafuu, mimi niwapongeze sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, niongelee kuhusu *National Housing*. Nitumie nafasi kuiomba sana Serikali; tunafahamu *National Housing* Serikali imewekeza fedha nyingi na msingi wake mkubwa ni kuendeleza Shirika hili liweze kujitegemea. Vile vile iko miradi na Kamati imesema vizuri, miradi mingi mikubwa, mizuri, imefanyika kwa muda mrefu na mingine imesimama fedha bado hazijakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaiomba sana Serikali waliunge mkono Shirika hili ili liweze kutimiza wajibu wake kama ambavyo limejipangia na namna ya kutekeleza shughuli nyingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika 10 ni chache sana, nizungumze sasa juu ya habari ya urasimishaji na umilikishaji wa ardhi. Nirudie tena kusema nampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya. Jiji la Mwanza pamoja na Manispaa ya llemela na Nyamagana tumekuwa watu wa kwanza katika nchi hii, hivi ninavyozungumza tumechapima viwanja zaidi ya 42,563.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika idadi hii ya viwanja zaidi ya hati 13,202 zimeshakabidhiwa kwa wananchi. Nitumie nafasi hii kuwapongeza sana Watendaji wa Ardhi wa Manispaa ya llemela pamoja na Jiji la Mwanza kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya ya kuwashudumia wananchi wa maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya Serikali kuititia mpango ambao waliuanzisha Dar es Salaam na Wizara ikatoa fedha kwa ajili ya manispaa fulani, sitapenda kuitaja jina ili itekeleze mpango wa urasimishaji makazi, kwenye Kitabu cha Mheshimiwa Waziri amesema wamepima viwanja 6,000 wametoa hati 170 peke yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu Nyamagana na llemela wamefanya kazi kubwa, tunaombia Mheshimiwa Waziri awaunge mkono kwa kuwaongezea fedha nyingi zaidi ili waweze kufanya kazi hii kwa umakini

mkubwa na wasiendelee kusuasua kama ambavyo wanajitahidi sasa pamoja na kazi kubwa sana hii wanayoifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo lingine juu ya namna nzima ya kushughulika na masuala ya utoaji katika suala nzima la umilikishaji. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, alipunguza ile gharama ya *premier* kutoka 7.5 mpaka 2.5 na sasa Kamati imeomba angalau iwe *one percent*, nami niendelee kusisitiza hapo aiangalie kwa upana na aweze kuona namna ya kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *program* ya ununuzi wa vifaa vya upimaji; Mheshimiwa Waziri ameongea kwenye Ukarasa wa 36, ni jambo nzuri sana kwa sababu atapunguza gharama za upimaji wa maeneo mengi kwenye manispaa zetu na halmashauri zetu. Hii itamsaldia mwananchi kulipa gharama nafuu sana ili sambamba na wakati tulionao sasa aweze kupima maeneo mengi zaidi. Vile vile kila Mwananchi apime akiwa na uhuru mkubwa ili aweze kujisaidia wakati fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ahadi hii itekeleze. Nafurahi kuona na nimpongeze tena, amesema mwezi wa Saba tunapoanza mwaka mpya wa fedha, fedha hizi na vifaa hivi vitakuwa vimeshapatikana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Master Plan*, nchi hii imekuwa ikitengeneza *Master Plan* nyingi, imekuwa ikitengeneza michoro mingi, lakini Mheshimiwa Waziri hakuna mpango mkakati wa kuhakikisha *Master Plan* hizi zinatekelezeka kwa wakati na matokeo yake tunaendelea kuchochaea migogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna nyingine, kama *Master Plan* hizi hazitafanya kazi kwa haraka, utekelezaji wake ukawa nyuma hatuwezi kufanikiwa kwenye malengo tulioyoyakusudia. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri tuweke msisitizo na tuimarishe maeneo haya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kwenye mpango mkubwa ambao tunaufanya sasa wa mpango wa miji mikubwa. Kwenye miji yetu mingi tunayo changamoto moja kubwa, mpango kabambe ni mzuri, lakini hebu tuangalie, wako wananchi kwenye maeneo fulani hawawezi kupimiwa na kupewa hati zao. Sasa hii itakuwa ngumu sana kwa mwekezaji anayekuja kuja kukutana na mtu ambaye si mmilikia halali, hana *document* ili aweze kumiliki eneo lile na kwenda sambamba na mpango kabambe tuliouandaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala litatukwamisha; yako maeneo ya Kata za Isamilo karibu mitaa name na mitaa mitano kwenye Kata ya Mbugani pale kwenye Jimbo la Nyamagana. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri aangalie na wajadiliaje vizuri, waone namna ambavyo tunaweza kumsaidia mwananchi huyu kwenye Kata hizi mbili za Mbugani na Isamilo ili naye awe kwenye mpango kabambe...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shekilindi, wajiandae Mheshimiwa Mgumba na Mheshimiwa Maulid Mtulia.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia Wizara ya Ardhi. Kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya na nguvu mpaka kuweza kuchangia katika Hotuba hii ya Wizara ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Lukuvi na timu yake kwa ujumla, pamoja

na Naibu Waziri Mheshimiwa mama Angelina Mabula kwa kazi kubwa wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Waziri na timu yake wanafanya kazi kubwa sana, na-*declare interest* kwamba mimi nipo kwenye Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii. Tulitembelea juzi miradi ya *NHC* pale Dar es Salaam, tuliona mambo makubwa sana. Wakati huku ndani watu walikuwa wanasema kwamba Mradi wa *NHC*, Mradi wa nyumba unakufa, lakini mradi upo vizuri. Nikupongeze Waziri endelea na kasi hiyo hiyo. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeona mfumo wa upimaji ardhi mpya ambao unaitwa *ILMIS*, mfumo ule ni mzuri, naamini kabisa utaondoa ile zana ya kudhulumiwa hati au wale wajanja wajanja sasa wanaotaka kuuza viwanja vya watu itakuwa sasa haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo niendelee kuchangia sasa katika suala la upimaji ardhi. Lushoto ni eneo ambao lina wakazi wengi sana, wanahitaji kupimiwa ardhi na wanahitaji hati. Hata hivyo upatikanaji wa hati katika Halmashauri ya Lushoto, tuseme Wilaya kwa ujumla ni mgumu sana. Nimwombe Waziri sasa, pamoja na kwamba ana mpango mzuri wa kupeleka vifaa vya kisasa kupima maeneo ya Lushoto, basi nimwombe aharakishe ili wananchi wa Lushoto waweze kupata hati zile. Maana kupata hati Lushoto ni sawasawa na kuokota dhahabu chini ya mchanga, ni ngumu sana, lakini kwa mfumo huu Waziri anaokuja nao naamini kabisa sasa mambo yatakuwa ni mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nimwombe sasa Waziri katika mfumo huu wa *ILMIS* usiishie Dar es Salaam tu, hebu uende kwa Kanda, wagawe Kanda ndani ya Tanzania hii ili uweze kwenda kwa kasi kwani mfumo huu ni mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la hati. Nilienda Dar es Salaam kwenye mtaa mmoja wanaita Kilungule A na B. Tulikuta wananchi wa Kilungule A

walioomba hati ni 600, lakini ambao wameenda kuchukua hati ni 176, kumuuliza Waziri akasema hati zote 600 zipo. Baada ya kuwaauliza wananchi wale wakasema kwamba hawana pesa za kulipia gharama ya hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sasa nimwombe Mheshimiwa Waziri hizi gharama za kulipia hati hebu ziangaliwe upya maana ni gharama kubwa, wananchi wale wanasema kwamba kupimiwa ni Sh.300,000 wakajumuisha pamoja na hati kwamba gharama yote ni Sh.300,000, matokeo yake kufika kule katika kuchukua hati wanaambiwa kuwa, kuna gharama za hati na kuna gharama za upimaji. Kwa hiyo hili niiombe sasa Serikali iangalie upya ili ipunguze wananchi wale waweze kupata hati kwa bei rahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende kwenye Mabaraza ya Ardhi. Kule Lushoto namshukuru Waziri Lukuvi alituwekeea Baraza la Ardhi, lakini Baraza la Ardhi lile mpaka sasa hivi halina Mwenyekiti, Mwenyekiti anatoka Korogwe. Kwa hiyo nimwombe sasa Mheshimiwa Waziri apeleke Mwenyekiti katika Baraza lile la Ardhi kwani kuna msongamano mkubwa sana katika Baraza la Ardhi la Lushoto na wananchi wengi wanatoka maeneo mbalimbali na maeneo ambayo kwa kweli wanafika pale huenda kwa siku moja au siku mbili. Kwa hiyo nimwombe sasa Waziri anisaidie kupeleka Mwenyekiti katika Baraza lile la Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la mipaka. Sisi na Kamati yetu tulienda maeneo ya Mtukula kule mpakani mwa Uganda na Tanzania; tuliona vile vizingi vya mkoloni ni vizuri kuliko vizingi vinavyowekwa na Serikali. Kwa hiyo ningeomba Serikali yangu sasa itumie *modal* ile ya vizingi vile vya mkoloni. Kwanza vizingi vile viimarishwe *then* viwekwe vya kutosha katika maeneo yote ya mpakani katika mipaka yetu yote ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo kuna mipaka kwenye maziwa; mipaka yetu kwenye maziwa haijulikani, kwa hiyo niombe Serikali yangu iweke maboya

yale sasa kwenye maziwa ili wananchi wetu wanapoenda kuvua katika maziwa yale wasiingie katika maeneo ya watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mgumba, wajiaandae Mheshimiwa Mtulia na Mheshimiwa Kigola.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na mimi kwa kunipa nafasi nichangie hoja hii iliyokuwa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kwanza na mimi niwapongeze sana Wizara ya Ardhi, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Pamoja na changamoto kubwa ya migogoro mingi iliyokuwepo kabla lakini kwa kasi wanayoenda nayo tunaimani siku moja itakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme mimi ni mmoja wa Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii, lakini ushirikiano tuliuopata kutoka kwenye Wizara hii katika majukumu yetu ni mkubwa sana. Tulikuwa na ziara na Kamati ya Ardhi kukagua mipaka ya nchi, lakini huwezi kuamini tulipewa ushirikiano na Naibu Waziri, Katibu Mkuu siku zote tulivyokuwa kwenye safari wote tulikuwa nao mguu kwa mguu mpaka tumerudi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulipokwenda Dar es Salaam siku tatu siku zote Waziri mwenyewe Lukvi tukawa naye siku tatu, ni tofauti kabisa na wakati mwingine kwa watu wengine ambao wanasema wako *busy*. Tunashukuru sana waendelee na moyo huo ili kuwatumikia Watanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hayo nina machache leo na zaidi ni ushauri. La kwanza, dhuluma ya

wamiliki ardhi hasa wanyonge hususani Manispaa ya Morogoro. Mheshimiwa Waziri ni mchapakazi na aliwahi kufika Morogoro kwa ajili ya kutatua migogoro hii ya ardhi. Hata hivyo, nataka nitoe mfano mmoja kwa Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya tatizo la njaa mwaka 1974, Mwalimu Nyerere alitaka tuwe na kilimo cha kufa na kupona na akasema kila Mkuu wa Mkoa asimamie suala la uzalishaji wa chakula, anayezembea basi kazi hana. Basi ilitokea siku moja akaenda Mkoa mmoja akakuta kwa sababu mtu nataka asipoteze kazi wakatafuta wafungwa Magerezani, wakatafuta shamba likalimwa, wakachukua mahindi ya wakulima wakayapanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyapanda ili kuonesha kwamba chakula hali safi akapelekwa pale Mwalimu. Sasa kwa sababu Mwalimu uzuri aliquwa anatafuta taarifa mbalimbali, kufika pale akanyofoa tu mhindi mmoja akaona ni feki na yule Mkuu wa Mkoa akapunguzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi, Mheshimiwa Waziri aliwahi kuja Morogoro Manispaa kutatua tatizo la ardhi na kusikiliza changamoto za dhlulma ya ardhi Mkoa wa Morogoro hususani Manispaa; lakini alichofanyiwa hakijui na sasa leo nataka nimwambie. Watu wa Morogoro hasa wamiliki wa ardhi wanyonge walichonganishwa na Serikali yao, lakini sasa wamepata ukweli wanamwomba sana arudi tena akawasilize ili atatute changamoto hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku ile Mheshimiwa Waziri alipokuja Morogoro watu wenye migogoro ya ardhi wakakusanya Ukumbi mwingine, halafu akapelekwa kwenda kuongea na watumishi. Watu walikasirika sana na hili jambo halipendezi, wanaleta chuki kugombanisha Serikali ya Awamu ya Tano na wananchi wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Morogoro Manispaa kuna dhuluma kubwa sana ya ardhi, kazi yote wanayofanya

Mawaziri inaharibiwa na watendaji wao kule chini. Kule chini wakigawa ardhi wanajigawia wao halafu wanauzu kwa watu wengine. Pia hata ile ardhi wanayogawiwa wanyonge, wale Maafisa Ardhi wanaowaleta na Wataalam wa Ardhi hawako kwa ajili ya kusaidia matatizo ya watu, badala yake ni kila siku kupora ardhi ya wanyonge na kuwauzia wenye pesa na wakija viongozi wakitaka kusema matatizo yao wanaminywa, wanakanyagwa kwenye Mikutano na Mabango yote yanachanwachanwa ili wasijue matatizo yanayowakabili Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba sana Mheshimiwa Waziri aje, kuna mchezo mchafu mpaka wanachoma mafaili ya wamiliki halali wa ardhi wanatengeneza hati mpya na mafaili mapya. Mheshimiwa Waziri anione nimpe ushahidi mimi mwenyewe mwathirika, marehemu baba yangu mwathirika, dada yangu mwathirika, majirani zangu waathirika, watu wa Morogoro waathirika. Nitampa hivyo viwanja vyote ambavyo na watu wengine wenye matatizo kama ya kwangu na jamii ya Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni kuhusu fidia ndogo wanayolipwa watu kupisha miradi ya maendeleo hususani vijijini. Kwanza tunashukuru sana Serikali inavyotuletea miradi mingi kwa ajili ya maendeleo hususani huu mradi wa reli inayoenda kasi. Wananchi wetu hasa Mikese *Station*, Ngerengere na Kidugalo ni miongoni mwa waliotoa ardhi yao kwa ajili ya kupisha miradi hiyo. Hata hivyo, fidia waliyolipwa ni *flat rate* 500,000 kwa heka, kitu ambacho ni tofauti na bei ya soko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajiuliza; Serikali hii hii taasisi zake kama *NSSF* au ukikuta *National Housing* wakitaka kujenga nyumba kwenda kununua ardhi wanunua kwa bei ya soko na hiyo bei ambayo haipo popote pale. Natoa mfano tu, mradi kule wa *Dege Beach* ilinunua heka moja zaidi ya milioni 800, kwa kusema *land for equity* hata *National Housing* hivyo hivyo, matokeo yake zile nyumba zinakuwa na gharama kubwa na wanakuja kuumizwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa wananchi wanajiuliza mbona Serikali hii ikitaka kujenga mjini au sehemu yoyote wanunua bei ya soko, lakini wakija kuchukua ardhi yetu huku vijijini wanasema tunalipa bei ya Serikali. Huku wanatumiza wanalipa mapato madogo kitu ambacho leo hii aliyeipwa 500,000 pale kupisha miradi hii hawezi kupata ardhi kama ile ile pale hata nusu ya pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, leo bei ya ardhi pale Mikese ni zaidi ya shilingi milioni nane kwa heka. Natoa mfano, Kampuni ya Mahashree ambayo imewekeza pale Kiwanda cha Mbaazi ilinunua mwaka jana heka moja milioni nane, lakini yenyewe imekuja kulipwa 500,000 kwa heka na Serikali ardhi ile ile, ndani ya mwaka mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa tuwe kama msumeno. Kama bei inayotumika ni 500,000 kote hata huku kwenye taasisi za umma kama *NSSF* na *National Housing* inapotaka kujenga miradi ya maendeleo bei iwe hiyo hiyo ili nyumba hizi ziwe bei nafuu wananchi hawa wapate uwezo wa kuzimiliki hizo nyumba tofauti na sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia bei kubwa ya kodi za ardhi, hili ni janga lingine, kwa sababu Mheshimiwa Waziri yeye mwenyewe ni shahidi, tumekwenda wote Kilungule amepima ardhi bure, lakini watu kwenda kulipia mpaka leo wameshindwa. Hili kama halitaangaliwa vizuri, basi tunakwenda katika njia nyingine ya kumilikisha ardhi kutoka kwa wanyonge kwenda kwa matajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusipotahadhari ardhi hii itamiliwa na wachache Tanzania kwa kisingizio cha Watanzania wengine kushindwa kulipa ardhi kwa sababu kama wanavyosema mtu akishindwa kulipa kodi watampelea Mahakamani, watamnyang'anya ardhi na kweli watawanyang'anya wengi, lakini ndilo lengo la Serikali? Maana yake ni nini, ni kwamba ardhi hii tunaipokonya sasa

kwa wanyonge walio wengi tunapeleka kwa matajiri wachache wenyewe uwezo wa kulipia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri na bora Mheshimiwa Waziri akaweka bei inayoweza kulipwa na wengi ili watu wote walipe kuliko wakiweka bei kubwa watalipa wachache wengine hawataweza kumilikishwa ardhi, kitu ambacho itakuwa ni hatari sana huko mbele. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, Umiliki wa Ardhi Vijijini. Nnafahamu kwenye nyaraka zinaonekena ardhi kubwa inamiliikiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri sana Mheshimiwa. Mengine onana na Mheshimiwa Waziri.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwiningi wa rehema kwa kunijalia mimi pamoja na Wabunge wenzangu kukutana mahali hapa leo na kupata fursa ya kuchangia Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Sambamba na hilo nitumie fursa hii kuwatakia watu wa Jimbo langu la Kinondoni, *Ramadhan Mubarak* na Watanzania kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli, niseme wazi naipongeza sana Wizara hii ya Ardhi kwa kazi kubwa wanayofanya. Nintaje kwa jina mzee wangu Mheshimiwa Lukuvi na Naibu wake, wanafanya kazi kubwa. Kwetu sisi Kinondoni hakuna asiyefahamu kwamba tulikuwa na migogoro mingi sana ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri alikuja pale tukaenda mpaka katika maktaba yetu ile ya ardhi

tukaangalia pamoja, tukaona namna gani baadhi ya watendaji wetu wanavyoikiuka utaratibu katika kutafuta namna ya kuwadhulumu wanyonge wenye ardhi yao na badala yake kuwapa umiliki huo matajiri. Kwa kweli, wamefanya kazi kubwa sana, tunawashukuru sana mwendelee kuchapa kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi leo najikita kwenye jambo moja tu. Jambo langu, kama mnavyojua, Jimbo langu la Kinondoni ni Jimbo ambalo lina kata 10 na kati ya kata hizo 10, kata tisa zote zimepitwa na mabonde na wananchi wangu katika hizo kata tisa wote wanaishi katika maeneo yasjyokuwa rasmi. Kwa hiyo, unapozungumzia suala la urasimishaji, suala la uendelezaji wa miji, suala la upangaji miji na wakati mwingine hata suala la kuleta bomoabomoa kwa ajili ya kutengeneza mji mimi ni mhanga na wananchi wangu ni wahanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitajikita sana hapa na kuiomba Serikali iangalie namna gani inaweza ikatusaidia sisi watu wa Kinondoni na Dar es Salaam kwa ujumla ambao mji wetu maeneo mengi watu walienda kama ni mashamba, lakini leo ni mji na yamepangwa katika mpango usiokuwa bora, tunafanyaje kuboresha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri na nimevutiwa na maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia ukurasa wa 38 Mheshimiwa Waziri anazungumzia Mpango Kabambe wa Utekelezaji wa Miji na katika mpango huo kabambe amelitaja Jiji letu la Dar-es-Salaam. Kwa hiyo, tuna mategemeo makubwa sana watu wa Dar-es-Salaam tutanufaika katika mpango huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda katika ukurasa wa 41 ameanzia ukurasa wa 40 ameendeleza urasimishaji wa makazi holela Jijini Dar-es-Salaam. Kama mnavoyelewa,

kama niliviyotangulia kusema katika Jimbo langu la Kinondoni hayo makazi holela yapo. Kwa hiyo, kwa kweli, nina mategemeo makubwa sana kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kuhusiana na jambo hili. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikienda tena ukurasa wa 47, Mheshimiwa Waziri ameелеza maendeleo ya sekta ya nyumba na hapa napenda kunukuu; Mheshimiwa Waziri anasema:-

*"Wizara yangu ina jukumu la kuratibu uendelezaji wa sekta ya nyumba nchini, sekta hii huchangia kukuza uchumi, kuongeza fursa za ajira na kupunguza umaskini. Kwa kuzingatia hayo Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi, ili kuvutia uwekezaji katika sekta hii na kuwezesha wananchi kumudu gharama za nyumba zilizo bora."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimevutiwa hapa katika Serikali kuwezesha wawekezaji kuja nchini. Sisi watu wa Dar es Salaam, tena hili niseme kwamba naungana na Mheshimiwa Waziri kabisa, tunashirikiana katika Mto wetu Msimbazi. Tunaathirika vile vile katika Mto Msimbazi, lakini vile vile tumeathirika katika Mto Ng'ombe, Mto Kibangu, mito mingi. Jambo hili limesababisha wananchi wangu kuishi katika maeneo ya mito na hata kuvunjiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipokuwa kwenye kampeni tulizungumzia Dar es Salaam mpya. Namwomba Mheshimiwa Waziri aje na mkakati sasa kwa sababu, tukisema kila anayekaa bondeni tumvunje, katika jimbo langu tutavunja asilimia 60 ya nyumba zote zilizokuwa katika Jimbo la Kinondoni. Kama niliviyotangulia kueleza kata tisa zote zina mabonde, tukiamua kwenda kuvunja nyumba maana yake zaidi ya asilimia 60 ya nyumba zote tutakuwa tunavunja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Mheshimiwa Waziri anazungumzia kutengeneza mazingira mazuri ya wawekezaji kuingia; Mheshimiwa Waziri ana mpango gani wa kuhakikisha tunarasimisha makazi haya ya Jimbo la

Kinondoni, ili Kinondoni ile ya kisasa tuliyokuwa tumeihubiri katika kampeni ipatikane?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wananchi nimezungumza nao, wako tayari kutoa maeneo yao kama atapatikana mwekezaji kwa ajili ya kushirikiana. Wao wanatoa maeneo mwekezaji anajenga nyumba za kisasa, ili tuondoe kabisa *squatter* katika Jimbo langu la Kinondoni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na vile vile tumeambwa katika Mto Msimbazi kama kuna mtu, kuna mtu kajitokeza anataka kuwalipa fidia wale watu wanaokaa mabondeni, ili ye ye alitumie jengo lile kwa ajili ya maendeleo. Sasa Waziri anatuambia nini kuhusu kuwapa fursa hawa wawekezaji? Kwa sababu, sisi kama Serikali tukiamua tufanye sisi, maana yake itabidi tukakope hela benki, lakini mwekezaji ameamua aje kuwekeza kwa gharama zake mwenyewe; Serikali ina mpango gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itambue kwamba, Jiji la Dar-es-Salaam lina zaidi ya watu milioni sita, lakini watu hawa wanataabika kwa mifereji ya Mto Msimbazi ambayo Serikali inapaswa kujenga miundombinu wezeshi, miundombinu ambayo itafanya Dar-es-Salaam iwe ya kisasa. Angalia juzi pale imenyesha mvua Jangwani, jiji lote limesimama; hivi kweli, tunasimamisha jiji kwa mradi ule Mto Msimbazi? Hivi kweli Mto Msimbazi hautibiki? Inafika mahali Dar-es-Salaam inasimama kwa Mto Msimbazi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na maelezo ya kutosha namna gani Dar-es-Salaam yetu mpya tunajengwa na hasa wananchi wako tayari kutoa maeneo yao kushiriki...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya, nakuongeza sekunde tano kwa sababu unazungumzia Msimbazi. (*Makofii*)

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mto Msimbazi kama kuna watu wanajitokeza kuwekeza na Serikali ikajiweka mbali wakalipwa fidia wananchi wetu hili jambo litakuwa lina manufaa kwa wananchi na lina manufaa Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Habari ndio hiyo, kuna mwekezaji yuko tayari kusaidia Serikali.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

Waheshimiwa tunaendelea, Mheshimiwa Mendrad Kigola, atafuatiwa na Mheshimiwa Anna Lupembe na ajilanda Mheshimiwa Rashid Akbar.

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana. Kwanza kabisa nianze na pongezi kwa Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri, tumeona kazi nzuri, kila mtu anajua kazi inafanyika vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mchango wangu una mambo machache tu. Jambo la kwanza, Mheshimiwa Waziri, tungeomba kujua vizuri masuala ya ardhi. Tukiangalia kuna Maliasili, kuna Wizara ya Ardhi, kuna sehemu fulani kama tunaingiliana. Kwa mfano sasa hivi ukiangalia kuna migogoro ya ardhi ambayo inajitokeza, watu wa Maliasili wanassema maeneo yale ni yao, tena ukienda Ardhi wanaweza wakasema yale maeneo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kuna mgongano kidogo pale. Ukiangalia watu wa Maliasili wenye wanaangalia vipimo vyatmiya ya 1976. Ukiangalia *population* ya mwaka 1976 tulikuwa Watanzania wachache sana, tulikuwa kama milioni nane, sasa hivi

Watanzania tuko milioni hamsini na nane na kila kijiji ukiangalia sehemu kubwa imechukuliwa na watu wa Maliasili. Wananchi sasa hivi hawana ardhi hata ya kufugia au kulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mimi kwenye jimbo langu, Jimbo la Mufindi Kusini, watu wa Maliasili walichukua maeneo makubwa sana na sehemu nyingine zilichukuliwa na wawekezaji, kwa mfano wakulima wa chai walichukua maeneo makubwa sana. Mfano, ukienda pale Kijiji ha Mtwango wananchi wamekaa tu kwenye barabara ni sehemu ndogo sana, hata kufanya sehemu za kilimo hakuna.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ukienda Kijiji cha Sawala kile wananchi hata kwa kujenga makazi hakuna. Hata tukisema tukafanye upimaji wa ardhi kwa ajili ya wananchi tutashindwa. Sehemu kubwa imechukuliwa na watu wa maliasili. Naomba sasa unapotupa maelekezo masuala ya ardhi tupate ufanuzi kwamba, Maliasili ana uwezo wa kujipimia ardhi au ardhi inapimwa na watu wa Ardhi? Hii itatusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, nimesikia kuna upimaji kule wanafanya vizuri sana, Wilaya ya Kilombero, kuna *program* nzuri sana. Ile *program* nimeipenda na inaenda kwa bei nafuu sana, nadhani wanatumia simu tu kwa bei nafuu, kuna wafadhili nadhani, Waziri anajua, ile *program* ingekuja Tanzania nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri kama anakuja wilaya nyingine namwomba kwenye Wilaya ya Mufindi basi aje apime. Kwa sababu sisi kule, kama nilivyoongea mara ya kwanza kwamba, wawekezaji wengi sana na sasa hivi tuna tatizo kubwa sana la ardhi. Kwa hiyo, tukija kupimiwa matumizi bora ya ardhi, halafu nasikia wanatoa hati bure, ile itatusaidia sana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri angalau atuangalie Wilaya ya Mufindi kwa ile *program* na sisi ije kule. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine kuna upanuzi wa ilikuwa vijiji, sasa hivi imekuwa miji tayari, tunaita miji midogo. Kwa mfano pale Igoole, Nyololo, Mnanga na Kasanga, ile ni miji midogo, lakini kuna upimaji ulifanyika pale. Upimaji ule nadhani watu wa halmashauri walisema wapime, ni upimaji mzuri si mbaya, lakini ukipima makusanyo yote yanaenda kwa halmashauri, hiyo ni njia nzuri na ile fedha tunajua ni *Basket Fund*, halmashauri inagawanya katika wilaya nzima, lakini kijiji husika ambacho kimetoa ardhi hakipewi mgawo mkubwa, kinaweza kikapewa mgawo mdogo sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali, kijiji husika basi kipewe *percent* kubwa, ili waweze kufanya maendeleo makubwa kwa sababu wale ndio waliota ardhi pale. Hii itakuwa imesaidia sana kuondoa migogoro ya ardhi ndani ya vijiji. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine, tuna mgogoro pale kati ya mpaka wa Makambako na Mufindi. Kuna Kijiji kimoja pale Nyigo tunapakana na Makambako. Ukiangalia Serikali ilipatia Kijiji cha Nyigo, mipaka iko Kijiji cha Nyigo lakini wa Makambako na wenyewe wanasesma ni sehemu yao, ule mgogoro ndio sasa unakuwa mkubwa. Naomba Wizara iingilie kati hilo suala la mgogoro wa ardhi ni mkubwa sana na unapanuka. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mwekezaji alitaka kuwekeza pale, lakini bado wananchi pale hawaelewi. Mheshimiwa Waziri nadhani ameiandika imekaa vizuri, lakini wananchi pale hawajui, kwa hiyo wangeenda pale wakawaelimisha wananchi itakuwa imetusaidia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine napongeza ugawaji wa viwanja, wamegawa viwanja vizuri, hata hapa Dodoma wametugawia viwanja vingi sana vya kununua. Hata hivyo mtu ukisema *square metre* moja Sh.6,000/= au Sh.12,000/=, bado hujawasaidia wananchi. Naishauri Serikali waweke bei nafuu, ila labda waweke masharti ya kujenga

kwamba, wajenge nyumba ambayo ni *reasonable*, inaonekana ni nyumba, lakini viwanja wakiuza kwa bei kubwa, kwa mfano, sasa hivi watu wametoka Dar-es-Salaam, wametoka wapi, wamekuja wafanyakazi wamesema hapa ndio makao makuu wajenge nyumba, wanahangaika wanapanga huku na huku nyumba hazieleweki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tusipunguze bei ya viwanja ili watu wajenge nyumba nzuri? Tukisema *square metre* moja Sh.12,000/= au Sh.6,000/=, mtu kusema anunue kiwanja sasa hivi milioni kumi, milioni ishirini, milioni thelathini, anunue kiwanja kwa hali ya sasa hivi nani atanunua? Itakuwa bado. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi napendekeza. Kwa sababu, sisi ndio tunaishauri Serikali, vile viwanja kwa *square metre* moja hata ukifanya Sh.3,000/= kwa *square metre* moja, mtu akanunua kwa milioni mbili ama milioni tatu kwa kiwanja itakuwa ni *reasonable*; lakini ujisema milioni kumi na ngapi huko itakuwa ni ngumu sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hati miliki. Zile hati miliki ni nzuri sana; kwa mfano kwenye jimbo langu, walipima kwa ajili ya hati miliki, lakini bado wananchi ile hati miliki hawaelewi kama anaweza akakopea mkopo benki, bado haijakaa vizuri. Kama tumetoa hati miliki zile za kimila, mimi nazungumzia zile za kimila, naomba kama mtu ameshapewa basi itambulike benki. Akiweza kukopea maana mwananchi yule inamfaidisha ardhi yake, akafanya maendeleo makubwa, hii itakuwa imemsaidia sana mkulima na yule mwenye ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, migogoro ya ardhi kwa wakulima na wafugaji. Nadhani hili suala siku moja tuseme sasa mwisho hakuna migogoro tena na ili kulimaliza vizuri lazima elimu ipite vizuri. Mkulima akielimishwa na mfugaji akielimishwa watu hawatauana, lakini elimu bado. Kwa mfano, zamani unaweza ukaona mtu analima pia ni

mfugaji lakini walikuwa hawagombani, lakini sasa hivi ardhi ya wakulima na wafugaji imekuwa ni mgogoro mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunaiomba Serikali, nadhani Mheshimiwa Waziri wetu yuko vizuri, wakashauriana vizuri na labda na huyu Waziri wa Ulinzi na wengine wanaohusika katika Wizara nyingine tutakuwa tumefikia mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu ni huo. Naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Anna Lupembe, wajiandae Mheshimiwa Rashid Akbar na Mheshimiwa Saul Amon.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai mpaka leo tuko mahali hapa. Naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi, naomba nimpongeze sana Waziri kwa kazi kubwa ambayo anaifanya pamoja na Naibu wake, wanafanya kazi kubwa sana kusema kweli. Lazima tuwape pongezi kwa sababu wamejitalidi kadiri ya uwezo wao, lakini Mungu ataendelea kuwasimamia kwa sababu kazi mnayofanya ni ngumu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii naye anajitahidi sana. Ni mama, naomba nikupongeze mama yetu, endelea kufanya kazi, Mungu ataendelea kukusimamia na kukupigania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze Rais kwa kuona sasa jukumu la ardhi ni kubwa ameona kwenye manispaa, halmashauri, vile vitengo vyote vitoke viwe vinaripoti kwa Katibu Mkuu moja kwa moja ili kurahisisha kazi iweze kuwa nzuri zaidi. Naomba nimpongeze sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ametufanya

kazi kubwa, sasa tunajua Wizara imekuwa Wizara kamili kwa ajili ya kazi ambayo inatakiwa kufanyika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Mkoa wetu wa Katavi; Katavi ni mkoa na pale Mpanda Mjini ni Manispaa. Tuna Maafisa wachache sana wa Ardhi na Mkoa wa Katavi unakua kwa kasi kubwa sana. Mkoa wetu wa Katavi maeneo mengi hayajapimwa, hususan Mji Mkongwe pale Mpanda Mjini, Kata ya Kashaulili; ule mji umepimwa lakini wananchi wale hawajapata hati mpaka leo. Tunajua hati ni muhimu sana ndani ya maisha yetu ya kifamilia maana hati ndio msingi wa maisha ya kila jamii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Ardhi ndani ya Mkoa wetu wa Katavi kwa sababu sasa hivi imekuwa ni Wizara ya Ardhi, tunaomba watuongzee watumishi, hatuna watumishi kabisa. Ndiyo maana sasa hivi ukiangalia Mpanda migongano ya ardhi imekuwa ni mikubwa sana kutokana na kwamba watumishi hatuna na wananchi wanajenga kiholela. Sasa ukija upimaji inakuwa ni shughuli kwa sababu viwanja vile vinagongana na maeneo mengi yanakuwa kuna migongano ya ardhi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Kata yetu ya Semulwa, Mtaa wa Kichangani, haujapimwa kabisa na ni ndani ya Manispaa ya Mpanda Mjini, haijapimwa kabisa. Naomba Wizara ya Ardhi sasa hivi kwa sababu, imeshakuwa Wizara kamili ndani ya maeneo yetu husika, tunaomba tuletewe Wilaya ya Mpanda wafanyakazi wa kutosha, ili migogoro ya ardhi Mpanda iweze kupungua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Kata ya Mpanda Hoteli na Kata ya llelbo. Wananchi wa Mpanda Hoteli na Kata ya llelbo walikuwa wana mashamba walikuwa wanalima kwa muda mrefu, lakini sasa imekuja kuwa migongano na jeshi; jeshi wanasema ile ardhi ni ya kwao, wananchi wanasema ardhi ile ni ya kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Ardhi, Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri pamoja na Wizara ya Ulinzi, tuje tutatue hili tatizo Mpanda. Ni tatizo kubwa mno kiasi ambacho ni mfarakano kusema kweli, naomba sana msaada wao, waje mtatue tatizo hili. Wananchi wanasema ardhi ni ya kwao na Jeshi wanasema ardhi ni ya kwao. Sasa migongano hii; na ukizingatia ndani ya Wilaya ya Mpanda imekuwa ni Mkoa, tunahitaji nafasi kubwa zaidi. Nashauri Jeshi waweze kutafutiwa sehemu nyingine, yale maeneo wapewe wananchi kwa sababu migongano yao haifurahishi kusema kweli. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Wilaya yetu ya Mpanda tulijengewa nyumba za *National Housing*. Tunaishukuru sana Serikali pamoja na shirika lenyewe, limejenga nyumba nzuri sana lakini hapa kuna tatizo. Hizi nyumba zimejengwa kwa sasa hivi ni takriban miaka kama mitano iliyopita. Hizi nyumba hazina watu na zimekwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hapa kuna tatizo; wamepanga sjui, wamenunua watu takriban kama sita tu katika nyumba mia mbili na kitu. Sasa sielewi: Je, hizi nyumba bei yake ni kubwa au *National Housing* hawana mpango mkakati wa kuweka hizi nyumba ziweze kupangishika kwa bei nafuu, wakawapangisha wananchi? Sasa hapo sielewi, kwa sababu zile nyumba sasa hivi zinaishi nyoka, manyasi yamelundikana pale, hazifanyiwi ukarabati wa aina yoyote. Kwa kawaida ukijenga nyumba, kama haiishi binadamu nyumba ile inakuwa boma. Sasa nyumba hizi zimetumia pesa nyingi sana za Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana hizi nyumba, *National Housing* watafute jinsi ya kufanya; aidha, wapunguze bei wapangishe wafanyakazi ambao wako ndani ya Mkoa wa Katavi, kwa sababu Katavi sasa ni Mkoa. Wawapangishe wafanyakazi wa Mkoa wa Katavi au waende wawakopeshe wafanyakazi wa Serikali ndani ya Manispaa, Halmashauri ili zile nyumba ziweze ku-survive kwa sababu pesa nyingi zimetumika kujenga zile nyumba na ni nyumba nzuri sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali itumie hekima kwa hizi nyumba za *National Housing* zilizojengwa kwenye Wilaya. Wali jenga kwa manufaa ya Watanzania ili kuititia Serikali yao waweze kupata nyumba hizo kwa bei nafuu. Sasa kutokana labda na kuuziwa viwanja vile kwa bei kubwa na wenyewe wanataka kuweka bei kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naomba niunge mkono hoja. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ajali Rashid Akbar, jiandae Mheshimiwa Amon.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia Wizara hii nyeti ya *Comrade Lukovi* kwani Wizara hii ni nyeti na ndiyo Wizara ambayo kwa kweli tunaitegemea kiuchumi. Bila ardhi tunaweza tusiwe na viwanda vyta kiuchumi, tunaweza tusiwe na kilimo, viwanda wala mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ardhi ni muhimu na ndiyo maana inahitaji iwekwe kwa mtu ambaye ni makini tena mtu ambaye kwa kweli awe ni sahihi kweli kweli. Mheshimiwa Waziri wa Ardhi amepewa yeye kwa kuwa ameonekana kwamba ni mtu makini. Ili aendelee kuwa makini, anatakiwa akemee baadhi ya Wizara. Wizara ambazo anapaswa kuzikemea ni pamoja na Maliasili na Utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maliasili na Utalii wakitaka kujikatia eneo, wao wanaamua tu kwenda kujikatia, wanaangalia thamani ya tembo wao, lakini hawaangalia thamani ya binadamu. Naomba wafuate utaratibu kwamba pale anapostahili kuwepo mnyama aendelee kuwepo mnyama na pale ambapo panastahili kuwepo makazi yaendelee kuwepo makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa watu wa Madini wakihitaji eneo lao, wao hawajali kama kuna watu ambao wapo ndani ama kuna mashamba ya watu. Wao wanachoangalia ni thamani ya yale madini yao. Kwa hiyo,

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

tunahitaji watu wa madini wapewe eneo lao na wale watu wanahitaji wabaki katika eneo lao madini, waendelee kubaki katika madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyozungumza mwenzangu ambaye amepita, hii Wizara ya Ulinzi tunahitaji sana ulinzi, lakini tunapohitaji kupanua mipaka, basi wawepo ndani ya mipaka yao ili na wananchi waendelee kutumia maeneo mengine. Kwa hiyo, ni vizuri Wizara ya Ulinzi ikatengewa maeneo yao nje ya maeneo ya binadamu mahali ambapo wananchi hawawezi kuwa na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yale maeneo ambayo yamekuwa katikati sasa hivi, kwa mfano Jeshi ambalo lilo katikati, hatuhitaji tena kuwa na Jeshi katikati ya mji. Nadhani tuangalie uwezekano wa kuchukua Jeshi tuweke nje ya mMji, maana tuna maeneo mengi ili waweze kufanya mazoezi kwa nafasi zaidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo naomba ni kuhusu Wilaya ya Newala. Wilaya ya Newala ilitangazwa mwaka 1959 kwa *GN* ambayo ilitoka mwaka 2000. Tulitegemea kwamba kama Wilaya ilianzishwa mwaka 1959 na *GN* ikatoka mwaka 2000 kuna mpaka ambao unaanzia pale Chiwata, Ndanda, Mpanyani hadi kule Mwena; hiyo mipaka ilianzishwa tangu mwaka 1959 na wale wananchi ambao walikuwa wanabeba *GPS* za Wazungu wapo. Kwa hiyo, tunategemea ile *GN* ambayo ipo, kilomita moja kutoka Ndanda ndipo ambapo Wilaya ya Newala inapoishia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mshangao kuna *GNya* mwaka 2010 ambayo ilitangaza Wilaya ya Masasi. Hii *GNya* mwaka 2010 inatofautiana na *GN* ya mwaka 2000 ambazo zote zinatoka katika Ofisi moja. Inakuwaje hizo *GN* ambazo zinatoka katika ofisi moja zinatofautiana? Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Comrade Lukuvi, aangalie *GN* ya mwaka 2000 inakuwa vipi tofauti na ile *GN* ya mwaka 2010?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii mimi naelewa kuwa kulitokea mgogoro mwaka 1994 juu ya mpaka, kwa hiyo,

watu wakatumia *advantage* ya miaka sita ile baadaye kurekebisha ile *GN* na ndiyo maana hata tafsiri ya mpaka leo wa Masasi na Newala unatofautiana. Wananchi wanajua mipaka yao inaishia wapi na kila mmoja anafahamu, lakini watalaam wanatofautisha. Wale wataalam ambao siyo waadilifu wanafanya mambo ambayo siyo sahihi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi juzi hapa kumetokea mgogoro kati ya watalaam wa Kanda ya Mtwara na wananchi pale Mpanyani. Haiwezakani mtu ambaye amekaa kuanzia mwaka 1918 yupo pale Mpanyani uende na *approach* umwambie bwana wewe upo Masasi, akwambie tu leo Mheshimiwa Lukvi wewe ni mtu wa Mbeya. Kwa kweli namshukuru sana yule Diwani wa Chilangala, alitumia busara. Vinginevyo wale watu leo tungkuwa tunaongea hadithi nyingine. Yale mambo yaliyotokea Dodoma, yangetokea Mtwara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri kwa kutumia busara zake aende akawaite wale wazee ambao walikuwa wamesimama na wanajua ile mipaka, awaite wananchi wa Masasi na Newala ambao wanajua mipaka yao na tumekuwa tukiishi kwa amani, sisi hatuna tofauti, isipokuwa kuna madini yatatusambaratisha, nchi hii itagawanyika katika vipande. Kuna wanasiasa wengine wanataka mashamba pale, wanahonga baadhi ya watalaam ambao siyo waadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kwamba tunapomaliza Bunge hili, yeye mwenyewe *Comrade* aje aangalie hali iliyoko pale. Haiwezekani leo mtu ambaye hakuwa anategemea kwenda Masasi au Newala asubuhi aambiwe kwamba leo wewe upo katika Wilaya ya Newala wakati ile mipaka wao wenyewe wanaifahamu au shamba lako unaambiwa lipo Masasi au halipo Masasi lipo Newala.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. AJALI R. AKBAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, kwani naamini kwamba Mheshimiwa Waziri atakuja baada ya Bunge hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Amon, Mheshimiwa Mbarouk ajiandae. Mheshimiwa Amon, hayupo. Mheshimiwa Mbarouk, naye hayupo.

### **MICHANGO KWA MAANDISHI**

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu kuruhusu Taasisi binafsi katika Upimaji Ardhi. Kutokana na uhaba wa fedha katika Wizara kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara hususan upimaji wa ardhi, naiomba Serikali iruhusu Taasisi binafsi katika kufanya shughuli za upimaji ili kuwafikia wananchi wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watu binafsi wanatoa huduma kwa wananchi wengi lakini changamoto kubwa ni VAT ambayo wanatozwa na hii hupelekea gharama za upimaji kuwa kubwa, naiomba Serikali iondoe VAT kwenye kampuni hizo za upimaji kusudi gharama za upimaji wa ardhi kwa wananchi zipungue.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa gharama za upangaji wa ardhi ni kubwa na wakati huo huo mtu analipia jengo; na kwa kuwa wananchi wanalipia kodi mara tatu, yaani kiwanja, nyumba na vifaa, naiomba Serikali ibakize kodi mbili tu. Yaani kodi ya kiwanja na kodi ya vifaa vya nyumba ambavyo vinakuwa vimelipiwa na mtu akishajenga jengo. Basi alipie jengo tu na siyo kulipia tena kiwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Kanisa la K.K.K.T Njombe Mjini limemilikishwa eneo kubwa hekta 120, katika Kijiji cha Magode na limeachwa bila kuendelezwa na

kusababisha mivutano kati ya Kanisa na wananchi wa Magoda; naiomba Serikali ichukue eneo hilo na kuwagawia wananchi wanaohangaika na wamechukuliwa maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote kwa kugeuza Wizara na kuifanya iwe bora. Nawapongeza kwa kuondoa utapeli wa viwanja, migogoro mbalimbali na kuweka nidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru kwa kuanzisha mradi wa nyumba ambazo zinajengwa na *NHC* kule Chatur - Muheza. Mradi huo umeanza vizuri na Wakandarasi wapo site.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muheza hatuna Baraza la Ardhi na malalamiko na migogoro ya ardhi inaongezeka kila siku. Wananchi wa Muheza inabidi waende Tanga. Tafadhali naomba tuangalie uwezekano wa kuanzisha Baraza la Ardhi hapo Mjini Muheza kwa msaada wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza miradi mbalimbali ambayo inajengwa na shirika letu la *NHC*. Miradi hiyo ni mingi, ila bei za nyumba bado ni kubwa. Pendekezo la kuondoa VAT kwa nyumba wanazouziwa wananchi inabidi liendelee kupendekezwa. Kuondolewa huko kutafanya nyumba hizo zinunuliwe kwa wingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Ofisi ya Ardhi Muheza isaidiwe fedha ikarabatiwe, hususan chumba cha kutunza kumbukumbu/takwimu haiendani na vifaa vilivyoletwa. Mheshimiwa Naibu Waziri ameona. Tafadhali naomba liangaliwe, vinginevyo nawapongeza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na afya njema. Nakushukuru wewe na mimi kwa kupata fursa nichangie ingawa kwa uchache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu ina migogoro mikubwa ya ardhi katika sehemu mbalimbali, kwa kiasi kikubwa migogoro hii inarudisha nyuma maendeleo ya nchi yetu. Tanzania ya viwanda itakuwa ni ndoto kama hatutaweza kupima ardhi na tukatenga maeneo kwa shughuli mbalimbali za kilimo, ufugaji, viwanda na makazi ya binadamu na tukiweza kufikia katika hatua hiyo, kwa kiasi kikubwa tutapunguza migogoro isijo ya lazima na kufikia malengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Ardhi ni muhimu sana katika kufikia malengo makubwa ya kimaendeleo Kitifa. Napendekeza Wizara hii ipewe kipaumbele kwa kutengewa bajeti ya kutosha kukidhi mahitaji ya mipango ya Wizara. Naomba Wizara iendelee kushirikiana na wadau mbalimbali katika kutekeleza mipango yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie kuhusu umiliki wa ardhi. Sheria za Ardhi zinatambua haki sawa, umiliki wa ardhi kati ya mwanamke na mwanaume. Hata hivyo uhalsia ni tofauti, kwani mila na desturi zilizopo nchini, nyingi hazitambui usawa huu hasa katika haki ya kurihi ardhi. Pamoja na wanawake kuwa zaidi ya asilimia 50 ya idadi ya watu wote nchini, pia wanawake wanazalisha kati ya asilimia 60 hadi asilimia 80 ya chakula tunachokula ukanda wa Jangwa la Sahara. Tafiti nyingi zinaonesha wanawake asilimia 20 ndio wamiliki ardhi Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hali hii kwa kiasi kikubwa inachangia wanawake kuwa maskini, kunyanyaswa na kudhalilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, usawa wa umiliki ardhi na urithi wa ardhi upo kisheria kati ya wanawake na wanaume, naomba Wizara isimamie usawa huu kwa ukamilifu hasa vijijini. Wizara ipige vita mila na desturi zenye kukandamiza wanawake katika urithi wa ardhi na umiliki.

**MHE. SILAFU J. MAIFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uhakika Wizara hii inafanya kazi kama mchwa kutokana na hali iliyopo katika suala zima la matumizi bora ya ardhi kwa nchi yetu na kujikuta na migogoro kila upande na inayoendelea kupatiwa ufumbuzi. Utekelezaji huu unatokana na umahiri, weledi wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na baadhi ya watumishi wazalendo wapendao maendeleo ya nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchini mwetu tuna mtihani mkubwa wa matumizi bora ya ardhi na kupanga nchi yetu na kiepusha na migogoro ya wananchi wetu. Hadi mwaka 2016/2017 tuliweza kuwa na wahitimu 559 tumejitahidi na kufikia 787 mwaka 2017/2018 kwa nyongeza ya watahiniwa 228.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Wizara ichukue maamuzi ya makusudi ya kuomba majengo kadhaa *UDOM* na kuendesha mafunzo ya wataalam wa ardhi huku tukiendelea na kuboresha miundombinu ya vyuo vyetu. Upungufu ni mkubwa kwa mahitaji yake, ukiangalia nchi ni kubwa na wananchi wanaongezeka kwa kasi kubwa kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kasi ya upimaji wa ardhi nchini imekuwa ya kusuasua kutokana na wataalam, pia vifaa husika. Pamoja na jitihada za Serikali na Wizara kuanzisha utaratibu wa kufungua ofisi husika kwa ngazi ya kanda, bado vifaa havijafika na wataalam wa kutumia vifaa hivyo bado hawajaandaliwa. Katika maonesho tumekutana na kampuni husika na upimaji ardhi wenye vifaa vya kisasa. Gharama ya ununuzi wa vifaa hivyo ni bei rafiki. Kwa chombo cha shilingi milioni 50 wao wanauza shilingi milioni 16. Je, Serikali haiongi umuhimu wa kudhamini Halmashauri kupata vifaa hivyo kutoka kampuni hiyo waweze kuwa na vifaa vyao na kuongeza kasi ya upimaji wa ardhi yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya fedha ni vema ikaona umuhimu wa kuwasilisha fedha zote zinazopitishwa

kwenye Bajeti ya Wizara ya Ardhi ili nao wafahamu kuwa ni wadau wa kupiga vita migogoro ya ardhi na uimarishaji wa matumizi bora ya ardhi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ni vema ikaona namna ya kutoa maelekezo ya ulipaji wa gharama ya viwanja kwa wananchi wetu wa kawaida. Pamoja na kuchukua kwao viwanja vidogo, bado uwezo wa gharama anayotakiwa kulipa ni mtihani kwao kwa kipindi cha mwezi,

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wana kiu ya maendeleo, naomba tuwape muda watimize ndoto zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wapima Ardhi Binafsi. Nipende kushauri Serikali kutambua kazi kubwa inayofanywa na sekta binafsi ya uendelezaji wa ardhi kwa kupima na kusaidia uendelezaji wa ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Serikali kuwaondolea VAT katika malipo yao au kodi ambayo itafanya kuongeza gharama kwa wananchi wanaohitaji kupimiwa ili kufanya kazi ya kupanga miji yetu na vijiji kufanyika kwa haraka ili kuokoa janga la ujenzi holela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapimaji binafsi wameongeza kasi ya upangaji miji kutokana na Serikali kutokuwa na wafanyakazi wataalam wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgawanyo wa Ardhi. Nishauri Serikali kuhakikisha kuwa inatenga ardhi kutokana na uhitaji mbalimbali. Kwa mfano, ardhi kwa ajili ya wafugaji; ielewewe kwamba kila mkoa, wilaya, kata zinatenga maeneo ya wafugaji na wakulima ili kuondoa migogoro inayopelekea wananchi kuuana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishauri Serikali kuangalia upya juu ya hifadhi za wanyama au maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya misitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali ifuatilie migogoro inayoendelea kati ya wananchi na Hifadhi za Taifa ili kujiridhisha mipaka ya awali badala ya kuwachomea wananchi nyumba zao na kuwanyang'anya mifugo yao au kupiga risasi mifugo ya wananchi, jambo ambalo limezalisha chuki baina ya wananchi na wahifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Gharama za Upangaji Ardhi na Malipo ya Majengo. Niishauri Serikali kuliangalia hili kwani limekuwa kikwazo kikubwa kwa wananchi. Mwananchi analipia ada ya kiwanja kila mwaka halafu analipia kodi ya jengo ambapo pia amelipa kodi wakati wa kununua vifaa vya ujenzi, hivyo mwananchi kuona kuwa na ardhi au kujenga nyumba ni kosa kwani kodi nyingi zinamfuata mwananchi huyu. Naishauri Serikali kuchagua kodi mojawapo ilipwe ili kuwapunguzia misururu ya kodi iliyopo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hati za Kimila Kutotambuliwa Kisheria. Niishauri Serikali kuliangalia hili kwani hati za kimila hazitambuliwi mara mwananchi ahitajipo mkopo benki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maeneo yasiyoendelezwa yarudishwe kwa wananchi au kupangiwa matumizi mengine. Nishauri Serikali maeneo ambayo hayatumiki mfano eneo kubwa la Shirika la Elimu Kibaha ambalo limekuwa pori na kusababisha mauaji na ubakaji mkubwa. Niombe Shirika la Elimu Kibaha kuchunguzwa.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mgogoro wa Mipaka kati ya Monduli na Arusha *DC* katika Kata ya Mfereji. Naomba kauli ya Wizara hii ya Ardhi, ni lini mgogoro huu ambao umekuwa ukigharimu maisha ya watu wetu kwa kuchomewa, mabomu na kujeruhija utatatuliwa?

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgogoro wa Monduli na Babati utatatuliwa lini kama Waziri alivyoahidi mwaka jana?

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hii, hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali imalize migogoro ya ardhi ya muda mrefu inayosababisha wananchi kunyanyasika na kuwa maskini. Migogoro hiyo ni kama ifuatavyo:-

(1) Migogoro kati ya Hifadhi ya Uwanda ya Akiba na Vijiji vya Ilambo, Kilangawana, Maleza, Legeza, Kapenta, Mkusi, Mpande, Kawila na Kipeta.

(2) Mgogoro mwingine ni kati ya Mwekezaji wa Shamba la Malonje na wanachi wa Kata ya Msanda Muungano; tunaomba mgogoro huo ufile mwisho.

(3) Mgogoro wa Gereza la Molo na wananchi wa Kata ya Msanda Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kuandika na kuiwasilisha kwa ufasaha hotuba hii. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, upimaji wa viwanja na mashamba; napenda kuipongeza Wizara kwa hatua yake

ya kuendelea kupima na kuwapatia viwanja vyta makazi wanachi wetu ili kuwaondolea matatizo ya uhaba wa viwanja. Makazi ni hitaji muhimu sana katika maisha ya mwanadamu lakini inaonekana kuwa bado bei ya viwanja si rafiki kwa wananchi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya viwanja ni kubwa sana kiasi ambacho wananchi wanakata tamaa na na hivyo kusababisha wananchi hao kutafuta njia mbadala ya kujikatia maeneo ya makazi kwenye maeneo yaliyo karibu nao, jambo ambalo linapelekeea kuharibu azma na mpango mzuri uliowekwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika jambo hili ni kuiomba Wizara kupunguza bei ya viwanja hasa vyta makazi ili kuwawezesha wananchi kumudu gharama hizi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINABU M. AMIRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya tote ninampongeza Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William V. Lukuvi pamoja na Naibu wake, Mheshimiwa Angelina S. Mabula, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya wananchi hususani katika Mkoa wa Dar es Salaam hununua nyumba maeneo ya makazi ya watu kisha kubadilisha matumizi ya ardhi hiyo kwa kujenga karakana au viwanda vidogo. Naishauri Serikali iwachukulie hatua za kisheria wale wote wanaofanya ubadilishaji wa matumizi ya ardhi bila kuzingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali, ili kupata wataalam wa ardhi wa kutosha Serikali ifanye mpango mkakati wa kudahili wanafunzi wengi katika vyuo vyetu hapa nchini katika fani mbalimbali zihusozo mambo ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itenye maeneo ya ardhi na kuwamilikisha kisheria wafugaji wote nchini na wakulima ili kuondoa migogoro ambayo hutokea mara kwa mara katika sehemu mbalimbali hapa nchini mwetu. Kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili kuweza kujua sheria za ardhi na kupunguza migogoro katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kulipa fidia kwa wakati kwa wale wananchi ambao ardhi zao zimetwaliwa na Serikali kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Walipe fidi hizo ili wananchii waweze kutumia fidia hiyo kuweza kutafuta maeneo mengine ya makazi au mashamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kuharakisha upatikanaji wa hati miliki za ardhi na pia vibali vyta ujenzi kwa haraka maana katika maeneo mengi kuna urasimu wa upatikanaji wa hati miliki na *building permit* huchukua muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kurasimisha pia maeneo yaliyojengwa kiholela (*squatters*) hususani katika Mkoa wa Dar es Salaam; kwa mfano Manzese, Tandale na kadhalika ili wananchi waweze wapate hati ambazo zitawasaidia kuweza kupata mikopo benki na kuboresha nyumba zao, pamoja na shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali itoe fedha zilizotengwa katika bajeti hii ya mwaka 2018/2019 kwa wakati ili kuisaidia Wizara kutekeleza majukumu yake kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, namwomba Mungu awape afya njema na umri mrefu Mheshimiwa William V. Lukuvi, pamoja na Naibu wako Mheshimiwa Angelina S. Mabula ili muweze kuwatumikia Watanzania katika Wizara hii muhimu ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa weledi.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ina mashamba ya mikataba 42 na mengine yamekuwa hayajaendelezwa ipasavyo na kugeuka kuwa mapori ya kuishi wanyama. Mashamba ya Tembo Tembo na ACACIA yaliyo Kijiji cha Mangola juu yameendelezwa kwa chini ya asilimia 40 na yanakosa sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili lilishapelekwa Wizarani na hata wananchi walimsimamisha kwa mabango Waziri Mkuu alipotembelea Karatu. Tunaomba Serikali iwarudishie wananchi wa Mang'ola juu sehemu na mashamba hayo hapo juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmiliki wa shamba la ACACIA amekataa kutoa njia ya wananchi wa Mang'ola Juu kwenda Kijiji cha jirani cha Makhomba. Huu ni ukatili wa hali ya juu na kuwanyima wananchi haki ya kutembeleana; mmiliki huyo haitambui Serikali. Tunaomba Waziri awasakiidie wananchi wa Mangola Juu kupata njia hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Karatu ambayo iligawanyika kutoka Wilaya ya Mbulu ya zamani ina utata wa mpaka kati yake na Wilaya ya Ngorongoro. Kihistoria eneo la msitu wa kutoka *gatela* Ngorongoro hadi *View Point* lilikuwa eneo la Wilaya ya Mbulu. Tunaomba Serikali isaidie kupata ukweli wa mpaka sahihi kati ya Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Ngorongoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mabaraza ya Ardhi ya Kata yanafanya kazi kubwa na muhimu sana ya kusimamia haki. Bahati mbaya Mabaraza haya ya Kata bado yanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Suala la posho zao, nauli pindi wanapokuwa kazini bado ni shida kubwa sana. Tunaomba Serikali iweke mpango wa wajumbe hao kuwa na posho ya uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka kati ya Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Ngorongoro uhakikiwe. Mpaka kati ya Wilaya ya Karatu na Wilaya ya Mbulu eneo la Maseda nao uhakikiwe.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwa kumwomba Waziri aje Wilayani Liwale ili kutatua migogoro kwenye Wilaya ya Liwale. Kuna mgogoro wa muda mrefu katika Kijiji cha Kikulyungu na Hifadhi ya Selous. Pia kuna mgogoro kati ya Kilwa na Liwale migogoro hii miwili imeshindikana kwenye ngazi zote, hivyo kuhitaji ngazi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Kanda ya Mtwara ni sehemu ya tatizo katika Halmashauri ya Liwale, kwani imekuwa ikisababisha migogoro badala ya kutatua migogoro. Mfano, Halmashauri ya Liwale imeingia mgogoro na mwananchi baada ya Halmashauri kupima shamba la mwananchi huyo, shamba ambalo lina Hati Miliki ya miaka 99.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri wamepima viwanja bila ridhaa ya mwenye shamba, Kamishna wa Ardhi anajua mgogoro huu lakini hadi leo hakuna hatua iliyochukuliwa. Pamoja na Halmashauri kuvunja sheria ya kupima kwenye ardhi ya mtu inayomilikiwa kihalali, mwananchi huyu ni Ndugu Hemedi Mewile katika Kijiji cha Mangando Wilayani Liwale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua vigezo vinavyotumika na Shirika la Nyumba la Taifa kujenga nyumba za bei nafuu katika maeneo mbalimbali nchini. Kwani mimi kwenye Halmashauri yangu ya Liwale kuna uhitaji mkubwa sana wa nyumba hizo hasa kwa wakati huu wa mazao ya korosho na ufuta kufanya vizuri. Ni lini Shirika hili litakuja Liwale kujenga nyumba hizi za bei nafuu? Ukizingatia kutokana na shida ya usafiri, hivyo vifaa vya ujenzi ni ghali sana na kufanya wakazi wengi wa Liwale kushindwa kumudu kujenga nyumba bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Msitu wa Nyera-Kipelele umechukua vijiji vingi sana, naomba Serikali kuangalia upya mipaka ya Msitu huu ili wanavijiji wanaozunguka Msitu huu wapate maeneo ya kulima na shughuli nyingine. Mfano, Kijiji cha Kiangara, Kipelele, Naujomba, Miruwi, Mtawatawa na

Kitogoro, vijiji hivi havina misitu kabisa kwa shughuli za ujenzi kwani sehemu zote zinamiliikiwa na Hifadhi ya Msitu wa Nyera-Kipelele.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kijiji cha Lumecha wanaleta tena changamoto ya ardhi yao ya shamba la Likenangena waliyoikabidhi kwa Kampuni ya Tumbaku walioiazima kwa ajili ya kuandaa mbegu za tumbaku. Baada ya kusitisha kuendelea na uzalishaji wa mbegu za tumbaku Kampuni hiyo ya *TLC* ambayo kwa sasa wamehamia Morogoro hawajairudisha ardhi hiyo ya Likenangena kwa wenyewe, yaani Kijiji cha Lumecha, Kata ya Msindo, Wilaya ya Namtumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hao hawana uwezo wa kuwafuatilia Kampuni ya *TLC* huko Morogoro, wanamwomba Mheshimiwa Waziri awasaidie wananchi hao warudishiwe ardhi yao waweze kuitumia kwa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, historia ya shamba hilo ni ndefu na Mheshimiwa Waziri anao uwezo wa kuipata kupitia watalaam wako wa ardhi wa kuanzia Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo, Mkoani Ruvuma hadi hapo Wizarani. Wananchi hao kila wakitoa changamoto yao kwa wataalam wako, wataalam hao wanasiliza lakini hawafanyi chochote cha kuwasaidia wananchi hao wakidhi haja zao. Ardhi hiyo ilitolewa bila malipo yoyote na hivyo dhana ya kuwa ardhi hiyo ni mali ya *TLC* haikubaliki na haipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Isimani mwenye dhamana ya Ardhi, anisaidie wananchi wa Kijiji hicho cha Lumecha wapate haki yao, warudishiwe ardhi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninalo tatizo la pili, katika Jimbo langu ambalo ni Wilaya yote ya Namtumbo tatizo lenyewe limesababishwa na Wizara yako

kutoa Hatimiliki kwa Chuo cha Wanyamapori cha Likuyu-Sekamaganga kwa eneo kubwa lilidochukuliwa na eneo la Kijiji cha Likuyu-Sekamaganga linalotumiwa na wanakijiji hao kwa shughuli za kilimo cha mazao mchanganyiko bila ya kuwahusisha wanakijiji hao wenye ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipaka ya ardhi ya Chuo hicho ilipanuliwa na kuchukua ardhi ya kilimo cha wakazi wa Kijiji cha Likuyu-Sekamaganga bila ya ridhaa yao, matokeo yake baada ya hatimiliki kutolewa na Kamishna wa Ardhi, Uongozi wa Chuo hicho umekuwa ukiwatumia Askari Wanyamapori kuwanyanyasa wakulima wa Kijiji cha Likuyu-Sekamaganga huku wakiwfafukuza katika ardhi yao na kupelekwa mahabusu kwa makosa ya kutungwa. Hatimiliki ya ardhi iliyotolewa katika ardhi yao wanakijiji kwa chuo ndio kinga ya kuwapiga na kuwanyanyasa wanakijiji hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ninakuomba kero hii uichunguze kwa umakini na hatimaye utoe haki kwa kurekebisha mipaka ya eneo lilitolewa hatimiliki kwa chuo kwa kuondoa eneo ambalo siyo sehemu ya chuo bali ni eneo la kilimo kwa wakazi wa Kijiji cha Likuyu-Sekamaganga ndani ya mipaka ya kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisha ili alifanyie kazi Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, Mbunge wa Isimani mwenye dhamana ya ardhi nchi hii.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naenda kuchangia hoja ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la migogoro ya ardhi katika Baraza la Ardhi kuchelewa kusikilizwa kutokana na tatizo la kukosa Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi. Tunduru hatuna Mwenyekiti na Baraza la Ardhi ili kusikiliza kesi za migogoro ya ardhi hivyo tunaomba tupatiwe Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi ili kuondoa kero hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la kuchelewa kupitishwa ramani/michoro ya Mji wa Tunduru kwa muda mrefu jambo ambalo linasababisha ucheleweshaji na wananchi kuendelea na mchakato wa kupata hati. Kwa mfano, Halmashauri ilitoa *offer* ya baadhi ya maeneo ya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru (Nakayaya) tangu 2011 mpaka 2018, bado wananchi wanaambiwa mchoro haujarudi Wizarani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linawakwaza wananchi wanaotaka kuendeleza maeneo yao kwa kutumia hati zao. Kukopa pesa benki tunaomba Wizara iangalie upya namna ya kutoa/kupitisha michoro ya Halmashauri mapema ili maeneo yaliyopimwa yapate hati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya vifaa vyatupima ardhi pamoja na wafanyakazi wenye ujuzi katika kupima ardhi. Kumekuwa na tatizo la wafanyakazi katika Kitengo cha Ardhi jambo ambalo linachelewesha upimaji wa ardhi na utoaji wa hati kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado kuna tatizo la baadhi ya wafanyakazi kuendelea na tabia za kupokea rushwa ili watekeleze majukumu yao ya kila siku. Vilevile Watumishi wa Halmashauri Kitengo cha Ardhi bado wanafanya kazi kwa mazoea bila kufuata maadili ya kazi. Vilevile kuna upungufu mkubwa wa Watumishi katika Kitengo cha Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la fedha. Kitengo cha Ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kinakumbwa kwa kiasi kikubwa na tatizo la fedha ili kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo ambalo linawalazimisha kuwachangisha wananchi wanaotaka huduma ya kupimiwa ardhi na hatimaye kupata hati ili kutekeleza majukumu yao. Hali hii inalazimisha wafanyakazi kutoketekeleza majukumu yao na hatimaye kuingia kwenye mtego wa kuomba rushwa ili huduma itolewe kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Ndassa, ombi maalum.

### **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 47 na 48 sitaki nizisome.

**MWENYEKITI:** Huna haja ya kusoma, wewe endelea tu.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika pitapita yangu mitaani pamoja na maeneo mbalimbali hasa kwenye *Petrol Station*, ukinunua mafuta leo huwezi kupewa risiti zile ambazo tunapewa siku zote. Nimepigwi simu kutoka Mwanza nikaambiwa kwamba hivi sasa *EFDs* zote hazifanyi kazi. Nimeongea pia na Waziri wa Fedha amesema kwamba kwa mujibu wa *TRA*, leo ni wiki ya tatu tangu tarehe 11 mpaka leo. Ukienda kununua kitu huwezi kupewa zile risiti za kielektroniki. Kwa kufanya hivyo, nina uhakika mapato yatapotea mengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungependa kujua sasa kwa sababu sasa wiki ya kwanza ya pili na ya tatu mashine hizi hazifanyi kazi, mapato yatapotea. Serikali inasemaje kuhusu tatizo hili ambalo ni janga la Kitaifa? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana hii ni *sabotage* kwa watu ambao hawatutakii mema nchi hii. Naomba Mwongozo wako. (*Makofii*)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha, halafu Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ajiandae.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa tuna hili tatizo, lilianza tangu tarehe 11 Mei, 2018 na tukalishughulikia ndani ya wiki moja hali ikawa imerejea kawaida lakini limerejea tena. Sasa hivi taasisi yetu ya e-

*Government Agency*pamoja na kitengo chetu cha *ICT*ndani ya Mamlaka ya Mapato tunaendelea kulishughulikia kwa nguvu zetu zote ili kuona hali inarejea katika kawaida yake. Kwa sababu tunafahamu changamoto zillizopo inapokuwa mashine hizi za *EFD* hazifanyi kazi na ndiyo maana tumeweza jitihada zetu zote. Tumekusanya watalaaam wote wa *ICT* wako *stationed* pale Mamlaka ya Mapato tunaendelea kukimbia nalo. Ni matumaini yetu kwamba tatizo hili litaondolewa ndani ya muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu, lakini Mheshimiwa Waziri *Service Provider* wenu muwe na uhakika ana *firewall* ya *up to date*. Bila kuwa na *firewall* kwenye maeneo ya shughuli zenu za *TRA* siku zote utakuta Serikali inahujumiwa na itakuwa inapoteza mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa ambayo tumeipata kuja angalau kujibu hoja za baadhi ya Wajumbe kwa maana ya Wabunge ambao wamechangia. Mpaka sasa waliochangia kwa kuongea ni 15 na waliochangia kwa maandishi ni 13.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia namshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuniamini, baada ya mabadiliko madogo ya Bazara la Mawaziri, basi aliendelea kuniacha katika Wizara hiyo ili niweze kuendelea kushirikiana na Mheshimiwa Lukuvi. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri wangu ambaye siku zote amekuwa akinielekeza na kuniongoza vyema katika kutenda kazi na tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao wametupongeza kwa sababu tunafanya kazi kama *team work* kwa maana ya

Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu pamoja na timu yake kule ndani. Pia kwa upande wa Waheshimiwa Wabunge tunashukuru Kamati ambayo imekuwa ikitusimamia na kutuelekeza vizuri. Napenda kuwashukuru pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama sitashukuru familia yangu ambayo imenivumilia kwa muda wote pamoja na kufanya shughuli za Kitaifa lakini bado wameendelea kuniamini na kunivumilia. Nawashukuru wapiga kura wangu, muda wote tumekuwa nao na pale ambapo sipo nao basi wanaendelea kunivumilia kwa sababu walinipa dhamana na Mheshimiwa Rais akanipa dhamana nyingine ya Kitaifa, lakini wanalitambua hilo na nawashukuru sana na wengine wako hapa leo kushuhudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi zote zillizotolewa, nawashukuru sana Watendaji wetu wote katika Halmashauri, Manispaa, Majiji na Miji ambao wamebadilika sana katika utendaji kiasi kwamba wanafanya Wizara ionekane inafanya kazi vizuri, lakini ni kwa sababu ya uadilifu wao, wamekuwa wakizingatia yale ambayo tunaelekeza. Ni wachache tu ambao bado hawajakaa sawa, nasi tutaendelea kuafuatilia ili tuweze kwenda nao sambamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nachukua fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, kwa namna ambavyo anaendesha Serikali hii ya Awamu ya Tano katika maelekezo na mtazamo chanya wa kwenda kwenye uchumi wa kati, lakini pia tukiwa na kauli mbiu ya Tanzania ya Viwanda. Kwa kweli Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote tumelibeba hili kwa pamoja na tunahakikisha kwamba uchumi wa kati tutakwenda kuufikia na hasa tutakapotumia rasilimali ardhi vizuri kama ambavyo tunatarajiwa na watu waliotupa dhamana hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na michango yote iliyotolewa, katika kujibu hoja hizi tutazijibu chache kulingana na muda lakini nyingine zote tutazijibu kwa maandishi na Waheshimiwa Wabunge wote watapata nakala zao. Kwa

uelewa wangu na nilivyoangalia maeneo mengi ambayo yamezungumziwa, tatizo kubwa liko kwenye uelewa ambapo wananchi wetu wengi hawajaweza kuelewa na ndio maana changamoto zinakuwa nyini. Hawajajua haki zao na hawajajua wafuate utaratibu gani pale ambapo wanatakiwa kudai haki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile uhaba wa vitendea kazi umezungumzwa. Haya yote yanachangia katika suala zima la kupunguza ufanisi katika maeneo yetu. Upungufu wa watumishi vile vile ni changamoto. Kwa hiyo, unapokuwa na mapengo kama hayo, lazima utendaji pia utakwenda kwa kusuasua kidogo kwa sababu ya uwezo mdogo katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto kubwa ambazo zimetajwa na Wabunge na ambazo pia Kamati wamezungumzia, nitazijilu kama ifuatavyo kulingana na muda. Kamati yetu inayosimamia Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii, wamezungumzia suala la pesa kutopelekwa katika Halmashauri zetu. Hili huchangia pia katika utendaji mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili tumelichukua na tunasema tutahakikisha kiasi kilichokwuwa kimetengwa na wenzetu wa fedha hapa wanaskia, kitakwenda ili kurahisisha kazi za utendaji. Kwa sababu kama tuliwekea bajeti na pesa inakusanya, basi kadri inavyoingia, ndivyo jinsi tunavyowapelekea ili waweze kufanya kazi zao. Kwa sababu wasipokuwa na rasilimali fedha hapo hapo na upungufu wa rasilimali watu lazima utendaji kidogo utayumba. Kwa hiyo, hili tumelichukua na tunatii maelekezo ya Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamezungumziwa masuala mazima ya Shirika la Nyumba. Shirika la Nyumba limezungumziwa pia hata na wachangiaji waliochangia kwa kuongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Shirika la Nyumba kama ambavyo sura ilikuwa inaonekana, sivyo ambavyo uhalisia wake ulivyo. Kamati inayosimamia imeshuhudia na

imelizungumza pia katika taarifa zake. Napenda niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba Shirika letu la nyumba pamoja na kelele zilizoko nje, lakini bado lina uwezo wa kufanya kazi zake vizuri. Ukiangalia zile mali walizonazo, thamani yake inazidi shilingi triliioni 2.8 kwa maana ya thamani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni yaliyokuwa yanazungumziwa, shilingi bilioni 249, ukichukua thamani ya rasilimali ya majengo waliyonayo *National Housing* ukagawia kufanya hesabu ndogo tu, unakuta linaweza kuendesha au kulipa madeni yale mara ishirini zaidi kwa maana ya kwamba lina mtaji mkubwa hasa ukiangalia thamani ya majengo ukilinganisha na madeni ambayo wako nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunapenda kuwahakikishia kwamba sura inayozungumzwa nje ni tofauti na uhalisia. Wajumbe wa Kamati wamefika na wameona. Kwa hiyo, napenda kuwahakikishia, changamoto nyingine zilizoko ndani, kwa mfano mmezungumzia suala la Menejimenti pengine, suala la bodi kutokuwepo, haya yote yanafanyiwa kazi na sasa hivi Wizara iko katika mchakato wa kuweza kuona kwamba ni jinsi gani tunaweza kupata bodi nyingine mpya baada ya Mheshimiwa Rais kuivunja ile nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua bila kuwa na bodi, kazi haziwezi kwenda vizuri. Kwa hiyo, hili kama Wizara linashughulikiwa kwa haraka na tutakwenda kupata taarifa siku siyo nyingi pale ambapo masuala ya *vetting* yatakuwa yamekamilika. Tukumbuke hili shirika ndiyo limebeba dhamana ya Wizara, ndiyo hasa ambalo tunatarajia liweze kumkomboa Mtanzania wa kawaida ukiacha haya mashirika mengine ambayo nayo yanafanya suala la uendelezaji miliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tunahitaji Watanzania wawe na makazi bora na makazi ambayo yamepangika. Kwa hiyo, hili tumelibeba na tunalifanya kazi kama ambavyo inatakitana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Lupembe amezungumzia suala la nyumba kuwepo na kwamba hazipati wanunuzi. Naomba niseme tu kwamba, katika suala zima la ujenzi wa nyumba, kuna Halmashauri ziliomba ikiwemo ile ya Mpanda kule Katavi, lakini kuna nyingine walijengewa baada ya *National Housing* kuweza kupata maeneo kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa zile Halmashauri ambazo ziliomba, basi zitekeleze malengo yake, kwa sababu, tumeshatoka kwenye kulazimisha kwamba watu lazima wanunue, suala la msingi sasa hivi, *National Housing* wana *product* tatu kwa maana ya kwamba unaweza ukawa mpangaji mnunuzi; unalipa kidogo kidogo baadaye nyumba inakuwa yako. Unaweza ukainunua moja kwa moja wewe mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, haya yote yanawezekana, lakini kikubwa tunachotakiwa, pale ambapo Halmashauri inahitaji, tunaomba sana mikataba iwe kamili na muweze kumaliza gharama hizo na kuweza kuchukua zile nyumba. Nawapongeza wenzetu wa Uyui, ndiyo Halmashauri pekee inayoongoza kwa kununua nyumba nyingi ukilinganisha na Halmashauri nyingine, ikifuatiwa na wenzetu wa Busekelo, Mvomero, Geita na Halmashauri nyingine ambazo zimeweza kuchukua nyumba hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limezungumziwa suala la manunuzi kwamba pengine utaratibu siyo mzuri. Naomba niwaambie, suala zima la manunuzi katika Shirika la Nyumba, linazingatia sheria zilizowekwa katika kumpata mnunuzi. Tuzingatie kwamba Shirika hili pia mbali na kuwa Shirika, lakini bado lina Taasisi mle ndani ambazo zimeandikishwa kisheria na zinatambulika. Zinapoingia kwenye mchakato wa kutaka kujenga, basi na wao wanatathiminiwa kama wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, suala la kupata Wakandarasi linazingatia sheria na hakuna mahali ambapo panakiukwa. Kwa hiyo, hili tunalizingatia, tunalifuata na tunaheshimu ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezungumzia suala la ukusanyaji wa mapato kuonekana kwamba pengine linasuasua na mapato hayapatikani. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa sababu katika suala zima la ukusanyaji wa kodi ya pango la ardhi, aliweza kutoa fursa kwa wananchi ambao walikuwa wamelalamikia kwamba pengine wanapokwenda pamoja na tatizo la *EFD Machines* na mitandao katika Halmashauri zetu, walikuwa wanapanga foleni kubwa sana, wanashindwa kulipa kwa wakati. Akatoa miezi minne, lakini bado akaongeza mwezi huu wa Tano ambao unaokwenda kwisha kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba muda ulioongezwa unatosha sana kwa wenzetu kuweza kutimiza wajibu wao kulipa kodi. Nami niseme kwamba baada ya kesho tunaomba sana Halmashauri zichangamkie fursa hii ya kuhakikisha kwamba inawabana wale wote ambao hawajaweza kuzingatia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto chache zinazoletwa na Wajumbe na Waheshimiwa Wabunge kwa kulalamika kwamba pengine gharama ni kubwa. Nadhani gharama siyo kubwa kiasi kile ambacho wanafikiria, lakini unapoona una changamoto kwenye *invoice* yako, tujue tatizo ni nini? Kwa sababu, suala la ardhi liko *fixed*, halipunguzwi wala halifanywi chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachoweza kuangalia, ni lini wewe ultakiwa kulipa na umelipa wakati gani? Kwa hiyo, *interest* inapigwa kila mwezi asilimia moja kulingana na wewe ulivyochelewa kulipa. Kwa hiyo, lazima tulione hili kwamba pia tunao wajibu wa kuzingatia muda wa kisheria ambao unatutaka kuweza kulipa madeni ambayo tunakuwa nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala zima la Mabaraza ya Ardhi ambayo yamezungumzwa. Nasema Mabaraza ya Ardhi mpaka sasa tunayo 97, lakini yanayofanya kazi ni 53, kwa maana ya kwamba yapo na Watendaji. Mpaka sasa hivi tuna kibali cha kupata Wenyeviti wa

Mabaraza 20 na tuna imani wakija hao wataweze kutupunguzia ile adha iliyokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo tulilonalo, kila Mheshimiwa Mbunge akinyanyuka, akiongelea Baraza, kama haliko kwake, kama wana-share labda Wilaya mbili, anataka liende kwake. Naomba tutambue kwamba Baraza linakuwepo pale kulingana pia na idadi ya mashauri au kero zilizopo pale. Kwa sababu hata ukikuta kwamba Mwenyekiti anahudumia Mabaraza matatu au manne, kuna Baraza lingine unaweza kukuta kwa mwaka wana mashauri yasiyofika 200, lakini Mabaraza mengine unakuta kuna mashauri yanakwenda mpaka 1,000 na kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukikuta kwamba Mwenyekiti anakuja mara moja moja ni kutokana na wingi wa mashauri yallyoko katika maeneo mengine ukililinganisha na ya kwako. Kwa hiyo, tunaomba tu tuvumiliane katika hili. Pia Wizara imetenga shilingi milioni 165 kwa ajili ya kufanya ukarabati katika maeneo mengine ambayo tunatarajia kuwa na Mabaraza. Kwa hiyo, nawaomba tu mvute subira kwa sababu tayari kama Wizara tumeshajipanga kuweza kuona ni jinsi gani tutaondoa hii adha ambayo imekuwepo katika suala zima la kuweza *ku-solve* matatizo ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie mipaka ambayo imezungumzwa katika suala zima la kulinda mipaka yetu. Wamezungumzia suala la usalama, hakuna ile njia ya kupita pengine kuweza kujua ni jinsi gani ambavyo unaweza ukalinda usalama wa mipaka yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kusema, kama tulivyojibu swalmoja wakati limeulizwa hapa Bungeni, katika mkuutano huu, tayari Wizara kwenye mradi pesa za maendeleo tulizokuwa tumeomba kwa mwaka huu wa fedha unaoisha, mlituidhinishia shilingi bilioni nne na tulizipata zote na kazi hiyo imeshaanza. Wanasaafisha masuala ya mkuza ili ukae vizuri, kuweza kujua, mipaka ya nchi na nchi, lakini pia makubaliano ya kiasi gani kiachwe kutoka kwenye eneo la *Nomad's land* kwenda kwenye eneo lingine, tayari

wenzetu wa Uganda tulishaingia nao katika ile *protocol* kwamba ni mita 30. Zoezi la Kenya lilikuwa linaendelea. Upande ule wa Tunduma na Zambia kule tayari yalishazungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa ambalo nataka kuwaambia ni kwamba, tunachohitaji kama Watanzania ni kuzingatia yale ambayo tumekubaliana kama nchi na nchi. Kwa upande wa Kenya na Tanzania bado kuna mazungumzo yanaendelea. Sasa suala la barabara ambayo itafanya kuwe na *movement* nzuri ya kuweza kukagua ule mpaka, hili linafanyiwa kazi. Tujue kwamba sekta ya barabara ni Wizara nyingine inayohusika lakini kwa sababu tunafanya kazi kama Serikali, tunalichukua na tunaenda kulifanyia kazi na tayari wenzetu ambao tulikwenda kukagua mipaka, tuliwaomba pia Halmashauri kwa sababu zile ni barabara za Halmashauri. Basi ihakikishwe angalau kunakuwa na upenyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inakosekana heshima ya nchi pale unapokwenda eneo, halafu ili uangalie mpaka wako lazima uingie nchi nyingine; na kama unapeperusha bendera, maana yake uishushe halafu uingie, ukitoka tena kule upandishe, inasumbua. Hilo tumeliona, tumepokea maoni ya Kamati linafanyiwa kazi na tunawaahidi litakwenda kufanyiwa kazi vizuri. Nawaomba tu wenzetu wa Halmashauri wajue yale pia ni maeneo ya usalama wao. Kwa hiyo, wanapochonga barabara zao, wazipe kipaumbele barabara za mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima limeongolewa la ukamilishaji wa maandalizi ya Sera ya Nyumba ya Taifa. Sera hiyo imefikia katika hatua nzuri. Sasa hivi tuko kwenye kukusanya maoni ya wadau. Pale ambapo tutakuwa tumeshakusanya wadau kuona wanaiboreshaje ile sera, italetwa hapa mtawezwa kuiona, tutaendelea katika utaratibu wake wa kuandaa. Kwa sababu itapelekwa Wizarani kwa ajili ya ukamilishaji ili tuweze kujua, kwa sababu huwezi kutunga sera ambayo haihusishi wadau. Kwa hiyo, kama Wizara mnakuwa na *draft* ambayo mnaona kwamba sera itapendeza kama ikiingiza vitu fulani. Ili iboreshwe vizuri,

ni lazima maoni ya wadau yaheshimike. Kwa hiyo, Sera ya Taifa ya Nyumba imeshafikia hatua ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali na lengo ilkiwa ni kuiboresha. Itakapokuwa tayari, taarifa zitaletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala limezungumzwa kuhusu tozo ya mwanzo kwa ajili ya kupata kiwanja (*premium*). Kweli watu wamepongeza na kusema ilitoka 15 ikaenda 7.5, ikaenda 2.5 na Kamati sasa imependekeza ishuke. Naomba kusema tu kwamba kama Wizara tulishalionia hilo na kadri unavyozidi kuwapa nafuu wananchi ndivyo jinsi kazi inavyozidi kuongezeka. Hata kazi ya urasimishaji iliyofanyika Mwanza mpaka kuongeza lengo, walipewa viwanja 35,000, lakini mpaka sasa wamevuka lengo wana 42,563 ni baada ya kupunguza kutoka 7.5 kwenda 2.5 ambapo Mheshimiwa Waziri ambaye ndio ana mamlaka hiyo aliweza kupunguza na kasi ikaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumeipokea, kweli tumeona matokeo chanya pale ambapo unampa nafuu mlaji wa kawaida. Kwa hiyo, hili tumelichukua kama Wizara, tutaona namna bora ya kuweza kuhakikisha tunawapunguzia gharama wananchi wetu ili wengi waweze kumiliki maeneo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe rai tu katika Halmashauri zetu, pale ambapo mnafanya zoezi la urasimishaji, zoezi hili siyo endelevu kama tunavyofikiri. Kwa ile miji ambayo imeshapanga mipango yake kabambe, pale ambapo mpango kabambe unaanza kutumika, *unless* uwe ulilingiza wakati unapanga mpango wako kabambe, ukasema kutakuwa na sehemu kinaendelea na urasimishaji kama wenzetu wa Singida walivyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haikuwa katika mpango huo, tunapoanza kutekeleza mpango kabambe maana yake zoezi la urasimishaji linakuwa halipo. Kwa hiyo, nitoe rai kwa Halmashauri zote ambazo zina zoezi la urasimishaji na wakati huo huo bado kuna zoezi la *master plan* ambazo amekuwa anaziandaa, lazima kasi iongezeke

na wananchi waelimishwe watambue kwamba unapokuwa unatekeleza mpango kabambe huwezi kuendelea kurasimisha kule ndani, utakuwa unagonganisha mambo ambayo siyo sahihi. Vinginevyo, vikiingiliana ina maana utakapokuja kupimiwa ni lazima uende sambamba na mpango kabambe ambao umeandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai tu kwa Halmashauri zetu kuwaelewesha wananchi wetu waweze kujua. Maeneo yale lazima tuwaelimishe wananchi wetu waweze kupata namna bora ya kuwa uhakika wa milki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limeongelewa suala la migogoro katika vijiji vinavyopakana na hifadhi. Maeneo mengi yenye migogoro ya hifadhi, tunashukuru kwamba sasa kuna mradi ambao Idara yetu yetu ya Mpango wa Matumizi ya Ardhi inapofanya kazi pamoja na Wizara ya Maliasili na Utalii kwa maana ya TANAPA wanakwenda kupima vijiji 392. Vijiji vyote vinavyozunguka maeneo hayo katika hizi mbuga ambazo ziko kama nane ambazo zinakwenda kufanyiwa kazi hiyo, jumla yake viko vijiji 427, lakini huu mpango ni wa kama miaka mitatu. Kwa hiyo, tunakwenda kupima maeneo hayo, yanapangiwa mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina imani wakishafanya ile, hapatakuwa na kelele tena kwa sababu wananchi wenyewe wanashirikishwa. Hatua iliyoko sasa hivi ni kuelimisha wananchi namna ambavyo mpango huu utakwenda. Wameanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya na baadaye watashuka kwenye vijiji vyenyewe ili viweze kushiriki. Hati zinazotolewa kule zinatambulika na mabenki. Tunayo mabenki zaidi ya 13 mpaka sasa yanatoa pesa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama mmesikiliza hotuba ya Mheshimiwa Waziri kipindi hiki, tayari zaidi ya shilingi bilioni moja zimetoka kwa kutumia hati miliki za kimila. Kwa mwaka wa fedha uliokwisha wa 2016/2017, mabenki yalishatoa pesa zaidi ya Sh.59,164,000,000/=. Kwa maana hiyo ni kwamba hati hizi zinatambulika na siyo kwamba hazitambuliki kama ambavyo wengine wanafikiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nililiruka suala la Mheshimiwa Mtuka, ambapo aliongelea kuhusu mpango kabambe. Naomba kusema, maandalizi yoyote au mamlaka ya upangaji miji ni Halmashauri zenyewe husika. Kwa hiyo, Halmashari yoyote ikishaona kwamba sasa inahitaji kupanga mji wake vizuri, kuwa na mpango kabambe wa miaka 15, 20, wanatakiwa wao kuanza kuja na hoja yao, halafu Wizara itawasaidia pale watakapoona kwamba pengine wamekwama wanahitaji utalaam. Kwa hiyo, mchakato lazima uanzie kwenye Halmashauri husika kwa sababu ndizo zenyeye mamlaka ya kupanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba tu kuitia hoja ya Mheshimiwa Mtuka, maeneo ambayo pengine walitajarajia kuwa na mpango kabambe wanafikiri ni Wizara inayoanzisha, mnatakiwa wenyewe muanze, Wizara tunakuja kusaidia pale ambapo pengine mtahitaji utaalam, kwa sababu lazima pia Wizara ipitishe, utafika kwenye Wizara, utashauriwa pale panapohitaji kushauriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza miji ambayo tayari mipango yake kabambe imeshazinduliwa na inafanya kazi. Miji ya Musoma, Singida, Mtwara ambao wote wameshamaliza na kazi inaendelea. Mwanza na Arusha nayo iko katika utaratibu, wenzetu wa Dar es Salaam nao bado, mchakato nadhani haujaka vizuri sana lakini, wako hatua hiyo. Tukishakuwa na hilo itatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *ILMIS* ambalo mjumbe amepongeza, niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri wakati anawasilisha hotuba yake, ameongelea faida ya kuutumia mfumo huu na namna gani ambavyo tunaweza pia tukadhibiti wale watumishi ambao hawakuwa waadilifu sana, tukadhibiti masuala ya kuchakachua nyaraka kwa kumwagia chai, majani ya chai na nini. Ukishakuwa katika mfumo huu huwezi *ku-temper* nao hata mara moja. Kwa sababu kazi atakayeifanya mtu Wilayani, moja kwa moja Wizara inaona. Kwa hiyo, mpango huu umeanzia Kinondoni lakini utakwenda utasambaa kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika hili tuelewe tu kwamba mfumo huu wa utunzaji wa kumbukumbu umeanza kwa majaribio, lakini utakwenda katika maeneo yote ili kuweza kuona ni jinsi gani ambavyo tunaweza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la upungufu wa Watumishi katika maeneo yetu na vitendea kazi; naomba nimshukuru tena Mheshimiwa Rais kwa namna ambavyo amewarudisha Watendaji wa Halmashauri katika Wizara. Naomba niseme, kama Wizara tutakwenda kulisimamia hili, tutapitia watumishi wote wa sekta hii walioko kwa nchi nzima na kuweza kuwapanga katika utaratibu ambao *uta-balance* ili angalau kila Halmashauri iweze kuwa na uhakika wa kuwa na watumishi. Kwa sababu ni kweli kuna maeneo hawana Watumishi, kuna maeneo mengine hawana Watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili tutaangalia kwa upya tukishapata ikama yao wako kiasi gani na mahitaji ya kila Halmashauri *then* tuanze kuwapanga kwa uchache wao wakati huo tunaangalia namna bora ya kuweza kuongeza idadi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la vifaa vyaa upimaji kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ameongea kwenye hotuba vitakuwepo *by July*. Nawapongeza sana, pamoja na kwamba na-*declare interest* kwamba mimi natoka Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela, Ilemela wameweza kununua vifaa vyao wenyewe na vinawasaidia katika kasi ya upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tu Halmashauri nyiningine, unapokuwa na vifaa vyako, unaepuka pia zile gherama ambazo zinakwenda kufanya gherama ya upimaji iwe kubwa. Kwa hiyo, pamoja na juhudzi zinazofanywa na Wizara, pamoja na kuimarisha kanda zetu lakini bado pia kama Halmashauri tunahitaji kuona kipaumbele cha upimaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia katika malipo, naomba sana na tumekuwa tukilizungumzia hili kwamba hatutakiwi kuwapunja wananchi; na mwananchi yoyote hataruhusiwa kutoa ardhi yake bila fidia, *unless* kuna suala ambalo ni la Kitaifa sana na halina mjadala katika suala hilo, bado kama Serikali tutazungumza nao na kuweza kuonesha umuhimu wa ule mradi ili aweze kuridhia. Ila hakuna kuchukua ardhi ya mtu bila kulipa fidia yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushuru sana kwa kunipa fursa ya kujibu machache. Kama nilivyo sema, mengine tutajibu kwa maandishi, nimalizie tu kwa kuwashukuru wote na kuwatachia kila lililo jema katika Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani, lakini pia tuombe ushirikiano wenu ambapo sifa zote mnazotupa hatuwezi kuzipata kama hatuna ushirikiano na ninyi. Nasi tunaahidi kuendelea kuwatumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.  
*(Makof)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii uliyonipa mara ya pili baada ya ile kusoma. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote kwa kutupa moyo mimi na Naibu wangu na Watendaji wetu. Nataka kuwahakikishieni kwamba hatutawaangusha. Leo mmetuchaji zaidi, tutaongeza *speed*. Nataka mhakikishe kwamba mwakani mkija kuzungumza wote ambao mmeandika na kusema, mje mtoe ushuhuda kwamba tumefika kwenu na tumezungumza haya mliyotutuma tukiwa kwenye Majimbo yenu. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na hoja yako, ulipokuwa unachangia hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye maswali yako wiki mbili zilizopita, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi kwamba ile *issue* ya Chama cha Wapangaji na *National Housing* wakutane, Mheshimiwa Waziri Mkuu ni

Kiongozi wetu, nawe ni Mwenyekiti wetu. Nataka kuku hakikishia kwamba *National Housing* wata kutana na viongozi wa Chama cha Wapangaji. Jana nimekutana na Mwenyekiti yuko hapo nje. Naagiza wakutane kabla ya tarehe 15 Mwezi wa Sita, halafu waniambie wamekubaliana nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, yale maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu yata tekeleza, Mwenyekiti wa Chama cha Wafanyakazi yuko juu hapa ananisikia na Kaimu Mkurugenzi wa *National Housing* yuko hapa. Naagiza wakutane kabla ya tarehe 15 Mwezi Juni baada ya hapo, wanione mimi kama Waziri njue nini naweza kuamua. Kama liko ndani ya uwezo wangu au la kupeleka kwenye Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa pendekezo hilo na namshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maagizo na namhakikishia kwamba nitatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumza wengi, nianze na rafiki yangu hapa Mheshimiwa Bobali. Amri yangu nilioitoa ni kwa mujibu wa Sheria ya Mchinga. Lile eneo nataka wasikie wote, ni eneo la Serikali. Zile ekari zote zilizochukuliwa na kampuni ile iliyochukua kuzunguka Bahari ya Hindi, lote ni eneo la Serikali. Walichukua kinyume cha sheria na nilikwenda na viongozi wote, walitoa hati kinyume cha sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna mazungumzo na migongano inafanyika huko, haiwezekani. Nimeshatoa amri na amri siyo yangu ni ya kisheria. Kwa hiyo wajue tu hili eneo ni la Serikali. Halmashauri ya Wilaya ya Lindi wajue hili ni eneo la Serikali na lazima walipange kwa mujibu wa sheria. Nilitangaza siku ile walipandishe hadhi kwa sababu walianza kutoa hati kabla, eneo lenyewe likiwa kwenye hadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hili hatubabaishani ndani ya Serikali. Mimi ndio nimepewa jukumu hili na Mheshimiwa Rais, namsaidia kufanya jambo hili. Zile Zahanati zitafunguliwa, vinginevyo anayetaka azibomoe akazijenge huko alikotaka. Zile Zahanati zimejengwa kwenye ardhi yenu.

Kwanza nashangaa, mnasubiri nyie kufunguliwa na nani? Nani awafungulie? Ziko kwenu, nani anawafungulia? Kufuli gani hiso zimewekwa? Mwambieni azichimbe azitoe. Nani alimpa kibali cha kujenga? Hakuna makubaliano? Kwa hiyo, nasema, hilo la Zahanati siyo langu, lakini ardhi ile haitoki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewasikiliza vizuri Mheshimiwa Bobali na *issue* zenu za mipaka, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Maftaha, ninyi mnatoka Mkoa wa Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nimepanga, sasa mmenipa nguvu. Nitatembelea Mkoa wa Mtwara na Lindi. Nitarudi tena pale Mjini Mtwara ili nione yule tapeli kama anaendelea kunyaanya, maana sehemu nyingi nimemkaba. Huyo huyo ndiye amehusika na huko Lindi, huyo huyo ndio Mtwara. Anatafuta watu wa Dar es Salaam wanakwenda kuchukua ardhi Mtwara kana kwamba Mtwara hawapo. Nitakuja Mtwara, Lindi na Newala kwa rafiki yangu Rashid. Kule nako ule mpaka kati ya Masasi na Newala tutakuja kuzungumza huko kwenye *site*, tutaelewana. Ni kweli baadhi ya Watendaji wa Ardhi kwa siku za nyuma walikuwa sio waaminifu. Tunapowatuma kwenda kurekebisha mipaka, wanarekebisha mipaka kutokana na eneo; wale wajanja wanaowapa fungu, basi mpaka unahamia huko. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumejifunza juzi kwenye mpaka wa Kilindi na Kiteto; zaidi ya kilomita 15,000 ziliikuwa zimehama. *GN* inaeleza watu waende Kaskazini Mashariki wenye wanakwenda Magharibi bila sababu. Sasa kutokana na nidhamu iliyowekwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, hakuna mtumishi anaweza kula hela tena. Kwa hiyo, sasa hivi mjue kila palipoandikwa *GN*, tutarekebisha kwa mujibu wa maandishi ya *GN unless* wananchi wakubaliane upya. Maana inawezekana *GN* na yenye we imepitwa na wakati, lakini mkikubaliana, sisi tunakuja kuiandika tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba sasa hivi utumishi wa Umma umebadilika, watu wana nidhamu, tutakuja kurekebisha hiyo mipaka ya Masasi na Newala na maeneo yote ambayo yana migogoro mipaka tutapitia na mingine tumeshaiandika, kama ile ya Makambako, Njombe na Mufindi, rafiki yangu Mheshimiwa Kigola amesema na mingine tulivoandika tutakuja kuishughulikia ili angalau watu wakae vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI naye ametoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa wahakikishe kwamba mipaka ya vijiji na vijiji migogoro yao wanaimaliza kwa sababu iko ndani ya uwezo wao. Alishaandika siku nyingi na nadhani hili wanomitekeleza. Maana haiwezi kuwa wanesubiri Mawaziri waende huko kushughulikia mipaka ya vijiji na vijiji wakati *GN* wanazo na mipaka hili illbuniwa na Wilaya zao. Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa wasimamie ukamilishaji wa utatuzi wa migogoro ya vijiji na vijiji kwa sababu iko ndani ya uwezo wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimeyasikia ya Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Maftaha. Lile la Mheshimiwa Maftaha la mjini kuhusu mgogoro wa fidia, kwa sababu wananchi waliingia mkataba na *UTT*; na *UTT* ni chombo cha biashara, kiko chini ya Wizara ya Fedha, hata mimi niliwashangaa. Kwa sababu waliosema watalipa mwaka 2017 ni wao, nami nilikuja Mtwara na nyie tulikutana na wewe ulikuwepo. Baadaye wamesema hailipi, wameenda kwa mwenye Wizara yake, Wizara ya Fedha wakamwambia, Mzee huu mradi haulipi, Bodi ya *UTT* wamekataa kuchukua ile ardhi kwa sababu ule mradi wakipima viwanja watauzza ghali na wananchi wa Mtwara hawataweza, hailipiki. Kwa hiyo, wameacha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi Wizara ya Ardhi hapa nilikuwa upande wa wananchi, lakini yamenishinda kwa sababu wenyewe mradi ambao mlifikubaliana nao wamesema hailipi. Ardhi haijachukuliwa, imerudi mikononi, kwa hiyo, tushirikiane tuipange wenywewe, tupime viwanja ili kila mtu

apate faida ya ardhi yake. Hatuwezi kuwang'ang'ania wale kwa sababu ilikuwa ni biashara. Nilitaka niseme hivyo, lakini nitakusaidia kuwaeleza zaidi nitakapokuja Mtwara. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mtuka amezungumzia habari ya *master plan* kule Manyoni, yeze ni mtalaam, anajua kabisa kwamba masuala ya *master plan* yanaanza kwao. Waazimie wao kutengeneza *master plan* halafu tutashirikiana. Waazimie kwenye *Council* kwamba wanataka kutengeneza *master plan* na kupanga mji wao, tunajua wana matatizo ya vifaa, vitakavyokuja tutawaelezeni, wataviazima hivi vifaa kila Halmashauri ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia mwezi wa Saba tutakuwa na vifaa nchi nzima, mtaviazima kila Halmashauri bure. Kabla ya mwezi wa Saba wataalam wa Serikali wa Halmashauri tulionao tutawafundisha sisi Wizara namna ya kutumia hivyo vifaa vyakisasa kupanga. Kwa hiyo, yeze kwa sababu anajua kupanga, yeze ni *surveyor*, hivi vifaa atavitafula, tutampa avitumie ili angalau vimsaidie katika kuharakisha. Tunajua jitihada zake, anafanya kazi vizuri pale, lakini tutashirikiana naye kuhakikisha anakwenda kwa kasi nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alivyosema Mheshimiwa Mwakasaka ni kweli Tabora kuna migogoro mingi, wajanja walishaiharibu pale siku nyngi. Nimekuja mara mbili, amekuja Naibu wangu lakini tutakuja tena. Tunajua siyo tatizo la Tabora, viongozi wengi wameshiriki katika kuharibu mipango miji na kudhulumu watu. Siyo Tabora, sehemu nyngi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya viongozi, hata sisi wa kisasa na Madiwani wakati mwingine huwa tunagombea kwa ajili ya viwanja. Kwa hiyo, kila mji umekwisha, umeshapangwa lakini umeingia kwenye madaraka, lazima upate viwanja. Sasa Watendaji wale walikuwa wanawaajiri ninyi, kwa hiyo, wakiwatisha kidogo wanabadilisha, wanawauzia. Sasa hawatawatisha tena. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameondoa hicho kichaka, wamekuja kwangu, maana walikuwa wanawatisha kwamba watawafukuza wasipotekeleza matakwa yao. Mheshimiwa Rais amewahamisha huko, amewaleta kwangu. Kwa hiyo, nataka niwaonye watumishi wote wa Serikali, sasa hakuna kwa kujificha, kitendawili kimeteguliwa, lazima watekeleze majukumu yao kwa mujibu wa sheria na hakuna vitisho. Mtu ye yote sasa atakayekosea huko hatajificha kwamba nililazimishwa na Kamati ya Mipango Miji, ni lwake, atakakufa na lwake na hahamishwi mtu, atafia hapo hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwakasaka kwamba kwa *issue* ya Tabora lazima tuje twende tena. Kuna mambo ambayo yamekaa vibaya pale. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, alichozungumzia Mheshimiwa Mabula ni kweli, katika zoezi la urasimishaji Tanzania watu wanaongoza wamefanya vizuri, kwa nidhamu na kwa heshima na kujitolea ni Wilaya ya Nyamagana na Illemela. Amesema kweli kabisa. Kwa hiyo, nami nawapongeza sana. Mheshimiwa Mabula anajua watu wake aliowaleta wiki iliyopita, tumekubaliana tukutane mwezi wa Sita katikati kule Jimboni. Kwa hiyo, namshukuru sana na yeye ametoa ushirikiano sana kule Nyamagana katika zoezi hili. Nyamagana na Illemela peke yake wameshatoa Hati zaidi ya 25,000. Namshukuru sana na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ametoa ushirikiano mkubwa katika zoezi hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba wananchi na viongozi wote wa Wilaya, wajue zoezi la urasimishaji halina mwenyewe. Watu wamejenga kwenye maeneo yasiyopangwa nchi nzima mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kila wilaya ijpange ihakikishe inawaokoa wananchi wao katika maeneo yale yasiyopangwa yanayoitwa makazi holela wayapange ili waweze kupata Hati, iwaongezee mzunguko wa fedha,

kipato kwa sababu watu wakipangiwa, wakipewa hati, wataingia benki, watazitoa zile hela za mabenki zitakuja mtaani, zitaongeza mzunguko wa fedha katika Halmashauri. Kwa hiyo, zoezi la urasimishaji ni la wote na viongozi wa Wilaya tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kwamba jambo hili linafanyika vizuri kama walivyofanya wenzetu wa Nyamagana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mheshimiwa Shekilindi, tukipata Wenyeviti wengine wa Mabaraza, tumeahidiwa tutarekebisha upungufu tunaopata kule Lushoto. Suala la upimaji, nafikiri halmashauri yake lazima ijjipange. Kama watu hawana Hati, basi ni uzembe wa Halmashauri yake. Kwa sababu Wizara haiwezi kwenda kupanga na kupima kila mahali, lazima tujipange tufanye wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Mgumba, ni kweli leo amenipa siri kwamba Morogoro walini piga changa la macho. Nitakwenda tena na kabla sijaenda nitashirikiana naye ili aniambie siri hiyo. Ni kweli yapo matatizo Morogoro, nakiri kabisa, lakini kwa sababu ya muda, nafikiri kwa sababu amenipa kidogo ufunguo, tutakwenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kigola, nimeshamwambia. Mheshimiwa Malecela Kilango amenialika kule, mimi nakwenda katika hizo Kata zote mbili. Mheshimiwa Lupembe amenialika Katavi, nitakwenda. Nikitoka Tabora nataka kwenda Katavi na nitakwenda na Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ili twende kuangalia hilo eneo mgogoro kati ya maeneo ya ulinzi na ardhi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema nawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, hatuna nafasi ya kuwataja kwa majina lakini wamechangia kwa maandishi na wengine kwa kusema. Mengine yaliyotoka kwenye Kamati ni maelekezo yetu. Haya yote waliyoyasema yametusaidia sasa kupanga ratiba ya kazi na Mheshimiwa Naibu Waziri. Kutokana na hayo waliyoandika na waliyoyasema sasa tumejua twende wapi. Tutawafikia kwenye Wilaya zao ili mtufafanulie zaidi. Kabla hatukwenda

### **NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

tutahakikisha tutawatafuta kwa simu ili tushiriki wenyewe kwenye Mikutano katika Wilaya zao. Tungependa wafunguke zaidi tukiwa pale ili angalau tushirikiane katika kukomesha hii migogoro katika maeneo yenu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisisitiza mambo matatu ya mwisho. Nataka kusisitiza kwa wananchi wote na viongozi na wananchi kwamba ulipaji wa kodi ni suala la kisheria, tumeongeza muda, hatuongezi tena, naomba wananchi wote walipe kodi. Baada ya mwezi nilioutangaza, sasa wale ambao wana malimbikizo wataanza kupelekwa Mahakamani kuanzia mwezi wa Sita. Naomba tulipe kodi kwa maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ziko taasisi za Serikali ambazo tunafikiri hazifanyi biashara kuzifutia madeni haya, lakini pia kuziangalia namna ya ulipaji wao wa kodi. Hatuwezi kutoza kodi kwenye Zahanati, Shule za Msingi na Shule za Sekondari ambazo hazitengenezi faida. Vile vile viro Vyuo na Taasisi za Serikali ambazo zimeomba zifutiwe, lakini zinafanya biashara. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mnataka kufutiwa. Tutaangalia ardhi ambayo mnaitumia kwa mabweni na kwa madarasa, lakini yale maeneo mnayofanya *Mlimani City* tutawatoza kodi. Kwa hiyo, siyo kwamba kila Taasisi ya Serikali tutaisamehe. Yale maeneo ambayo mnatoza hela na sisi tutatoza kodi. Yale ambayo mnafanya bure nasi tutawasamehe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nizungumzie habari ya urasimishaji. Nimesema nawaombeni viongozi wote tushirikiane tufanye suala hili la urasimishaji, lakini *partners* wa urasimishaji makampuni binafsi lazima tuwe na nidhamu katika kufanya jambo hili. Imeonekana kama jambo hili sasa halina mwenyewe, mnaingia ingia hovyo, wasio na sifa na wenyewe sifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeagiza bodi zangu zote zinazoshughulika na upimaji na upangaji zisimamie na kuhakikisha zinayafuatilia makampuni binafsi yanayokwenda kufanya kazi hii kwa kukiuka utaratibu. Jana nilisema,

wananchi wanachanga wenyewe gharama za urasimishaji, Serikali haichangii, lakini fedha zile zisiende mikononi kwa kampuni, zikae kwenye kikundi cha urasimishaji.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Dakika tatu.

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA**

**MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema nawaomba sana Halmashauri zote zisimamie suala la matumizi bora ya ardhi. Kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji na miji ni kazi yetu wote. Naahidi kama nilivyosema, vifaa vya upimaji tutavisambaza kwenye kanda ili Halmashauri ivitumie. Lengo ni kupunguza gharama kwa wananchi ili kasi ya upangaji na upimaji iende kwa kasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, narudia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kama nilivymoshukuru mwanzo kwa kasi na ushauri mbalimbali ambao amekuwa anatupa. Sisi tunafanya kazi na pongezi hizi, lakini mjue kuna mtu anatusukuma tunafuata *vision* yake na mnajua aliwahi kuwa Wizara hii na kasi yake, *vision* yake tunaifuata. Tunamshukuru sana kwa msukumo na ushauri wa mara kwa mara ambao anatupatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaahidi kwamba baada ya bajeti hii, tutapanga ratiba ili tupate fursa ya kuwatemeblea Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ratiba yenu sasa tumeshaipanga kulingana na kero mbalimbali mlizotupatia hata ambao wameandika kwa maandishi tumeona kero zao. Tumejipanga, mpaka mwezi wa Saba ninyi wenyewe mtakuwa mashahidi kwamba kweli mlikuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makofii*)

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,  
WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono.  
Katibu.

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI-KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 48 - Wizara ya Ardhi, Nyumba  
na Maendeleo ya Makazi**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na utendaji mzuri wa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Timu yake, hakuna chama chochote kimeleta majina ya Waheshimiwa Wabunge kutaka kutoa shilingi kuzuia mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nakupongeza kabla hata hujamaliza bajeti yako. (*Makofi*)

Kif. 1001 – <i>Admin.and HR Mgmt</i> .....	Shs. 9,633,588,821/=
Kif. 1002 – <i>Finance and Accounts</i> .....	Shs. 841,980,000/=
Kif. 1003 – <i>Policy and Planning</i> .....	Shs. 812,598,000/=
Kif. 1004 – <i>Management Inform. System</i> ....	Shs. 921,076,000/=
Kif. 1005 - <i>Internal Audit Unit</i> .....	Shs. 343,620,000/=
Kif. 1006 – <i>Procurement Mg'nt Unit</i> .....	Shs. 305,712,000/=
Kif. 1007 – <i>Gov't Comm.Unit</i> .....	Shs. 380,304,000/=
Kif. 1008 – <i>Legal Service Unit</i> .....	Shs. 420,280,000/=
Kif. 2001 – <i>Land Administration Division</i> ....	Shs.3,986,488,000/=
Kif. 2002 – <i>Surveys and Mapping Division</i> ...Shs.3,508,696,000/=	
Kif. 2003 – <i>Registration of Titles Unit</i> .....	Shs.1,008,624,000/=
Kif. 2004 – <i>Valuation Unit</i> .....	Shs. 867,024,000/=
Kif. 2005 – <i>Dar es Salaam Zone</i> .....	Shs. 509,245,500/=
Kif. 2007 – <i>Central Zone</i> .....	Shs. 511,140,000/=
Kif. 2008 – <i>Western Zone</i> .....	Shs. 414,730,000/=
Kif. 2009 – <i>Lake Zone</i> .....	Shs. 538,620,000/=
Kif. 2010 – <i>Northern Zone</i> .....	Shs. 532,160,000/=
Kif. 2011 – <i>Southern Zone</i> .....	Shs. 429,430,000/=
Kif. 2012 – <i>Southern Highlands Zone</i> .....	Shs. 402,610,000/=
Kif. 2013 – <i>Simiyu Zone</i> .....	Shs. 432,440,000/=

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Kif. 3001 – *Rural & Town Planning Div.*.....Shs.2,876,691,656/=  
Kif. 3002 – *Housing Division*.....Shs.2,021,855,661/=

*(Vifungu viliviyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3003 – *District Land &  
Housing Tribunal Unit*.....Shs.3,752,832,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufanuzi kwenye fungu hili, *Sub Vote 21114*, naona yaani fedha zimekuwa nyingi sana. Mwaka uliopita kwanza ilikuwa zero na mwaka 2016/2017 ilikuwa shilingi milioni tisa, lakini sasa hivi imekuja shilingi milioni 165.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO  
YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa swali lake. Napenda tu kumfahamisha kwamba kifungu hiki linaonekana kweli kina pesa nyingi lakini fedha hizi zimetengwa kwa ajili ya kuwalipa waajiriwa wa muda ambao wanafanya kazi kwenye Mabaraza yetu ya Ardhi kwa sababu Mabaraza mengi yana upungufu wa Watumishi, lakini pale ambapo kunakuwa na kazi kubwa inabidi pia zifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo, tengeo hili ilikuwa kwenye kifungu kingine ambacho kilikuwa ni tofauti na hiki kwa maana ya *basic salary*. Ilikuwa kwenye kifungu 21112, kwa hiyo, imewekwa katika fungu moja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 – Tume ya Taifa ya Mipango  
ya Matumizi ya Ardhi**

Kif. 1001 – *Finance & Admin. Division*.....Shs.1,072,746,000/=

**NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)**

Kif. 1002 – *Planning Unit*.....Shs. 94,180,000/=  
Kif. 1003 – *Procurement and Mg'nt*.....Shs. 78,980,000/=  
Kif. 1004 – *Internal Audit Unit*.....Shs. 55,780,000/=  
Kif. 1005 – *Legal Service*.....Shs. 46,382,500/=  
Kif. 2001 – *Physical Planning Division*.....Shs. 316,880,000/=  
Kif. 2002 – *Land use Coordination,  
Comm. & Policy Division*.....Shs. 162,800,000/=  
Kif. 2003 – *Research and Documentation*..Shs. 254,177,500/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 48 – Wizara ya Ardhi, Nyumba na  
Maendeleo ya Makazi**

Kif. 1001 – *Administration & HR Mgmt*.....Shs. 1,100,000,000/=  
Kif. 2001 – *Land Admin. Division*.....Shs. 21,537,602,000/=  
Kif. 2002 – *Surveys and Mapping Div*..... Shs. 7,400,000,000/=  
Kif. 3002 – *Houseing Division*.....Shs. 500,000,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**Fungu 03 - Tume ya Taifa ya Mipango  
ya Matumizi ya Ardhi**

Kif. 2001 – *Physical Planning Division*.....Shs. 5,000,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu killipitishwa na Kamati  
ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati  
ya Matumizi imemaliza kazi yake.

*(Bunge lilitrudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae. Mtoa hoja. *(Makof)*

## TAARIFA

### **WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA**

**MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na heshima kubwa tuliyonayo kama Wizara kwa Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na kwako Mwenyekiti na Wenyevitit wote, Kamati yetu na Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi zake. Naomba Taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante hoja imeungwa mkono. Waheshimiwa sasa nitawahoji. (*Makofii*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe  
(Hoja ilihamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka  
2018/2019 – Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi  
yaliiidhinishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana na Naibu wako pamoja na Katibu Mkuu, Kamishna Mary na Timu yenu kwa kazi nzuri mnazofanya, kwa kweli mnastahili pongezi. Mabadiliko makubwa sana yapo kwenye Wizara hii. Nchi hii katika mipaka yetu migogoro mingi imeshuka kwa asilimia kubwa sana. Kwa hiyo *you are doing a very good job.*

Mkurugenzi wa *National Housing*, maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu umeyasikia. Upo kwanza ndani eeh? Yumo? Aah upo huko eeh! Umesikia maagizo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, kaa na Kamati ile ya wapangaji, mimi sina shida ya Stakabadhi Ghalani wala pembejeo, shida kwangu ni nyumba, ndiyo agenda zangu za Ubunge. Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kuwauzia na

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

mwachane na hayo mambo ya kupandisha kodi holela; kila mkiamka asubuhi kodi kodi kodi. Hawa ni Watanzania hawana uwezo huo. (*Makofi*)

Baada ya maneno hayo machache, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kazi nzuri, tumemaliza kazi mapema kwa sababu taratibu zote zimefuatwa, lakini hii ni Wizara ya mfano kabisa. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.00 mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 31 Mei, 2018, Saa Tatu Asubuhi)*